TOKA

SABATO

KWENDA

JUMAPILI

CARLYLE B. HAYNES

# TOKA

# SABATO

# KWENDA

# JUMAPILI

Mjadala wa kihistoria wa Hoja juu ya Sabato, Ukionyesha Jinsi Gani, Lini, Kwa Nini, na Ni Nani aliyefanya Badiliko hilo kutoka Siku ya Saba kwenda Siku ya Kwanza ya Juma.

Mtunzi: Carlyle B. Haynes

Mfasiri: Moses Mwamalumbili

(From Sabbath to Sunday - Kiswahili)

YALIYOMO

Badiliko katika Utunzaji wa Sabato.................................................................

Sabato ya Biblia............................................................................................

Hakuna Kibali cha Mungu kwa Badiliko hili.....................................................

Kwa Jinsi Gani, Kwa Nini, na Ni Hani Aliyefanya Badiliko hili.......................

Siku ya Saba ni ile ile.................................................................................

Badiliko la Kalenda...........................................................................................

Msimamo wa Uprotestanti.................................................................................

Unabii wa Kale unaohusu Utunzaji wa Sabato Siku Hizi.................................

Kuuyakamilisha Matengenezo Yaliyositishwa...............................................

Kwenda Nuruni.................................................................................................

# SURA YA 1

## BADILIKO KATIKA UTUNZAJI WA SABATO

Mahali fulani katika zama za giza katikati ya siku zile za Kristo na siku zetu, utunzaji wa Sabato umebadilishwa kutoka siku ya saba ya juma kwenda siku ya kwanza.

Ni hakika ya kwamba amri ya Mungu inahusu kuitakasa na kuitunza siku ya saba kama Sabato. Hakuna uwezekano wo wote wa kukosa kuelewa maana yake hapa. Amri ni hii:

"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya sabato akaitakasa." (Kutoka 20:8-11).

Pia ni hakika kwamba hakuna amri nyingine yo yote iliyotolewa katika Maandiko Matakatifu inayoitaja siku nyingine au siku iliyo tofauti na hii. Biblia, katika utimilifu wake wote, yaani, Agano la Kale na Agano Jipya, inaamuru, inathibitisha, inatetea, na kufundisha utunzaji wa siku ya saba kama Sabato. Vivyo hivyo ni kama ilivyo hakika kwamba makanisa mbalimbali yenye waumini Wakristo leo hii katika kila sehemu ya ulimwengu huu, ukiacha tofauti chache mno zilizo za muhimu, wanaitunza siku ya kwanza ya juma kwa pamoja, nao wanajiunga pamoja katika kuutetea utunzaji wake

Basi, inaonekana ya kwamba kuna dosari kati ya uzoefu wa siku hizi wa makanisa mengi katika suala hili la utunzaji wa Sabato na yale mafundisho yaliyo wazi kabisa ya Biblia. Dosari hii inayoonekana wazi imeyasumbua mawazo ya wengi, na kufanya iwepo haja halisi ya kupata maelezo sahihi na yanayoaminika juu ya historia ya nyuma inayohusu badiliko hili katika utunzaji wa Sabato, wakati gani badiliko hili lilitokea, na sababu za kufanya badiliko hili. Kwa hiyo, inashauriwa hapa kwamba tuingie katika utafiti wa somo hili kwa tumaini la kutoa maelezo yatakayomwezesha kila msomaji kuufikia uthibitisho dhahiri wa kweli hii na wajibu huu kiasi cha kumwondolea mashaka yote na kuchanganyikiwa kwake.

Katika utafiti kama huu, kwa kweli, itakuwa ni lazima kwetu kudadisi chanzo cha utunzaji wa Sabato, pamoja na kuyachunguza maandiko yanayoonyesha historia ya kanisa na sababu za kuibadili siku hiyo. Kwa hiyo itatupasa kutafakari kwa makini maelezo ya Biblia yahusuyo kuanzishwa kwa Sabato miongoni mwa wanadamu, na sababu zitokanazo na fikara zake Mungu kwa kuamuru itunzwe katika mojawapo ya amri zake kumi.

## SHERIA ILINENWA NA KUANDIKWA NA YEHOVA

Sheria pekee ya Mungu inayojulikana miongoni mwa wanadamu iliyoagiza utunzaji wa Sabato inapatikana katika Biblia, nayo imekwisha kudondolewa katika ukurasa huu. Ingetupasa kuonyesha wazi ya kwamba amri hii ilinenwa, pamoja na amri zile nyingine tisa, kwa kinywa chake Yehova Mwenyewe.

"BWANA [YEHOVA] akasema nanyi kutoka kati ya moto; mkasikia sauti ya maneno, lakini hamkuona umbo lo lote; sauti tu. Akawahubiri agano lake, alilowaamuru kulitenda, yaani, zile amri kumi; akaziandika juu ya mbao mbili za mawe." (Kumbukumbu la Torati 4:l2,l3).

Amri hizi kumi, ikiwamo amri hii ya Sabato, ziliandikwa kwa kidole cha Mungu Mwenyewe juu ya jiwe la kudumu. "Akaziandika juu ya mbao mbili za mawe." (Kumbukumbu la Torati 4:l3). "Mbao mbili za ushuhuda, mbao mbili za mawe, zilizoandikwa kwa chanda [kidole] cha Mungu." (Kutoka 3l:l8).

Sheria hii inasemwa katika Maandiko kuwa ni "ya haki," "ya kweli," "nzuri," na "kamilifu." "Tena ulishuka juu ya mlima Sinai, ukasema nao toka mbinguni, ukawapa hukumu za haki, na sheria za kweli, na amri nzuri na maagizo." (Nehemia 9:l3). "Sheria ya BWANA ni kamilifu" (Zaburi l9:7).

Sheria hii inao wajibu wote umpasao mwanadamu.

## KRISTO HAKUBADILI SHERIA

Halikuwa kusudi lake Kristo kubadili, kuondoa, kutangua, wala kuibatilisha sehemu yo yote ya sheria hii. "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza." (Mathayo 5:l7).

Badala ya kuitolea sheria hiyo sifa mbaya, Kristo alikuja kuifanya iadhimishwe. "BWANA akapendezwa kwa ajili ya haki yake, kuitukuza sheria na kuiadhimisha." (Isaya 42:21).

Naam, kwa kadiri Sabato inavyohusika, Kristo aliitunza, pamoja na kila amri nyingineyo. "Siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake." (Luka 4:l6).

Kusema kweli, imani kwa Kristo, badala ya kuiweka sheria kando, inaithibitisha na kuiimarisha. "Basi, je! twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! kinyume cha hayo twaithibitisha sheria." (Warumi 3:3l).

Sheria hii ya Mungu, ambayo ndani yake imo amri ya Sabato, inatangazwa na Paulo kuwa ni "ya rohoni," "takatifu," "ya haki," na "njema." "Kwa maana twajua ya kuwa torati [sheria]

asili yake ni ya rohoni" (Warumi 7:l4). "Basi torati [sheria] ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema." (Warumi 7:l2).

Sheria hii ni lazima ishikwe kama sharti la kupata uzima wa milele. "Heri wale wazishikao amri zake, wawe na haki kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake." (Ufunuo 22:l4, Tafsiri ya King James Version).

Naam, hiyo ndiyo kanuni, au kipimo, ambayo kwayo ulimwengu wote utahukumiwa. "Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru." (Yakobo 2:l2).

. SHERIA BADO INA NGUVU

Kwa hiyo, linaonekana kuwa ni jambo la ajabu kwamba utunzaji kama huo wa Sabato ungekuwa umebadilishwa hata kidogo. Sheria hii ya Mungu bado ina nguvu. Sheria hii inaamrisha utunzaji wa siku ya saba ya juma. Lakini siku hiyo haitunzwi hivi sasa na watu wengi mno wanaokiri ya kwamba wao ni watu wa Mungu. Hata hivyo, sheria hii haibadiliki, bado ina nguvu, na hiyo ndiyo kipimo cha hukumu yake Mungu.

Siku nyingine imewekwa badala ya siku iliyoamriwa. Siku hiyo ilitoka wapi? Kwa nini imewekwa badala ya ile iliyokuwapo? Je, utunzaji wa siku hii [nyingine] unakubalika na Mungu?

Haya ndiyo maswali ambayo sasa sisi tutayashughulikia.

## SURA YA 2

## SABATO YA BIBLIA

Mwasisi wa Sabato ndiye Mwasisi wa dini ya Kikristo ----- Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

Yeye ndiye aliyeiumba dunia hii, akiifanya kwa siku sita. Yeye ndiye aliyestarehe siku ile ya saba, na kuibarikia siku ile, na kuitakasa. Kwa maana Mwana wa Mungu alikuwa na hata sasa ndiye Muumbaji. "Vyote vilifanyika kwa huyo."

"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo Yeye hakukufanyika cho chote kilichofanyika" (Yohana l:l-3). "Alikuwako ulimwenguni, hata kwa Yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua" (Fungu la l0). "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli" (Fungu la l4).

"Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia Yake, na kwa ajili Yake" (Wakolosai l:l5,l6).

Kama tulivyokwisha kuona tayari, wakati alipoifanya Sabato ulikuwa ni mwishoni mwa juma lile la uumbaji. (Mwanzo 2:l-3).

Njia aliyoitumia kuifanya Sabato ilikuwa kwa kuchukua siku moja, siku ile ya saba, na Yeye Mwenyewe kustarehe siku hiyo, kuibarikia, na kuitakasa.

## SABATO NI SIKU, SIO KANUNI

Kifaa alichotumia kuifanya Sabato ni siku ile ya saba. Akaitwaa siku ile, na kuifanya Sabato. Sabato sio kitu fulani alichokiweka juu ya siku ile. Ni siku ile yenyewe. "SIKU ya saba ni sabato ya BWANA, Mungu wako."

Hatuamriwi kwamba tu"ikumbuke SABATO t[]uitakase." Amri inasema hivi: "Ikumbuke SIKU ya sabato uitakase." Sabato si kitu fulani kilicho tofauti na siku hiyo, ambacho kinaweza kusogezwa huku na huko na pengine kuwekwa juu ya siku nyingine. Ni siku yenyewe hasa, siku ile ya saba.

Siku hizi tunasikia mengi juu yaKANUNI ya Sabato. Lakini Biblia haizungumzi kamwe juu ya KANUNI ya Sabato. Hakuna kitu kama hicho cha KANUNI ya Sabato iliyobarikiwa na kutakaswa kwa faida ya binadamu, mbali na siku yenyewe.

Ilikuwa ni SIKU yenyewe ambayo ilibarikiwa kwa kutakaswa; na kwa sababu hiyo ni SIKU hiyo ambayo inakuwa Sabato.

Siku ile aliyoibarikia Mungu kamwe haiwezi kutenganishwa na Sabato. Nayo Sabato haiwezi kamwe kuondolewa kutoka katika siku ile aliyoibarikia Mungu. Vitu hivi viwili haviwezi kutenganishwa. Havitengeki kwa sababu siku zote viko pamoja.

SIKU YA SABA ndiyo Sabato; Sabato ndiyo SIKU YA SABA.

Yesu aliifanya Sabatokwa ajili ya taifa zima la kibinadamu, sio kwa ajili ya kundi moja tu ama taifa moja tu. "Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu" (Marko 2:27).

## SABATO INADUMU MILELE

Mungu aliifanya Sabato kwa ajili ya wakati wote. Haikukusudiwa kuwa ya muda tu, bali ya milele. Kamwe hapatakuwa na wakati wo wote ambapo siku hii ya saba haitakuwa siku iliyobarikiwa, siku ya Mungu ya kupumzika. "Maagizo [amri] yake yote ni amini. Yamethibitika milele na milele (Zaburi lll:7,8).

Hata katika nchi mpya Sabato ya siku yasaba iliyobarikiwa itaendelea kutunzwa na mataifa ya wale waliookolewa. "Na itakuwa ... Sabato hata Sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema BWANA" Isaya 66:23).

Sababukwa nini Mungu aliwaamuru wanadamu kuitunza siku ya Sabato ni hii: "Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya sabato akaitakasa" (Kutoka 20:ll).

Kwa hiyo, Sabato ni kumbukumbu ya uumbaji wa nchi hii kwa siku sita, naye Mungu ameiweka kama ishara ya uweza Wake wa Uumbaji. Kwa njia ya kuitunza Mungu alikusudia kwamba mwanadamu angemkumbuka Yeye daima kama Mungu wa kweli na wa pekee, Muumbaji wa vitu vyote.

## ISHARA YA UTAKASO

Uwezawa Mungu wa uumbaji ulitumika kwa mara ya pili katika kazi yake ya ukombozi, ambayo kwa kweli ni uumbaji mpya. Sabato kama kumbukumbu ya uweza wa uumbaji inakuwa kumbukumbu ya wokovu wetu katika Kristo. Iliwekwa dhahiri kama ishara ya utakaso. "Tena naliwapa sabato zangu, ziwe ishara kati ya Mimi na wao, wapate kujua ya kuwa Mimi, BWANA, ndimi niwatakasaye" (Ezekieli 20:l2).

Kama Kristoalivyo Mmoja awatakasaye watu Wake, hivyo ndivyo Sabato inavyokuwa ishara ya vile Kristo alivyo kwa yule aaminiye. Ni kumbukumbu ya pumziko letu kutoka dhambini, kumaliza kazi Yake ya wokovu kamili ndani yetu. Kumbukumbu kama hiyo inadumu milele hata milele.

Ni Yesu anayeokoa kutoka dhambini. Wokovu huu kutoka dhambini ni utendaji halisi wa uweza wa Mungu wa uumbaji. Ni kwa njia ile tu ya uweza ulioletwa na Roho Mtakatifu kwa wenye dhambi, inaweza kushindwa dhambi katika mwili wa mwanadamu, na mwanadamu huyo kuweza kuingia katika pumziko hilo la imani. Ni Yesu anayetoa pumziko hilo.

"Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, NAMI NITAWAPUMZISHA" (Mathayo ll:28).

## ISHARA YA UKOMBOZI KUTOKA DHAMBINI

Ishara ya uweza wa Kristo wa uumbaji ni Sabato. "Sabato maana yake pumziko. Ilitolewa sio tu kwa ajili ya pumziko la kimwili, bali kama ishara ya pumziko la kiroho na ukombozi kutoka dhambini. Kwa hiyo yule anayeitunza Sabato kwa akili ameingia katika raha yake Mungu, "Yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Yake" (Waebrania 4:l0).

Kwa njia hii Sabato, kwa yule aaminiye katika Kristo, inakuwa ishara ya yote yale ambayo Injili inayo kwa ajili yake katika Kristo.

## MWANZO NA MWISHO WA SABATO

Sabato inaanza jua linapozama na kuisha jua linapozama [kesho yake]. Njia ya Biblia ya kuhesabu siku sio kuanzia usiku wa manane mpaka usiku wa manane [kesho yake], bali ni kutoka jioni hata jioni [kesho yake]. Jua linapozama siku inakwisha, na siku mpya inaanza. Jioni ndio mwanzo wa siku. "Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja" (Mwanzo l:5). Yaani, jioni, au sehemu ya siku yenye giza, inakuja kwanza, nayo inafuatiwa na asubuhi, au sehemu ya siku yenye mwanga.

Agizo la Mungu ni kwamba, "tangu jioni hata jioni, mtaishika hiyo sabato yenu" (Mambo ya Walawi 23:32)

"Jioni" inaanza jua linapozama. "Jioni, katika machweo ya jua" (Kumbukumbu la Torati l6:6). "Jioni, na jua limekwisha kuchwa" (Marko l:32).

Kwa hiyo, jua linapozama jioni siku ile ya sita ya juma, huo ndio mwanzo wa Sabato ya Mungu. Ijumaa jioni jua linapozama huo ndio mstari unaogawa wakati mtakatifu."BWANA AKAIBARIKIA siku ya Sabato AKAITAKASA" (Kutoka 20:ll).

Ni wakati huo mtakatifu tunaoagizwa kwamba tuu"kumbuke" ili ku"[u]takas[a]." Mungu aliifanya TAKATIFU; anamwamuru mwanadamu KUITAKASA.

## KUSUDI LA KUITUNZA SABATO

Kuitakasa Sabato ni kuitumia kwa kusudi lile lile iliyowekewa. Ilikusudiwa kuwa siku ya ibada kwa wote pamoja na maombi ya faragha. "Siku ya saba ni sabato ya kustarehe kabisa, KUSANYIKO TAKATIFU" (Mambo ya Walawi 23:3). Tunacho kielelezo cha Yesu Mwenyewe akihudhuria ibada siku ya Sabato: "Na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi Yake" (Luka 4:l6).

Maandalio ya kuitunza vizuri Sabato ni pamoja na kupika chakula na kuandaa vitu vingine vinavyoweza kuhitajika ili kuwa tayari kuacha kufanya kazi za kawaida, za kidunia wakati Sabato inapoanza, na kuutumia muda wetu kwa mambo matakatifu, ya mbinguni (Kutoka l6:22,23; Luka 23:54).

Sabato sio siku ya kufanya kazi za kawaida, wala uzembe, wala burudani. Ni kwa ajili ya kupumzika, kiroho na kimwili; kwa ajili ya kutafakari; ibada ya faragha na ya wote; kwa ajili ya furaha takatifu, na kwa kusaidiana. Ilikusudiwa kuwa siku ya furaha, uchangamfu, na bora kuliko zote katika zile siku saba.

## NI MSINGI WA UKAMILIFU WA EDENI

Ni mojawapo ya mambo mawili yaliyosalia ya maisha yale ya Edeni ambayo yameendelea kuwako tangu Anguko lile, jingine ni ndoa, na, kwa hiyo, ni mojawapo ya kanuni za awali za Edeni. Siku hii ya mapumziko hutokea kila juma, ili kuweka mbele yetu daima ukweli wa kustarehe kwake Mungu mwishoni mwa juma lile la Uumbaji. Tunapaswa kumkumbuka Mungu kila siku, lakini Sabato inakuja kwetu kila juma, ikituletea nafasi nyingi za kupumzika, kutafakari, na kuzungumza na Muumbaji wetu. Kabla haijapoteza mibaraka yake na mambo yake ya thamani, kuja kwa Sabato nyingine huufanya mpya mvuto wake utakasao. Hivyo inazifanya siku zote kuwa za kupendeza na kuueneza mbaraka wake katika saa zetu zote, basi, na tu"IKUMBUKE siku ya sabato [t]uitakase."

## SABATO YA AGANO JIPYA

Agano Jipya halibadilishi hata kwa kiwango kidogo mno wajibu wetu wa kuitunza siku ya saba iliyoamriwa na Mungu. Kristo aliitunza siku hii katika kipindi chote cha maisha Yake hapa duniani. Wanafunzi wake waliitunza barabara siku hii katika kipindi chote cha maisha yao, wakati wanaanzisha makanisa ya Kikristo ya mwanzo. Hakuna tukio

hata moja katika kumbukumbu za Agano Jipya ambapo binadamu awaye yote alijaribu kuitunza siku ya kwanza kama Sabato.

Sabato ya Agano Jipya ni Sabato ile ile ya Agano la Kale, yaani, siku ya saba ya juma.

# SURA YA 3

## HAKUNA KIBALI CHA MUNGU KWA BADILIKO HILI

Yesu Kristo hakubadili Sabato. Yeye kama Muumbaji aliifanya ili iendelee kuwako. Aliiweka iwe kumbukumbu ya Uweza Wake katika kazi Zake zote mbili za Uumbaji na Ukombozi. Alipokuja duniani kulitekeleza kusudi lile la milele la wokovu wa wanadamu, ni shida mno kuweza kufikiria kwamba angeweza kuiweka kando kumbukumbu hiyo ambayo ni Yeye Mwenyewe aliyeianzisha kwa ajili ya kuadhimisha kazi Yake ya ukombozi iliyokuwa imekamilika.

Wanafunzi wake Kristo na makanisa yale ya kwanza ya Kikristo hawakupata kusikia kitu kama hicho cha badiliko lililofanywa na Mungu kuhusu utunzaji wa Sabato. Kwa hiyo, utunzaji wa siku nyingine yo yote kama Sabato mbali na ule wa siku ya saba hautambulikani katika Agano Jipya. Utunzaji wa siku ya Jumapili na waumini wa Kikristo chimbuko lake ni la baadaye sana kuliko kipindi kile cha Biblia.

Naam, hakuna sehemu ndogo hata moja ya mahubiri ya hadhara na kazi Yake Kristo ambayo haionyeshi kitu gani ni halali na cha haki kutendwa katika siku ile ya saba, jambo ambalo ni gumu sana kulieleza kwa wale wanaodai kwamba wanasadiki [Kristo] aliitangua Sabato.

Utunzaji wa Sabato wa Wayahudi wa siku zile za Kristo ulikuwa haufanani kabisa na ule ambao Mungu alikusudia. Mbali na kuwa mbaraka, [Sabato] ikawa mzigo mzito.

Shetani alikuwa amefanya kila aliloweza kwa njia ya majaribu yake yapotoshayo kuwafanya Wayahudi waache kuitunza Sabato. Katika jambo hilo alifanikiwa kwa sehemu tu. Mungu akawaacha watu wake kwenda utumwani kule Babeli kwa sababu ya dhambi zao, ambazo zilikuwa ni pamoja na kuivunja Sabato. Mara tu waliporudi toka utumwani, Wayahudi hao waliazimu kuitunza Sabato kwa uaminifu sana kama Mungu alivyoamuru. Lakini yule Mwovu akaamua kuwatega [kuwanasa] tena, naye alifanikiwa kwa kuwaongoza kuipotosha maana na kusudi la Sabato, mpaka ikajazwa na masharti mengi yaliyokuwa mzigo mzito uliowalemea watu.

Yesu alipojitokeza kama Mwalimu wa watu miongoni mwa Wayahudi, hakupoteza nafasi hata moja kuzisahihisha dhana [fikara] potofu juu ya Sabato. Alilitumia kila tukio kuiweka huru siku hiyo mbali na sheria zile zilizotungwa na wanadamu ambazo zilikuwa mzigo mzito uliowalemea watu.

## MIUJIZA SIKU YA SABATO

Naam, alizitumia vizuri nafasi hizo, maana kwa makusudi mazima aliichagua Sabato kama siku ya kufanya miujiza Yake mingi pamoja na matendo yake ya huruma.

Kule Kapernaumu, akiwa ndani ya sinagogi siku ile ya Sabato, alimtoa "roho ya pepo mchafu" kutoka ndani ya mtu yule aliyekuwa amefungwa na pepo huyo. Baadaye, Sabato ile ile, alimponya "homa kali" yule "[mkwewe Simoni], mamaye mkewe." (Angalia Luka 4:30-39.)

Matendo kama hayo yaliyofanyika siku ya Sabato yaliangaliwa kwa swali kubwa na Wayahudi, maana hawakutaka kumletea wagonjwa wao siku ya Sabato, bali walingoja mpaka "jioni, na jua limekwisha kuchwa." (Angalia Marko l:32-34; Luka 4:40.)

Hata hivyo, Yesu aliendelea tu kuyasahihisha mawazo yao kuhusu nini kilichofanya utunzaji wa Sabato uwe sahihi, naye aliendelea kufanya matengenezo katika utunzaji wa Sabato. Ili kuwajulisha ukweli wa suala hilo alizungumza nao kama mtu aliye na mamlaka, akiitumia nafasi ile ya tukio la wanafunzi wake walipovunja masuke ya ngano siku ile ya Sabato, aliwatangazia ya kwamba "Mwana wa Adamu ndiye Bwana [Yehova] wa Sabato." (Angalia Mathayo 12:l-8.) Katika jambo lilo hilo aliwapa mafundisho ya kuwasaidia juu ya desturi ya utunzaji sahihi wa Sabato.

## YESU ALIJITOA MAISHA YAKE MHANGA KUIWEKA HURU SABATO

Lilikuwa ni jambo la muhimu sana kwake kuiweka huru Sabato mbali na mapokeo yao potofu waliyoizungushia, ambayo yalifika mbali sana kiasi cha kuzuia kufanya tendo lo lote la kuwaponya wagonjwa siku ile, hata Kristo ikabidi asimame kwa ushujaa kupinga ukorofi huo wa Mafarisayo na kujitoa maisha Yake mhanga ili kuiweka huru Sabato mbali na vizuio [masharti] potofu walivyoviweka. Wakati alipomponya mtu yule aliyekuwa amepooza mkono wake katika sinagogi siku ile ya Sabato, na kuhusiana na jambo hilo akatoa mafundisho mengi yaliyohitajika juu ya utunzaji sahihi wa siku hiyo, Mafarisayo, kwa hasira, "wakafanya shauri juu yake jinsi ya kumwangamiza." (Angalia Mathayo 12:9-14.)

Alimponya mtu yule aliyepooza penye birika lile la Bethzatha, Alimponya udhaifu wake wa muda wa miaka thelathini na minane. Kitendo hicho kilipolalamikiwa, na Wayahudi walipomwudhi Yesu na "kutaka kumwua," Aliitumia tena nafasi hiyo kuwapa mafundisho sahihi kuhusu utunzaji wa Sabato, akisema, "Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi." (Angalia Yohana 5:1-19.)

Miezi kadhaa baadaye kisa hicho hicho cha uponyaji kilijadiliwa, naye aliwafafanulia tena maadui zake maana ya Sabato. (Angalia Yohana 7:21:23.)

## KUIOKOA SABATO NA MZIGO ULEMEAO WA MASHARTI YAKE

Hata hivyo, Wayahudi walikataa kupokea mafundisho hayo, naye Bwana akaona ni lazima aendelee na kazi Yake kwa ajili ya Sabato, kazi ile ya kuiokoa kutoka katika upotoshaji

uliokuwa umefichwa kwa watu wengi bila kuwaonyesha kusudi lake halisi na kuwazuia wengi wasiweze kuipata mibaraka ya kiroho na raha.

Siku ya Sabato alimkuta mtu mmoja aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa, naye kwa kumhurumia, akatema mate chini, akafanya tope kwa yale mate, akampaka yule kipofu tope za macho, na kumtuma aende akanawe katika birika. Mtu yule akaenda, akanawa, na kurudi akiwa anaona. Kule kufanya tope lile na kule kumponya yule kipofu vilihesabika kama ni uvunjaji wa Sabato na wale maadui zake washupavu wa dini, lakini [tendo lile] lilikuwa ni ukamilifu wa kuitunza Sabato. (Angalia Yohana 9:1-38.)

Baadaye, siku nyingine ya Sabato, alimponya mwanamke mmoja aliyekuwa amefungwa na Shetani kwa miaka kumi na minane, naye alikuwa amepindana, hawezi kujinyosha kabisa. Akapambana na makelele ya wapinzani wake kwa kuwapa mafundisho zaidi juu ya utunzaji sahihi wa Sabato, akiwanyamazisha kabisa na kuwaletea furaha watu waliokuwapo pale. (Angalia Luka 13:10-17.)

Wakati wa chakula cha jioni katika nyumba ya Farisayo mmoja, Alitoa mafundisho ya ziada juu ya namna ya kuitunza Sabato kama ipasavyo, na wakati uo huo akamponya mtu mmoja mwenye ugonjwa wa safura. (Angalia Luka 14:1-6.)

Basi historia ya kazi ya Kristo inamdhihirisha Yeye kama Mtunza Sabato wa kweli. Alifanya juhudi ya kudumu kuyasahihisha makosa yale ya muda mrefu juu ya Sabato, akijitahidi kuiondolea vizuio vyote vilivyowekwa kwa ukali na vilivyowalemea watu kutokana na mapokeo ya Mafarisayo.

Naam, tukiwa tumekabiliwa na kumbukumbu kama hiyo, ni upumbavu kusisitiza kwamba Bwana wa Sabato alikusudia kufutilia mbali utunzaji wa siku hii ya saba. Kama hilo lingekuwa ndilo kusudi lake, basi, asingetumia muda mwingi sana katika kazi yake miongoni mwa watu akiwafundisha watu jinsi ya kuitunza kwa usahihi siku hii.

Si haki kabisa, kusema kwa maneno laini, kwa waalimu Wakristo wa leo kutekeleza kusudi lao la kuigeuza mioyo ya wanadamu ili ipate kuichukia Sabato ya Biblia, kwa kuvifanya vizuio vile vilivyowekwa na ule msimamo mkali wa Mafarisayo kuwa mambo hayo ni sehemu halisi ya Sabato ya Mungu, na kwa njia hiyo kuielewa vibaya juhudi yenye nguvu ya Kristo ya muda mrefu kuwa hiyo ndiyo ushahidi kwamba Yeye [Kristo] alikuwa ameivunja amri ya Mungu ya Sabato na kwamba hiyo ndiyo jitihada yao [waalimu hao] ya kuifanya Sabato yenyewe isikubaliwe na watu. Wale wanaofanya hivyo, kwa kweli, wanachukua msimamo wao kinyume na Bwana wa Sabato, nao wanajiunga pamoja na wale Mafarisayo, wakisema, "Mtu huyo hakutoka kwa Mungu, kwa sababu hashiki Sabato" (Yohana 9:16).

## SIKU YA KWANZA IMETAJWA MARA SITA KATIKA VITABU VYA INJILI

Vitabu vinne vya Injili huitaja siku ya kwanza ya juma mara sita, na katika mafungu hayo wale wanaoitunza siku ya kwanza ni lazima wakipate kibali chao kwa utunzaji kama huo. Vifungu vinavyoitaja siku ya kwanza katika Injili ni hivi: Mathayo 28:1; Marko 16:1,2,9; Luka 23:56 na 24:l; Yohana 20:1,l9.

Hapa, kama kuna mahali pengine po pote, ni lazima kitafutwe kibali kama kipo cho chote ambacho kilitolewa kuhusu utakatifu wa siku ya Jumapili. Mafungu haya yanasema tu juu ya "siku ya kwanza ya juma." Yanaungana pamoja kutangaza kwamba ufufuo wa Bwana wetu ulitokea siku ile. Wanaoitunza Jumapili wanadai kwamba kule kutokea kwa tukio hili siku ile kulileta badiliko la Sabato toka siku ya saba kwenda ile ya kwanza. Kama hivyo ndivyo ilivyo, basi, mafungu haya yangetoa maelezo yaliyo wazi.

Lakini katika kuyachunguza mafungu haya inadhihirika kwamba hayasemi kitu cho chote juu ya badiliko la Sabato. Yanasema juu ya Sabato, ni kweli, lakini yanaainisha [yanatofautisha] kwa uangalifu mkubwa sana kati ya Sabato na siku ya kwanza ya juma, yakiliweka wazi jambo hili kwamba Sabato ya Agano Jipya ni siku ile iliyo kabla ya siku ya kwanza. Hayatoi cheo [sifa] cho chote cha utakatifu kwa siku ile ya kwanza. Yanatoa cheo [sifa] hicho kwa siku ile ya Saba. Hayasemi kwamba Kristo alistarehe siku ile ya kwanza, jambo ambalo lingekuwa la lazima katika kuifanya siku hiyo kuwa Sabato. Hayasemi lo lote kuhusu baraka yo yote kuwekwa juu ya siku ile ya kwanza. Hayatuambii lo lote juu ya Kristo kwamba kuna wakati wo wote aliopata kusema neno lo lote kuhusu siku ya kwanza, aidha kama ni siku takatifu, au vinginevyo. Hayatoi kanuni au amri yo yote kuhusu utunzaji wake [siku ya kwanza]. Hakuna cho chote katika mafungu haya kinachotangaza kuwa siku ya kwanza iangaliwe na wafuasi wake Kristo kama kitu cho chote kile zaidi tu ya kuwa ni siku ya juma ya kawaida kama inavyotajwa ----- ni "siku ya kwanza ya juma" tu.

## HAKUNA KIBALI CHO CHOTE CHA UTAKATIFU WA JUMAPILI

. Baada ya kuyatafakari kikamilifu mafungu yote haya, Kamusi ya Biblia iliyoandikwa na Smith, katika makala yake juu ya "Siku ya Bwana," anakiri kama ifuatavyo:

"Labda yakichukuliwa [mafungu hayo] moja moja, na hata kama yakichukuliwa yote kwa pamoja, mafungu haya kwa shida sana yanaonekana kutosheleza kuithibitisha hoja ya kuitenga siku hii ya kwanza ya juma kwa matumizi ya kidini kwa makusudi yaliyotajwa juu ya kwamba lilikuwa ni jambo lililofanywa na mitume, au hata kwamba ilikuwa ni desturi ya mitume wale." ----- Ukurasa 356.

Kwa hiyo, hakuna ushahidi wo wote katika mafungu haya unaoweza kumfanya mfuasi ye yote wa Bwana wetu kusadiki kabisa kwamba [mafungu hayo] yana kibali kinachosema kwamba siku ya Jumapili ni takatifu.

Badala ya jambo hilo kuwa la kweli kwamba Yesu aliibarikia na kuitakasa siku ya kwanza, ukweli halisi ni kwamba hata mara moja hakupata kuitaja siku ya kwanza kamwe. Wala hakulitamka jina lake [siku ya kwanza] kwa kinywa chake, kwa kadiri tulivyo na kumbukumbu ziwazo zote.

## SIKU YA KWANZA IMETAJWA MARA MOJA KATIKA KITABU CHA MATENDO

Siku ya kwanza ya juma imetajwa katika sehemu nyingine mbili tu katika Agano Jipya. Ya kwanza kati ya hizo imo katika kitabu cha Matendo ya Mitume: "Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane. Palikuwa na taa nyingi katika orofa ile tulipokuwa tumekusanyika" (Matendo ya Mitume 20:7,8).

Hapa tunayo kumbukumbu ya mkutano wa kidini uliofanyika siku ya kwanza ya juma. Kwa kupita tu, inatupasa kuzingatia kwamba huu ni mfano mmoja tu uliopata kuandikwa katika Agano Jipya unaoonyesha kufanyika kwa mkutano wa kidini katika siku ya kwanza ya juma. Hata hivyo, kifungu hiki hakina ushahidi wo wote kuhusu badiliko la Sabato, wala hakiungi mkono wazo la utakatifu wa siku ya Jumapili. Ulikuwa ni mkutano uliofanyika siku ya kwanza ya juma, lakini sio mkutano wa ibada ya kawaida ya siku ya Jumapili. Ulifanyika usiku. "Palikuwa na taa nyingi," na Paulo "akafuliza maneno yake hata usiku wa manane." Usiku pekee wa siku ile ya kwanza ni ule ambao sisi tunaujua kama Jumamosi usiku [Saturday night]. Siku za Biblia zinaanza na kuisha jua linapozama [machweo]. Siku ya kwanza ya Biblia huanza jua linapokuchwa [machweo] Jumamosi jioni, na inakwisha jua linapokuchwa Jumapili jioni. Kwa hiyo, "usiku wa manane" ambao Paulo "alifuliza maneno yake" ni lazima ungekuwa, ungaliweza tu kuwa, ni ule wa Jumamosi usiku.

Conybeare na Howson, katika kitabu chao kinachostahili kupendwa na watu wote cha 'LIFE AND EPISTLES OF THE APOSTLE PAUL,' wakishughulika na suala la wakati mkutano huo ulipofanyika, wanasema maneno haya:

"Ilikuwa ni jioni ile iliyokuja baada ya Sabato ya Wayahudi. Jumapili asubuhi merikebu ilikuwa tayari kwa safari." ----- Scribner's ed., Vol.II, uk.206.

Daktari [Dkt.] Horatio B. Hackett, profesa wa Agano Jipya la Kiyunani [Kigiriki] katika Chuo cha Thiolojia cha Rochester, katika kitabu chake cha 'COMMENTARY ON ACTS,' asema hivi:

"Wayahudi walihesabu siku zao toka jioni hata asubuhi, na kwa kanuni ile usiku ule wa siku ya kwanza ya juma ungekuwa sawa na usiku wetu wa Jumamosi. Endapo Luka alihesabu hivyo hapa, kama wengi wanaotoa ufafanuzi wao wanavyodhani, basi, mtume alingoja mpaka Sabato ya Wayahudi ilipokwisha, na kufanya mkutano wake wa kidini wa mwisho [wa kuagana] pamoja na ndugu zake kule Troa... Jumamosi usiku, naye hatimaye aliendelea na safari yake Jumapili asubuhi." ----- Toleo la l882, uk.22l,222.

Kisa hicho kilichotolewa katika kitabu cha Matendo ya Mitume kinachosimulia habari za mkutano huu uliofanyika usiku kiliandikwa na Luka karibu miaka thelathini hivi baada ya kusulibiwa kwake Kristo. Ni jambo la maana kwetu sisi kuona ya kwamba anapoitaja siku hiyo ya kwanza haitaji kwa cheo au jina lake takatifu. Hasemi lo lote juu ya hali ya utakatifu wake [siku hii ya kwanza] unaodhaniwa na watu wengi kuwa upo. Anaitaja tu kama mojawapo ya siku za juma, "ya kwanza" miongoni mwa zile saba.

Hakuna neno lo lote linalounga mkono katika fungu hili kuhusu utakatifu wa siku hii ya Jumapili.

KUTAJWA KWA MARA YA MWISHO KWA SIKU YA KWANZA

Kutajwa kwa mara ya mwisho kwa siku hii ya kwanza ya juma katika Biblia ni katika Maandiko ya Paulo, ni wakati mmoja tu ambapo mwandishi huyu wa Nyaraka hizi, au Nyaraka nyingine zo zote za Agano Jipya, anapoitaja siku hiyo na kuihusianisha na mambo ya kidini: "Kwa habari ya ile changizo [michango] kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni hivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake [nyumbani], kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja" (l Wakorintho l6:l,2).

Hoja inatolewa kutokana na kifungu hiki kwamba siku ya kwanza hapana budi ilikuwa ni siku ya ibada kwa wote katika makanisa ya Korintho na Galatia, na kama ilikuwa hivyo katika [makanisa] hayo, basi, inaelekea kabisa kwamba ilikuwa hivyo pia katika makanisa mengine ya mitume, na ya kwamba kwa ajili hiyo Sabato ilikuwa imebadilishwa kwenda katika siku ile. Walakini, jambo hilo ni kwenda mbali sana na fungu hilo kuliko linavyomaanisha kwa mbali.

HAPAKUWA NA MKUTANO WA IBADA YA SIKU YA JUMAPILI

Fungu hili linaweka mpango ulio KINYUME kabisa na sadaka ya pamoja inayotolewa kanisani. Kila muumini kule Korintho alitakiwa AWEKE AKIBA KWAKE kama Mungu alivyomfanikisha, sio kuchukua sadaka yake na kwenda nayo mahali pa mkutano wa ibada, sio kuendesha mkutano wo wote kabisa siku ile kwa ajili ya ibada ya wote. Kamusi ya Kiyunani ya Greenfield inatafsiri Kiyunani kilichotumika hapa hivi: "kwake mwenyewe, yaani, nyumbani kwake."

Bwana William Domville, katika kitabu chake kiitwacho 'THE SABBATH' [SABATO], anayo maneno haya ya ufafanuzi kwa madai ambayo mara nyingine yanatolewa kuhusu maana ya kifungu hiki:

"Ni ajabu kwamba fungu hili ambalo halisemi neno lo lote juu ya mkutano wo wote ule kwa kusudi lo lote lile, lingeweza kuletwa kama uthibitisho wa desturi hii ya kukusanyika pamoja kwa madhumuni ya kidini!...

"Kama hilo ni jambo la ajabu kuweza kuiona sababu ya kuweka desturi hii ya kukusanyika pamoja, japokuwa hakuna mkutano wo wote wa ibada uliotajwa katika [fungu] hilo, basi, inaonekana bado kuwa ni ajabu zaidi, bado hakuna ulinganifu wo wote wa kuona ndani yake... kwamba agizo lile la kuweka nyumbani sadaka hii ya kuwasaidia maskini liweze kuwa na maana ya kwamba sadaka hizo za kuwasaidia maskini zitolewe kanisani....

"Tafsiri inayopatikana katika Biblia zetu za kawaida inapatana kabisa na ile ya asilia: 'Kila mtu kwenu na aweke akiba kwake.' Tafsiri nyingine zaidi inayotafsiri neno kwa neno ya neno lililotumika katika lugha ya asili, THESAURIZON [kuweka akiba], ingelifanya [fungu hilo] kuwa wazi zaidi kwamba kila aliyetoa mchango huo ilimpasa yeye mwenyewe kudunduiza

[kuweka kidogo kidogo], wala sio kuupeleka [mchango huo] juma kwa juma kwa mtu mwingine awaye yote." -----Ukurasa l0l-l04.

Hakuna neno lo lote katika kifungu hiki linaloonyesha kwamba makanisa yale ya mwanzo yalikuwa yanaitunza siku ya Jumapili kama Sabato. Siku ya kwanza imetajwa, ni kweli, lakini kama tu mojawapo ya siku za juma, siku ambayo, baada ya kumaliza kuitunza Sabato na kuanza tena kazi zao za kila juma na kuanza juma jipya la kazi, walitakiwa kufanya mahesabu yao, ili kukadiria faida waliyopata juma lililopita, na kujifunza jinsi Mungu alivyowafanikisha, wakiweka kando sehemu ya mapato yao kwa ajili ya ndugu zao waliokuwa na njaa penginepo.

## SABATO ZA KIVULI [MAADHIMISHO] ZILIKOMA

Inadhaniwa na wengine kwamba Paulo alikuwa anataja badiliko la Sabato wakati alipowaandikia Wakolosai: "Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo" (Wakolosai 2:16,17).

Mfumo wa kafara [dhabihu] (ceremonial system) wa Agano la Kale ulikuwa na sikukuu nyingi, siku takatifu nyingi, na sabato za kila mwaka. Mfumo ule ulio"amriwa hata wakati wa matengenezo mapya" (Waebrania 9:10), ulikufa pamoja na Kristo [pale msalabani], ambaye huo ulikuwa ni kivuli chake. Kwa sababu hiyo, yule aliyemwamini Kristo hakulazimika kuirudia mifano (types) hiyo na vivuli (shadows) vyake. Hakuwa na haja ya kuzishika sabato zake saba zilizotokea kila mwaka (Mambo ya Walawi 23:4,24,32,39), [Sabato 7 za kivuli ni hizi: l. f.7; 2. f.8; 3. f.l6,21; 4. f.24,25; 5. f.3l-32; 6. f.34,35,39; 7. f.36] zote hizo zilitakiwa kushikwa kama nyongeza kwa au "kando ya Sabato za BWANA" (Mambo ya Walawi 23:38). Na kama vile kafara na kawaida hizo za dini zilizoadhimishwa zilivyokuwa hazina nguvu tena, ndivyo Mkristo muumini, katika kifungu hiki cha Wakolosai anavyotahadharishwa asije akamruhusu mtu ye yote kumhukumu katika mambo hayo. Kifungu hicho hakina uhusiano kabisa na Sabato ya Bwana ya siku ya saba.

Labda jambo hili litapokewa kwa upesi, na kuonekana wazi zaidi, kama mawazo yetu yataelekezwa kwenye ufafanuzi wa kifungu hiki uliotolewa na watu maarufu wenye mamlaka. Dkt. Adam Clarke, katika kitabu chake cha Ufafanuzi (Commentary) [Komentari] kilichoandikwa kwa jina lake, anasema hivi kuhusu Wakolosai 2:l6:

"Hakuna taarifa hapa isemayo kwamba SABATO iliondolewa, au kwamba matumizi yake ya kimaadili yalibatilishwa kwa kule kuanzishwa kwa Ukristo. Nimeonyesha mahali pengine kwamba, 'Ikumbuke siku ya sabato uitakase' ni amri ya UWAJIBIKAJI UNAODUMU MILELE, nayo haiwezi kutanguliwa isipokuwa mpaka wakati wa mwisho hapo utakapokomeshwa wakati wote. Kama ilivyo MFANO [TYPE] wa raha ile inayosalia kwa watu wa Mungu, yaani, raha ile ya milele, basi, haina budi kuendelea kwa nguvu zake zote mpaka umilele ule utakapofika; kwa maana hakuna MFANO [TYPE] unaokoma mpaka hapo KITU HALISI (ANTITYPE) kinapokuja. Zaidi ya hayo, sio dhahiri kwamba mtume huyu anaitaja SABATO mahali hapa, iwapo ni ile ya Kiyahudi ama ile ya Kikristo; SABBATON zake, ZA SABATO (ZA MAJUMA), inaelekea zaidi sana kuzihusu zile SIKUKUU ZA

MAJUMA walizokuwa nazo, ambazo mengi sana yamesemwa katika maelezo juu ya vitabu vitano vya Musa (Pentateuch). ----- Toleo la l85l.

Dkt. Barnes, mfafanuzi wa Kanisa la Presbyterian ambaye alijulikana sana, anaandika hivi katika maelezo yake ya 'NOTES ON COLOSSIANS (2:l6)':

"'[OR OF THE SABBATH DAYS] AU SABATO [yaani, SIKU ZA SABATO].' Neno hili 'sabato' katika Agano la Kale linatumika sio tu kwa siku ya saba, bali kwa siku zote za pumziko takatifu ambazo zilishikwa na Waebrania, na hasa zile zilizotokea mwanzo na mwisho wa sikukuu zao kuu. Pasipo shaka lo lote mahali hapa zinatajwa siku zile, kwa vile neno hili [sabato] limetumika katika wingi, na mtume huyu haitaji hasa ILE Sabato inayoitwa hivyo kihalali. Hakuna ushahidi wo wote kutokana na kifungu hiki kwamba angeweza kufundisha kwamba hapakuwa na wajibu wo wote wa kushika wakati WO WOTE ulio mtakatifu, kwa sababu hakuna sababu hata kidogo ya kuamini kwamba [Paulo] alimaanisha kufundisha kwamba amri hii moja katika zile kumi ilikuwa imekoma kuwafunga wanadamu.

"Kama angelitumia neno hilo katika umoja 'THE SABBATH' [SABATO], hapo, kwa kweli, ingekuwa wazi kwamba alikuwa na maana ya kufundisha kwamba amri ile ilikuwa imekoma kuwa mojawapo ya masharti, na ya kwamba Sabato hiyo isingeweza kushikwa tena. Lakini yale matumizi ya neno hilo katika wingi, na uhusiano wake, huonyesha ya kuwa jicho lake [Paulo] lilikuwa linaziangalia zile siku nyingi zilizoshikwa na Waebrania kama sikukuu zao, kama sehemu ya sheria yao ya Kafara na Kivuli (Ceremonial and typical law), na sio sheria ile iliyohusika na maadili (Moral law), ama [yaani] zile Amri Kumi. Hakuna sehemu yo yote ya sheria hii ya maadili ----- hakuna mojawapo ya amri hizo kumi ----- ambayo ingesemwa kuwa ni 'KIVULI cha mambo [mema] yajayo.' Amri hizi, kulingana na tabia ya sheria hii ya maadili, ni za milele na zinatoa wajibu kwa ulimwengu mzima." ----- Toleo la l850, uk.306,307..

Kwa hiyo, baada ya kulichunguza Agano Jipya kwa makini, tunafikia mwisho wa kukata maneno kwamba [fungu hilo] halina ushahidi wo wote kuhusu badiliko hilo la Sabato, hakuna kibali cha Mungu kinachounga mkono badiliko kama hilo, wala hakuna kuungwa mkono ko kote hata kama ni kwa kiwango kidogo kwa utunzaji huo wa siku ya Jumapili

## SURA YA 4.

## KWA JINSI GANI, KWA NINI, NA NI NANI ALIYEFANYA BADILIKO HILI

Badiliko toka Sabato ya kweli kwenda sabato ya uongo lililetwa na uasi mkuu uliotokea katika kanisa la mwanzo ambalo liligeuka na kuwa katika mfumo wa Kikatoliki wa Rumi [Roma]. Sababu zilizolisukuma kanisa hili kuitupilia mbali Sabato ya Bwana na kuichagua siku ya waabudu jua zilikuwa mbili: nazo ni hizi, tamaa ya kuepuka kufananishwa na Wayahudi, ambao ushupavu wao wa dini na anguko lao viliwafanya kuchukiwa na watu wote; na tamaa yenye nguvu sawa na hiyo ni ile ya kutaka kuwaongoa wapagani waliokuwa wanaabudu jua na kuwafanya washikamane na kanisa.

Hata katika siku zile za Mitume uasi huo ulianza kujitokeza. Paulo aliandika hivi: "Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi" (2 Wathesalonike 2:7).

Tena alitangaza hivi: "Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu, wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawandamie wao" (Matendo ya Mitume 20:29,30).

### MPINGA KRISTO NDIYE MWASISI WA UTUNZAJI WA JUMAPILI

Ukengeufu huo kutoka katika imani ungeenea na kukua kwa kiwango kikubwa, alisema Mtume huyo. "Ukengeufu" huo mkubwa, ama uasi, hatimaye ungemfunua "yule mtu wa kuasi [mtu wa dhambi]," "mwana wa uharibifu; yule mpingamizi [Mpinga Kristo], ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu [Kanisa], akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu" (2 Wathesalonike 2:3,4).

Kwa kutimiza unabii huu uliotabiriwa, imani ya Kikristo na utawala wa kanisa la Kikristo vikabadilika kabisa katikati ya siku zile za Mitume na kule kutangazwa kwa uongofu wake Konstantino (Constantine), Mfalme wa Rumi [Roma]. Kweli ikabadilishwa na kuwa uongo, na upotoshaji wa imani ile ya kweli uliongezeka kasi sana kwa kiwango cha kushangaza.

"Urembo wa ibada na kawaida za ibada ambazo wala Paulo, wala Petro hakupata kuzisikia, zikaingia kanisani kimya kimya na kuanza kutumika, na baadaye zikadai kuwa zina cheo sawa na zile zilizowekwa na Mungu. Maofisa [wa kanisa] ambao Mitume wale wa zamani wasingeweza kupata mahali pa kuwaweka, pamoja na vyeo vyao ambavyo kwao [Mitume] vingekuwa havina maana yo yote kabisa, vikaanza kuleta changamoto kwa watu, na kuitwa kuwa ni vyeo vya Mitume." ----- WILLIAM D. KILLEN, D.D., THE ANCIENT CHURCH, Utangulizi kwa Toleo la Kwanza, uk. xvi.

Miongoni mwa maadhimisho haya ya ajabu, mapya, na ya uongo yaliyoingizwa katika kanisa lile lililoanguka, ilikuwa ni sikukuu ya Jumapili.

Kuhusu uasi huu, na mwanzo wa uadhimishaji huu wa siku ya Jumapili miongoni mwa Wakristo ambao ulitokana na huo [uasi], pamoja na sababu zilizojificha nyuma ya kuichagua sikukuu hii ya kipagani, ushuhuda mwingi sana wa kihistoria unaweza kuletwa. Kile kilichotolewa hapa kimechukuliwa toka katika maandiko ya wale tu ambao wamekuwa au ni WATUNZAJI WA SIKU HII YA JUMAPILI, kwa maana UNGAMO LAO kuhusu chanzo cha utunzaji wake [Jumapili] litakuwa na uzito mkubwa zaidi kuliko shutuma ambazo zingeweza kutolewa na wale WANAOITUNZA SABATO.

Wilhelm August John Neander, mwanathiolojia mkuu na mwanahistoria wa Kijerumani toka Heidelberg, ambaye kitabu chake cha 'HISTORY OF THE CHRISTIAN RELIGION AND CHURCH' kina thamani kubwa na sifa kiasi cha kumpatia cheo cha "mkuu wa wanahistoria wa Kanisa," anatangaza kwa kusema kweli tupu:

"Upinzani kwa dini ile ya Kiyahudi ulisababisha kutangazwa kwa sikukuu maalum ya Jumapili mapema sana, naam, ikiwa badala ya Sabato.... Sikukuu ya Jumapili, kama zilivyo sikukuu nyingine zote, daima ilikuwa ni amri ya wanadamu tu, nayo ilikuwa mbali na makusudi ya wale Mitume kuweza kuanzisha amri ya Mungu kwa njia kama hii, na tangu mwanzo wa kanisa la Mitume wazo hili la kuhamisha sheria za Sabato kwenda Jumapili lilikuwa mbali nao. Labda, mwishoni mwa karne ya pili ndipo matumizi potofu kama hayo yalianza kufanyika; maana kufikia wakati ule watu wanaonekana kwamba walianza kufikiria kuwa kufanya kazi siku ya Jumapili ilikuwa ni dhambi." ----- Rose's translation from the first German edition, uk.l86.

## UTUNZAJI WA SABATO HAUKUKATIZWA

Utunzaji wa siku ya saba haukukatizwa na Wakristo wale wa kwanza kwa kipindi kirefu baada ya kupaa kwake Kristo. Mamia ya miaka yalikuwa yamepita kabla ya nguvu na uwezo wa Upapa (Papacy) kuiondoa kanisani. Kusema kweli, kamwe haijakatizwa kabisa kabisa, kwa vile siku zote kumekuwako na mbegu ya wenye haki walioendelea kuwa waaminifu na watiifu kwa Sabato takatifu ya Mungu.

Bwana Morer, mchungaji msomi wa Kanisa la Kiingereza (Church of England), asema kwamba "Wakristo wale wa zamani walikuwa na kicho kikubwa sana kwa Sabato, nao waliitumia siku hiyo kwa ibada na mahubiri. Na hapana mashaka yo yote kwamba waliipata desturi hiyo toka kwa Mitume wenyewe." ----- DIALOGUES ON THE LORD'S DAY, uk.l89.

Profesa Edward Brerewood wa Chuo cha Gresham, London, kutoka katika Kanisa lilo hilo asema hivi:

"Sabato ile ya zamani iliendelea kuwako na kutunzwa... na Wakristo wale wa Kanisa la Mashariki (East Church), kwa zaidi ya miaka mia tatu baada ya kifo cha Mwokozi wetu." ----- A LEARNED TREATISE OF THE SABBATH, uk.77.

Mwanathiolojia mwangalifu na msema kweli na mwanahistoria, Lyman Coleman, asema hivi: "Kuendelea mpaka kufikia karne ile ya tano utunzaji wa Sabato ya Kiyahudi uliendelezwa na kanisa la Kikristo, lakini nguvu yake na utaratibu wake wa ibada vikaendelea kupungua pole pole mpaka hapo ilipokoma kabisa kutunzwa." ----- ANCIENT CHRISTIANITY EXEMPLIFIED, Sura ya 26, Sehemu ya 2, uk.527.

Socrates, mwanahistoria ya kanisa Myunani aliyeishi katika karne ile ya tano, ambaye kazi yake ilikuwa ni maendelezo ya ile ya Eusebio [Eusebius] asema hivi:

"Karibu makanisa yote ulimwenguni wanaadhimisha meza takatifu ya Bwana siku ya Sabato ya kila juma, lakini Wakristo wale walioko Alexandria na Rumi, kutokana na mapokeo fulani ya zamani, wameacha kufanya hivyo." ----- ECCLESIASTICAL HISTORY v.22.2l,22, in A SELECT LIBRARY OF NICENE AND POST-NICENE FATHERS, 2d Series, Vol.II, uk.l32.

Sozomen, mwanahistoria wa kanisa mwingine wa karne ile ya tano, anathibitisha kwa maneno haya:

"Watu walioko Constantinople, na karibu wa kila mahali, wanakusanyika pamoja siku ya Sabato, na vile vile katika siku ya kwanza ya juma, desturi ambayo kamwe haifuatwi kule Rumi na kule Alexandria." ----- ECCLESIASTICAL HISTORY, vii.l9, in A SELECT LIBRARY OF NICENE AND POST-NICENE FATHERS, 2d Series, Vol. II, uk.390.

## SIKU YA KIPAGANI YAINGIZWA KATIKA UKRISTO

Katika suala hili la kwamba Jumapili ilikuwa haijulikani kama siku ya mapumziko katika karne zile za kwanza, maneno haya yanaonekana katika Kamusi ya Kumbukumbu za Mambo ya Kale ya Kikristo iliyoandikwa na Smith na Cheerham (Smith and Cheerham's Dictionary of Christian Antiquities):

"Wazo lile la kubadilishwa kwa Sabato ile ya Kiyahudi kwenda Siku ya Bwana [Jumapili] kwa kibali rasmi cha Mitume na kuihamisha kwenda kwa [siku] hiyo, labda katika hali yake ya kiroho, pamoja na wajibu wake wa Sabato ulioanzishwa kwa kutangazwa amri ile ya nne, halina msingi wo wote, aidha katika Maandiko Matakatifu au katika kumbukumbu za kale za Kikristo... Wazo ambalo hatimaye liliwekwa katika kichwa cha 'Sabato ya Kikristo' na kuadhimishwa kwa kufuata maagizo makali ya Kiyahudi, kwa kadiri tuwezavyo kuona, lilikuwa halijulikani kabisa katika karne zile za mwanzo wa Ukristo." ----- Article "SABBATH," uk.l823.

Hutton Webster, Ph.D., katika kitabu chake cha 'REST DAYS' anayo haya ya kusema:

"Wakristo wale wa kwanza mwanzoni kabisa walikuwa wamelipokea juma la Kiyahudi la siku saba pamoja na hesabu zake za siku za juma, lakini karibu na mwisho wa karne ya tatu B.K. [Baada ya Kristo], juma hilo likaanza kuachwa na badala yake likafuatwa juma la Sayari; na katika karne ile ya nne na ya tano majina ya kipagani yakawa yamekubalika kwa jumla katika nusu ya Magharibi ya Ukristo. Matumizi ya majina ya sayari na Wakristo wale hudhihirisha mvuto wa dhana za kinajimu (astronomical speculations) zilizoletwa [kanisani] na waongofu waliotoka kwenye upagani.... Katika karne zizo hizo ibada za kuabudu jua, hasa ile ya Mithra [Ibada ya jua ya Waajemi], ambazo zilitoka Mashariki, zikaenea katika ulimwengu ule wa Kirumi, na kuwafanya wapagani kuweka ibada yao ya 'DIES SOLIS' [Siku ya Jua] badala ya ile ya 'DIES SATURN' [Jumamosi], na kuifanya iwe siku ya kwanza ya juma lile la sayari.... Hivyo ndivyo siku hii ya kipagani ilivyopandikizwa taratibu katika Ukristo." ----- Ukurasa 220,221.

## UPOTOFU WA UKRISTO

Utunzaji wa siku ya Jumapili ulianza kipindi cha mapema katika historia ya kanisa. Walakini, kule kuingizwa kwake [Jumapili] mapema sio sababu ya kuifanya iwe halali kuadhimishwa kama wajibu ulioagizwa na Maandiko. Amri ile tu itokayo katika Maandiko ndiyo inayotosheleza kwa jambo kama hilo. Wala hakuna amri kama hiyo inayotokana na Maandiko kwa kuiadhimisha Jumapili.

Hakuna idhini yo yote ya Maandiko kwa kuingiza mageuzi yale potofu katika kanisa lile la kwanza, ambalo hatimaye liligeuka na kuwa Upapa. Juu ya suala hilo, Dowling, katika kitabu chake cha 'HISTORY OF ROMANISM,' anasema maneno haya:

"Hakuna cho chote kinachoushtua moyo wa mwanafunzi mwangalifu wa historia ya kale ya kanisa kwa mshangao mkubwa sana kama kipindi kile cha mapema sana ambacho kilishuhudia uingizaji [kanisani] wa upotofu mwingi sana wa Ukristo, ambao umo katika mfumo wa Kiroma, ukiotesha mizizi yake na kukua; hata hivyo isidhaniwe kwamba waasisi wale wa kwanza wa

mawazo hayo mengi pamoja na kawaida zake ambazo ni kinyume na Maandiko ya kuwa walikusudia kuvipandikiza viini hivyo vya upotofu, wakitazamia au hata kuwazia kwamba vingekua kiasi hicho na kuzalisha mfumo mkubwa na wa kuchukiza kama huo uliojaa ushirikina na makosa mengi kama ule wa Upapa." ----- Thirteenth ed., i.1, Sec. 1, uk.65.

## SIKU YA JUA ILIAZIMWA KUTOKA KWA MAKAFIRI

Makusudi yaliyowasukuma kufanya badiliko hilo kutoka Sabato ya kweli kwenda siku ile ya jua yanaelezwa zaidi na kasisi wa mtaa wa Kanisa la Kiingereza, Reverend T. H. Morer, katika kitabu chake cha 'SIX DIALOGUES ON THE LORD'S DAY':

"Haiwezi kukanushwa kwamba tunaazima jina la siku hii [Jumapili] kutoka kwa Wayunani wale wa zamani na Warumi, nasi tunakubali kwamba Wamisri wa zamani waliabudu jua, na kama KUMBUKUMBU ya kudumu ya ibada yao iliyotolewa kwa siku hii kwake [mungu jua]. Nasi tunauona mvuto wa mifano yao ukiwafikia mataifa MENGINE, na miongoni mwao wakiwamo Wayahudi wenyewe, wakimwabudu yeye [mungu jua]; walakini desturi hizo potofu [za ibada] hazikuweza kuwazuia Mababa wale wa Kanisa la Kikristo na kuwafanya waibatilishe au kuiweka kando kabisa siku ile au jina lake, bali tu kuitakasa na kuviendeleza vyote viwili [siku ile na jina lake], kama walivyofanya pia kwa mahekalu ambayo yalikuwa yamenajisiwa kabla kwa ibada ya sanamu, na mifano mingine ambayo watu wale wema walikuwa na udhaifu katika kufanya badiliko jingine lo lote isipokuwa lile lililoonekana wazi kuwa ni la lazima kubadilishwa, na katika mambo hayo [potofu] yaliyokuwa wazi hakuna ulinganifu wo wote na dini hii ya Kikristo; kwa vile Jumapili ilikuwa ni siku ambayo Mataifa [Wapagani] walikuwa wanaiabudu sayari ile [jua], na kuiita Siku ya Jua [Jumapili], kwa sehemu kutokana na mvuto halisi wa siku ile, na kwa sehemu kutokana na umbile lake [jua] la kiungu (kama vile wao walivyolifikiria), basi, Wakristo wakaona ya kwamba inafaa kuitunza siku ile ile na kulitumia jina lake lile lile, ili wasije wakaonekana kuwa wana chuki nao [wapagani], na kwa njia ile ambayo vinginevyo ingeweza kuwa kubwa zaidi [kwa wapagani] kuonyeshwa dhidi ya injili." ----- Ukurasa 22,23.

## MUUNGANO WA UKRISTO POTOFU NA UPAGANI

Hivyo ndivyo inavyoonekana ya kwamba muungano huu kati ya Ukristo potofu na upagani uliozalisha Ukatoliki wa Rumi ulikuwa ndio udongo ulimokua ule utunzaji wa sabato ya bandia, yaani, Jumapili. Mfumo huu wa Ukatoliki na Jumapili ni kitu kimoja. Vyote viwili chimbuko lake ni katika upagani, na vyote viwili vilipandikizwa katika kanisa la Kikristo kwa kipindi kile kile kimoja. Vyote viwili viliufagilia mbali upinzani wote, na kuwa sehemu za mamlaka zile zilizouongoza ulimwengu ule wa Kikristo. Baada ya kujizatiti, vyote viwili vikatafuta njia ya kuelezea chimbuko lao kuwa linatoka siku zile za Mitume. Papa akadai kwamba yeye anachukua mahali pa Petro, na Jumapili nayo ikadai kwamba siku ile ya ufufuo ndilo chimbuko lake. Madai yote mawili hayakuwa na ukweli wo wote ndani yake, wala hakuna dai lo lote katika hayo mawili lililopata kuthibitishwa [kwa Maandiko]. Hata hivyo, udanganyifu

huu wa aina mbili ulikua sana sana na kupata nguvu kubwa sana, Papa akiwa ndiye Bwana wa Maaskofu na Jumapili nayo ikiwa Bwana wa siku zote; lakini kule kufanikiwa kwao [Papa na Jumapili] kulimfukuza yule Bwana wa uzima nje ya kanisa, na kumwacha humo yule Mpinga Kristo peke yake.

Mmojawapo wa watetezi (apologist) wa siku hii ya kipagani katika miaka ile ya mwanzo, Tertullian, aliyetambulikana kama mwandishi wa kanisa na Kanisa la Katoliki, aliyaandikia kitabu mataifa yale yaliyokuwa bado yanaendelea kuabudu sanamu, na katika kitabu hicho alijaribu kuiondoa hali ya kuchanganyikiwa iliyoletwa na kule kuichagua siku ile ya Jumapili kulikofanywa na Wakristo, ambayo [Jumapili] ilizusha wazo la kwamba [Wakristo] walikuwa wanageukia kabisa kwenye ibada ya jua. Yeye asema hivi:

"Kwa kujali sana uungwana wetu yatupasa kukiri kwamba wengine wanadhani jua ni mungu wa Wakristo, kwa sababu ni jambo linalojulikana kabisa kuwa tunasali tukielekea mashariki, au kwa sababu tunaifanya Jumapili kuwa sikukuu yetu. Ni nini basi? Je, ninyi mnafanya chini ya hayo? Je, wengi miongoni mwenu, wakati mwingine kwa kujifanya kuwa mnaviabudu viumbe vile vya mbinguni (heavenly bodies), hamchezeshi vile vile midomo yenu kuelekea kule jua linakotokea? Ndio ninyi ambao, kwa vyo vyote, mmeliingiza hata jua katika kalenda yenu ya juma; nanyi mmependelea kuichagua siku yake hii [Jumapili] kuliko siku ile iliyotangulia, kuwa ndiyo siku inayofaa katika juma aidha kwa kuacha kabisa kuogelea, au kuahirisha mpaka jioni itakapofika, kwa ajili ya kupumzika na kula karamu zenu. Kwa kufuata desturi hizi, kwa makusudi mnajitenga na kawaida zenu za ibada na kuzitumia zile za wageni." ----- AD NATIONES, i.l3, in THE ANTE-NICENE FATHERS, Vol. III, uk.l23

Utetezi wa pekee ambao mwandishi huyo Mkristo wa zamani aliweza kutoa kwa kuichukua Jumapili kutoka kwa Wapagani ulikuwa ni ule wa kuwauliza swali hili: "Je, ninyi mnafanya chini ya hayo?" Anaonyesha kwamba ni Wapagani walio"liingiza jua katika kalenda ya juma," na hao ndio walioipendelea Jumapili kuliko ile "siku iliyotangulia," ambayo ilikuwa ni Sabato. Anatoa hoja yake kwa kusema kwamba kwa jinsi gani, basi, wangeweza kuwakaripia Wakristo kwa kuiga mfano wao wenyewe? Hakika huu ni ushahidi wa kutosha kuhusu chimbuko ambako utunzaji wa Jumapili ulianzia.

## AMRI YA JUMAPILI YA ZAMANI SANA IJULIKANAYO KATIKA HISTORIA.

Amri ya Jumapili ya zamani sana ijulikanayo katika historia ni ile ya Konstantino iliyotangazwa mwaka 321 B.K. Inasomeka hivi:

"Katika siku tukufu ya jua hebu mahakimu na watu wale wanaokaa mijini wapumzike, na viwanda vyote vifungwe. Walakini huko vijijini [mashambani] watu wale wanaoshughulika na kilimo wanaweza kuendelea na kazi zao kwa uhuru na kwa kulindwa na sheria hii; kwa sababu mara nyingi hutokea kwamba siku nyingine yo yote haifai sana kwa kupanda mbegu za nafaka au kwa kupanda mizabibu; isije ikawa kwa kupuuzia wakati ule unaofaa kwa shughuli kama hizo mibaraka ile ya mbinguni ikapotezwa. (Imetolewa siku ya 7 ya Machi, Krispo (Crispus) na Konstantino (Constantine) wakiwa wote wawili wawakilishi wa Wananchi (Consuls) kwa mara ya pili.) ----- CODEX JUSTINIANUS, lib.3, tit.l2,3; translated in PHILIP SCHAFF, D.D., HISTORY OF THE CHRISTIAN CHURCH (Seven-volume edition, l902), Vol.III, uk.380.

Konstantino alikuwa Mfalme wa Rumi kuanzia mwaka 306 mpaka 337 B.K. Yeye alikuwa mwabudu jua katika kipindi cha mwanzo cha utawala wake. Baadaye alijitangaza mwenyewe kuwa ameongoka na kuwa Mkristo, lakini ndani ya moyo wake aliendelea kuwa mshabiki wa kuabudu jua.

Kuhusu dini yake, Edward Gibbon, katika kitabu chake cha 'THE DECLINE AND FALL OF THE ROMAN EMPIRE, asema hivi:

"Ushabiki wa dini wa Konstantino ulielekezwa kwa bidii zaidi kwenye jua, Apolo (Apollo) wa miungu ya Wayunani na Warumi; naye [Konstantino] alipendezwa kuwakilishwa kwa ishara za mungu huyo wa nuru na mashairi. Mishale isiyokosea ya mungu huyo, mng'ao wa macho yake, taji yake ya heshima, uzuri wake usiokoma, na mafanikio yake mazuri, vilionekana kumsonda kidole [huyo Apolo] kama ndiye mlezi (patron) wa Shujaa huyo kijana. Madhabahu za Apolo zilistawishwa kwa sadaka zilizotolewa na Konstantino kama nadhiri yake; na umati wa watu wale wajinga walifundishwa kusadiki kwamba Mfalme yule aliruhusiwa kuangalia kwa macho yake ya kibinadamu utukufu wa mungu wao mlinzi; na kwamba, aidha anapoamka au anapokuwa katika maono alikuwa anabarikiwa na heri za ndege njema [bahati] ya utawala wake mrefu na wenye ushindi. Jua lilisherehekewa ulimwenguni kote kama ndiye kiongozi asiyeshindikana na mlinzi wa Konstantino." ----- Sura ya 20, aya ya 3.

## JUMAPILI NA IBADA YA JUA

Amri iliyowekwa na Konstantino ya kuanzisha uadhimishaji wa Jumapili inatajwa na vitabu viwili vya insaiklapidia (encyclopedias):

"Utambuzi wa kwanza kuliko wote wa uadhimishaji wa Jumapili kama wajibu wa kisheria ni amri ile ya Konstantino ya mwaka 321 B.K., iliyoamuru kwamba mabaraza [mahakama] yote ya sheria, wakazi wote wa mijini, na viwandani wanalazimika kupumzika siku ya Jumapili (VENERABILI DIE SOLIS [SIKU TUKUFU YA JUA]), isipokuwa upendeleo maalum ulitolewa kwa wale waliokuwa wanashughulika na kazi ya kilimo." ----- ENCYCLOPAEDIA BRITANNICA (llth ed.), art. "SUNDAY."

Kwamba amri hii ya Jumapili haikuwa na uhusiano wo wote na Ukristo ni dhahiri kama mambo yaliyomo katika kifungu cha maneno kifuatacho kilichonukuliwa yatazingatiwa:

"Amri hii iliyotolewa na Konstantino pengine haikuwa na uhusiano wo wote na Ukristo; kinyume chake, inaonekana kwamba Mfalme huyo katika uwezo wake kama Kuhani Mkuu (Pontifex Maximus), alikuwa anaongeza tu siku nyingine ya jua, ambayo ibada yake ilikuwa imeimarishwa sana katika Dola yote ya Warumi, juu ya siku zile nyingine za kishenzi [kipagani] za kalenda yao takatifu." ----- HUTTON WEBSTER, Ph.D., REST DAYS, uk.l22, l23.

## KUIMARISHA UTUNZAJI WA JUMAPILI KWA AMRI

Kufuatia amri hiyo ya awali, wafalme wote na mapapa wote katika karne zile zilizofuata waliongeza amri nyingine za kuimarisha utunzaji wa Jumapili.

"Walakini, kile kilichoanza kama amri ya kipagani, kikaisha kama amri ya Kikristo; msururu mrefu wa amri za kifalme katika karne ile ya nne, ya tano, na ya sita, zikaamuru kwa ukali kujizuia kufanya kazi siku ya Jumapili." ----- Kitabu kile kile (ibid.) uk.270.

Hatua hizi za ziada ambazo kanisa na serikali walizichukua kuhakikisha ya kwamba Jumapili inakuwa badala ya Sabato kwa lazima, zimeelezwa katika aya chache tu na mwanasheria maarufu wa Baltimore, Maryland, aitwaye James T. Ringgold:

"Katika mwaka 386, chini ya Gratian, Valentinian, na Theodosio (Theodosius), iliamriwa kwamba mashauri [daawa] yote mbele ya sheria pamoja na shughuli zote hazina budi kukoma [siku ya Jumapili]....

"Miongoni mwa mafundisho ya dini yaliyoandikwa katika waraka wa Papa Innocent I, ulioandikwa katika mwaka wake wa mwisho wa upapa (4l6), ni kwamba siku ya Jumamosi [Sabato] iadhimishwe kama siku ya kufunga [kuacha kula chakula] tu....

"Katika mwaka 425, chini ya Theodosio Kijana, kujizuia kufanya michezo ya kuigiza (theatricals) pamoja na kutofanya tamasha (circus) [Jumapili] kuliamriwa....

"Mwaka 538, katika Baraza la Orleans,... iliagizwa kwamba kila kitu kilichoruhusiwa siku za nyuma kufanyika siku ya Jumapili kiendelee kuwa halali; bali kwamba kazi ya kulima kwa plau, au katika mashamba ya mizabibu, kukata majani, kuvuna, kupura nafaka, kulima, na kuweka boma la miti viepukwe kabisa, ili watu waweze kuhudhuria kanisani kwa raha zaidi....

"Karibu na mwaka 590 Papa Gregory, katika waraka wake kwa Warumi, aliwashutumu kuwa ni manabii wa Mpinga Kristo wale waliosisitiza kuwa kazi isingepaswa kufanywa siku ile ya saba." ----- THE LAW OF SUNDAY, Uk..265-267.

Aya ya mwisho ya kufungia maneno yaliyonukuliwa juu huonyesha kwamba bado walikuwamo ndani ya kanisa hadi kufikia mwaka 590 B.K. wale ambao walikuwa wanaitunza na kuwafundisha wengine kuitunza Sabato ya Biblia. Kusema kweli, utunzaji kama huo kwa wale wachache umefuatwa katika karne zote za Kikristo. Miongoni mwa wale walioitwa Waldensia (Waldenses) walikuwamo watunzaji wa siku ya saba.

Neander anauliza swali hili:

"Je, tusiweze kudhani kwamba tangu zamani za kale kikundi cha Wakristo wanaofuata desturi za Kiyahudi kilisalia, ambacho kutokana nacho madhehebu hii [ya Wapasaginia (Pasaginians), waliowekwa katika kundi moja na Waldensia na baadhi ya waandishi wanaoaminika] inapaswa kufikiriwa kama tawi lao?" ----- CHURCH HISTORY, FIFTH PERIOD, Section 4, l5th American ed., Vol. IV, uk. 59l.

Amri za kidini na serikali zilizotajwa sasa hivi katika kuianzisha amri ya Jumapili zinaliweka suala hili kwa wazi sana hata Eusebio, Askofu maarufu wa Kanisa Katoliki, baba

mmoja mwenye kusifika wa historia ya kanisa, na mwenye mazoea ya kujipendekeza mno kwa Konstantino na mwandishi wa habari za maisha yake, alikuwa na haki kusema hivi:

"Mambo yo yote ambayo yalikuwa ni wajibu kufanyika siku ya Sabato, hayo sisi tumeyahamishia katika Siku ya Bwana [Jumapili]." ----- COMMENTARY ON THE PSALMS, COMMENT ON PSALMS 9l (92 IN AUTHORIZED VERSION), quoted in ROBERT COX, LITERATURE OF THE SABBATH QUESTION, Vol.I, uk. 36l.

## KUIWEKA SIKU YA KIPAGANI MAHALI PA SIKU YA MUNGU

Huku kuiweka Jumapili badala ya Sabato sio jambo ambalo Kanisa Katoliki linakana au linajaribu kuficha. Kinyume chake, linakiri wazi, na kwa kweli linaonyesha kitendo hicho kwa majivuno kuwa ni ushahidi wa uwezo wake wa kubadili hata amri ya Mungu. Soma maneno haya yaliyonukuliwa kutoka katika Katekesimo za Kikatoliki:

THE CONVERT'S CATECHISM OF CATHOLIC DOTRINE, kazi ya Reverend Peter Geiermann, C.S.R., Januari 25, l9l0 ilipokea "mbaraka wa kitume" wa Papa Pius wa X. Juu ya somo hili la badiliko la Sabato, Katekesimo hii inasema hivi:

"SWALI. ----- Siku ya Sabato ni siku gani?

"JIBU. - ---- Jumamosi ndiyo siku ya Sabato.

"SWALI. ----- Kwa nini tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi?

"JIBU. ----- Tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu Kanisa Katoliki, katika Baraza la Laodikia (336 B.K.), lilihamisha taratibu ya ibada kutoka Jumamosi kwenda Jumapili." ----- Toleo la pili, uk. 50.

A DOCTRINAL CATECHISM, iliyoandikwa na Reverend Stephen Keenan, iliidhinishwa na Most Reverend John Hughes, D.D., Askofu Mkuu wa New York. Inayo maneno haya kuhusu suala hili la badiliko la Sabato:

"SWALI. ----- Unayo njia nyingine yo yote ya kuthibitisha kwamba kanisa linao uwezo wa kuanzisha sikukuu ambazo zinashikwa kama amri?

"JIBU. ----- Kama lisingekuwa na nguvu kama hizo, lisingaliweza kufanya kile ambacho wanadini wote wa siku hizi wanakubaliana nacho ----- lisingaliweza kuweka utunzaji wa Jumapili siku ya kwanza ya juma mahali pa utunzaji wa Jumamosi siku ya saba, badiliko ambalo halina Maandiko yo yote yanayolipa kibali hicho." ----- Ukurasa l74.

AN ABRIDGMENT OF THE CHRISTIAN DOCTRINE, iliyoandikwa na Reverend Henry Tuberville, D.D., wa Chuo cha Douay, Ufaransa, ina maswali na majibu haya:

"SWALI. ----- Unathibitishaje wewe kwamba kanisa linao uwezo wa kuamuru sikukuu na siku takatifu?

"JIBU. ----- Kwa kitendo kile kile cha kuibadili Sabato kuwa Jumapili, kitendo ambacho Waprotestanti wanakikubali; na kwa hiyo wanajikanusha wenyewe kijinga, kwa kuitunza Jumapili kwa ukali, na kuzivunja karibu sikukuu nyingine nyingi sana zilizoamriwa na Kanisa lilo hilo.

"SWALI. ----- Unalithibitishaje hilo?

"JIBU. ----- Kwa sababu kwa kuitunza Jumapili, wanaukiri uwezo wa Kanisa wa kuamuru sikukuu, na kuziamuru chini ya sharti la dhambi; na kwa kule kutozitunza zile zilizobaki [katika sikukuu] ambazo zimeamriwa nalo, kwa kweli, wanaukana tena uwezo ule ule." ----- Ukurasa 58.

## HAKUNA FUNGU HATA MOJA LA BIBLIA KWA KUITUNZA JUMAPILI

Kadinali Gibbons, katika kitabu chake cha 'THE FAITH OF OUR FATHERS,' asema hivi:

"Unaweza kusoma Biblia toka Mwanzo hadi Ufunuo, nawe hutalipata fungu [mstari] hata moja linaloidhinisha utakatifu wa Jumapili. Maandiko yanaamuru utunzaji wa kidini wa siku ya Jumamosi, siku ambayo sisi hatuitakasi kamwe." ----- Toleo la l893, uk.11

## "KANISA KATOLIKI... LILIBADILI SIKU"

Gazeti la 'CATHOLIC PRESS' la Sydney, Australia linasisitiza kwamba utunzaji wa Jumapili asili yake ni ya Kikatoliki peke yake.

"Jumapili imewekwa na Wakatoliki, na madai yake ya kuitunza yanaweza kutetewa tu kwa kanuni za Kikatoliki.... Toka mwanzo mpaka mwisho wa Maandiko [Biblia] hakuna hata kifungu kimoja cha maneno ambacho kinaunga mkono uhamishaji huo wa ibada ya [watu] wote ya kila juma toka siku ya mwisho wa juma kwenda siku ya kwanza." ----- Agosti 25, l900.

Katika kitabu chake cha 'PLAIN TALK ABOUT PROTESTANTISM OF TODAY,' Monsignor Segur asema hivi:

"Lilikuwa ni Kanisa Katoliki ambalo, kwa idhini ya Yesu Kristo, lilihamisha pumziko hili kwenda Jumapili kwa ukumbusho wa ufufuo wa Bwana wetu. Hivyo utunzaji wa Jumapili kwa Waprotestanti ni kuisujudia (pay homage) mamlaka ya Kanisa [Katoliki], kinyume chao wenyewe." ----- Toleo la l868, Sehemu ya 3, Kifungu cha l4, uk.225.

Katika mwaka l893 gazeti la 'CATHOLIC MIRROR' la Baltimore, Maryland lilikuwa chombo rasmi cha Kadinali Gibbons. Katika toleo lake la Septemba 23 la mwaka ule lilichapisha usemi huu wa kushangaza sana:

"Kanisa Katoliki kwa zaidi ya miaka elfu moja kabla ya kuwako Mprotestanti hata mmoja, kwa utume wake mtakatifu, lilibadili siku toka Jumamosi kwenda Jumapili." "Kwa hiyo, Sabato ya Kikristo [Jumapili] mpaka leo hii inakubalika kama mtoto wa Kanisa Katoliki likiwa mke wa Roho Mtakatifu, wala hakuna neno hata moja la kugombeza kutoka kwenye ulimwengu huo wa Kiprotestanti." ----- Reprinted by the CATHOLIC MIRROR as a pamphlet, THE CHRISTIAN SABBATH, uk. 29,3l.

## UTUNZAJI WA JUMAPILI HAUNA KIBALI CHO CHOTE CHA MUNGU.

Burns na Oates wa mjini London, ni wachapishaji wa vitabu vya Kanisa Katoliki la Roma [Rumi], kimojawapo wanapendezwa kukiita 'THE LIBRARY OF CHRISTIAN DOCTRINE.' Sehemu yake moja inaitwa "Kwa nini Huitunzi Siku ya Sabato?" na kinajenga hoja ifuatayo kati ya Mkatoliki na Mprotestanti:

"Utaniambia ya kwamba Jumamosi ilikuwa Sabato ya Kiyahudi, na ya kwamba Sabato ya Kikristo imebadilishwa kwenda Jumapili. Imebadilishwa! lakini na nani? Ni nani aliye na mamlaka ya kubadili amri dhahiri ya Mungu Mwenyezi? Mungu anaponena na kusema, 'Utaitakasa siku ya saba,' nani atakayethubutu kusema, La, unaweza kufanya kazi yako na kufanya shughuli zote za kidunia katika siku ile ya saba; bali utaitakasa siku ya kwanza badala yake? Hili ndilo suala la maana kuliko yote ambalo mimi sijui jinsi unavyoweza kulijibu.

"Wewe ni Mprotestanti, nawe unajidai kwamba unakwenda kwa Biblia na Biblia peke yake; na bado wewe, katika jambo hili la maana sana kama vile kuadhimisha siku moja katika zile saba kama siku takatifu, unakwenda kinyume cha andiko lililo wazi la Biblia, na kuweka siku nyingine badala ya siku ile ambayo Biblia imeamuru. Amri ile ya kuitakasa siku ya saba ni mojawapo ya zile kumi; je! unaamini ya kwamba zile nyingine tisa bado zinamfunga mwanadamu; na ni nani aliyekupa mamlaka ya kuigeuza amri ile ya nne? Kama wewe ni mnyofu kulingana na kanuni zako mwenyewe, kama kweli unaifuata Biblia na Biblia peke yake, basi, ingekupasa kutoa fungu fulani la Agano Jipya ambalo linaonyesha wazi kwamba amri hii ya nne imebadilishwa." ----- Ukurasa 3,4.

Baada ya kuichunguza Biblia kwa makini, pamoja na historia ya serikali na kanisa, na maandiko ya kithiolojia, komentari (commentaries), kanuni za kanisa (Church Manuals), Katekesimo, na maungamo ya kweli ya wale wanaoitunza Jumapili, tunalazimika kuhitimisha suala hili kwa kusema kwamba hakuna kibali cho chote katika Maandiko Matakatifu cha kuitunza Jumapili, hakuna kibali cho chote kilichotolewa kwa mwanadamu ye yote kufanya badiliko hilo ambalo mwanadamu amelifanya sasa; kwamba badiliko hili la kuiweka sabato ya uongo [Jumapili] mahali pa Sabato ya kweli ya Bwana [Jumamosi] ilikuwa ni kazi ya kundi lile la Mpinga Kristo ambalo lilichagua utunzaji wa siku ile ya kipagani kabisa na kwa ushupavu wao kuiweka ndani ya kanisa la Kikristo; na ya kwamba utunzaji kama huo hauwezi kumfunga Mkristo muumini ye yote, bali ingepaswa kutupiliwa mbali katika kawaida zetu za

ibada, na Sabato ya kweli ya Mungu kurudishwa mahali pake pa halali, ndani ya mioyo ya watu Wake na katika kawaida za ibada ya kanisa Lake.

## SURA YA 5

## SIKU YA SABA NI ILE ILE

Siku hizi, hata watu watofautiane kiasi gani juu ya kuitambua Sabato, hapawezi kuwa na tofauti yo yote ya maoni kuhusu kweli hii. Siku ya saba ya juma lile la Uumbaji ilitengwa na siku zile nyingine, nayo ikatangazwa kuwa imebarikiwa, ni siku takatifu ya Muumbaji ya kupumzika [kustarehe]. Kumbukumbu ni hii: "Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya" (Mwanzo 2:l-3).

Kama siku ya saba imepotea tangu wakati ule, basi, haikupotea baadaye. Ilikuwa ni siku ile ya mwisho wa juma, yaani, ya saba.

Madai yanatolewa sasa kwamba siku ile ile ya saba ya uumbaji haiwezi kupatikana. Tunajulishwa kwamba kujaribu kuitambua sasa ingekuwa ni kazi bure, isiyowezekana kabisa. Sababu yake inayotolewa kuhusu suala hilo ni kwamba inasemekana kuna utata ulioletwa na mabadiliko mengi ya kalenda mbalimbali katikati ya kipindi kile na hiki cha sasa, kutokuwako kabisa kwa kalenda ya aina yo yote katika vipindi vile vya zamani sana na kushindwa kutunza mahesabu ya kuonyesha mara ngapi dunia hii imezunguka katika mhimili wake katika karne zote.

Tunaambiwa kwamba hizi ndizo sababu zinazofanya kazi ya kuipata siku ya saba katika kipindi hiki cha mwisho cha historia ya ulimwengu huu kuwa ni kazi kubwa mno kabisa inayotushinda.

Lakini, endapo watu wanataka kweli kuipata siku ile ya saba, inawezekana. Si kazi kubwa kama inavyodhaniwa kuwa. Endapo kuna tamaa ya kweli ya kutaka kuijua kweli, basi, siku zote kuna njia ya kuivumbua.

## MUNGU ANATUNZA KUMBUKUMBU SAHIHI

Mungu hakuliacha kabisa suala hili la utunzaji wa kumbukumbu sahihi mikononi mwa wanadamu. Njia zao za kuhesabu wakati unaopita, kuhesabu siku zao, kalenda zao pamoja na Kalenda maalum za miezi, siku, na miendo ya jua, mwezi na nyota (almanacs), havina haja ya

kuchukuliwa kama ndivyo vigezo pekee vya kutegemewa katika kuipata siku ile ya saba. Mungu anayo njia yake tunayoweza kuitegemea kabisa kwa usalama katika kutunza mambo Yake aliyoyaweka na maagizo Yake, pamoja na watu Wake.

Kwa kweli hapawezi kuwa na swali lo lote juu ya kwamba Mungu aliweka umuhimu Wake mkubwa sana katika utunzaji wa Sabato ya siku ile ya Saba. Alishuka toka mbinguni katika Mlima ule wa Sinai, na katika usikivu wa labda watu wapatao milioni tatu akasema maneno ya sheria ile ya Amri Kumi. Miongoni mwa maneno yaliyosikika toka kinywani mwake ni haya: "Lakini siku ya saba ni sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote" (Kutoka 20:10).

Mungu aliweka adhabu ya wazi kabisa na nzito kwa kuivunja amri hii. Alitangaza kwamba uvunjaji wa sheria yake ni dhambi. "Kila mtu atendaye dhambi anavunja sheria ya Mungu, maana dhambi ni uvunjaji wa sheria" (l Yohana 3:4, AJKK).

Dhambi inatangazwa kuwa adhabu yake ni mauti. "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti" (Warumi 6:23).

Hivyo inaweza kuonekana wazi ya kwamba lilikuwa jambo kubwa sana la maana kujua siku ipi ilikuwa siku ya saba. Kutojua ilikuwa ni kujiweka katika hatari ya kuivunja sheria ya Mungu. Hivyo ndivyo mtu angalivyoweza kupata adhabu ya kifo.

## SIKU ZA UUMBAJI

Siku za uumbaji ni sawasawa na siku hizi tunazozizoea sasa, zikiwa na sehemu ya giza iitwayo jioni, au usiku, na sehemu yenye nuru iitwayo asubuhi, au mchana.

Siku zile za uumbaji hazikuwa vipindi virefu vya wakati [mabilioni ya miaka] kama wengi wanavyodhani kwa kupotoka, bali zilikuwa na muda ule ule kama zilivyo siku zetu leo ----- zilikuwa na jioni na asubuhi, au sehemu yenye giza na sehemu yenye nuru ----- kwa kadiri dunia yetu ilivyoendelea kuzunguka kwenye mhimili wake. Jambo hili litadhihirishwa na kumbukumbu za Mungu: "Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru. Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza. Mungu akaiita nuru Mchana; na giza akaliita Usiku. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja [siku ya kwanza]" (Mwanzo l:3-5).

Ni dhahiri, hii ilikuwa ni siku halisi, ikiwa na jioni yake na asubuhi yake, sehemu yake ya giza ikija kwanza na sehemu yake ya nuru ikimalizia.

Kama inavyoendelea kueleza kumbukumbu hii ya juma lile la Uumbaji, kazi ya kila siku ilimalizika kwa maneno haya, "Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya pili"; "Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tatu"; "Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya nne"; "Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tano"; "Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya sita" (Mwanzo l:8,13,19,23,31).

## NI SIKU HALISI

Hakuna lugha nyingine yo yote ambayo ingechaguliwa na mwandishi huyu aliyevuviwa ambayo ingeliweka wazi sana wazo hili la Mungu kuliko maneno haya yanavyoliweka. Hakuna maneno mengine yanayoweza kupatikana katika lugha ya Kiebrania ambayo yanaweza kulielezea wazo hili la siku halisi kwa nguvu zaidi kuliko maneno yale yaliyotumika hapa.

Palikuwa na siku ya kwanza, siku ya pili, siku ya tatu, na kuendelea mpaka siku ya saba; kila moja ya siku hizi ilianza na jioni na asubuhi halisi yenye mipaka yake dhahiri. Tafsiri ya neno kwa neno ya Kiebrania inasema hivi: "Palikuwa na jioni, palikuwa na asubuhi, siku ya kwanza"; "palikuwa na jioni, palikuwa na asubuhi, siku ya pili," na kadhalika.

Kuna kila sababu ya kuamini kwamba mwandishi huyu aliyevuviwa kuyaandika maneno haya, yaani, Musa, mtu huyu wa Mungu, alielewa na alikusudia wasomaji wake wapate kuelewa kwamba siku hizi zilikuwa ni siku halisi za kawaida. Kwa kweli hakuwa na mawazo yo yote moyoni mwake yanayofanana na yale yanayopendekezwa na jiolojia ya siku hizi iliyojengwa juu ya misingi ya evalusheni (modern evolutionistic geology).

Yehova aliposhuka Mlimani Sinai kutoa sheria Yake, alizitaja siku hizo za Uumbaji kama ni siku halisi, naye alikusudia watu Wake wapate kuzielewa hivyo. Sababu aliyotoa kwa kuikumbuka siku hii ya Sabato ni kwamba "kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba." Hakuna moyo wo wote ulio mnyofu utakaoweza kuyasoma maneno haya na kufikia hitimisho lililo tofauti kuliko lile la kusema kwamba zile SIKU SITA, pamoja na ile YA SABA, zilikuwa ni siku halisi za kawaida.

Wala hakuna sababu nyingine yo yote ya kutafuta maana nyingine kuliko hiyo. Kama Mungu aliumba nchi, kwa nini asingeweza kuiumba kwa siku sita? Kwa nini angehitaji muda mrefu zaidi kuliko huo kwa KUSEMA tu na vitu kutokea? Hatuna shukrani yo yote kwa wale ambao, kwa kutaka kuondoa matatizo ya kumbukumbu hii, wamebuni maelezo ya nadharia tupu na ya kujitungia wenyewe tu kama waotao ndoto kwa kutoa maelezo ya vipindi virefu mno vya wakati [kuziwakilisha siku saba za uumbaji]. Maelezo kama hayo ndani yake yana matatizo mengi na makubwa sana kuliko yale wanayotaka kuyakwepa. Tunakataa kupoteza kila kitu na kutopata cho chote kwa kuacha kutumia tafsiri zile zilizo rahisi na za kawaida na za kweli kuhusu kumbukumbu hizi za Uumbaji ambazo zimo katika Maandiko.

Kwa hiyo, hizo zilikuwa ni siku za kwelikweli, kama vile tunavyozijua siku za sasa, sio vipindi virefu mno vya wakati kama wanaevalusheni (evolutionists) wanavyosema.

## JE, SIKU YA SABA YA KWANZA YAWEZA KUPATIKANA LEO?

Ndipo katika siku ile ya saba ya juma lile la uumbaji Mungu akafanya mambo fulani tofauti. Siku ile Yeye aka"starehe... akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya." Basi, kwa sababu

alikuwa amestarehe siku ile ya saba, "Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa." (Angalia Mwanzo 2:1-3.)

Swali linaloulizwa ni hili: Je! inawezekana sasa kuipata na kuiweka mahali pake siku ile iliyobarikiwa, takatifu, siku ya awali ya mapumziko aliyoiweka Muumbaji? Hakuna shaka lo lote kwamba ilitolewa kwa mwanadamu kama Sabato, na kwamba ilikuwa ni Sabato wakati ule, na ya kwamba Mungu alikusudia utunzaji wake na wanadamu ungewaletea mbaraka na kuwa njia ya kupatia neema Yake.

Lakini, je! inaweza kupatikana sasa? Je, kuna uwezekano wo wote wa kuitambua kabisa kabisa ile siku ya saba ya kwanza na kuondoa mashaka yote, pamoja na kwamba karne nyingi zimepita na palikuwa na kalenda za muda mfupi zilizobadilikabadilika?

Hebu maneno haya na yaandikwe hapa kwa mara ya kwanza na yasimame milele: Mungu hajaisahau siku yake takatifu; Hajaiacha ipotee vivi hivi tu bila kupatikana tena, Hajauacha utunzaji wake kutegemea mahesabu ya wanadamu wenye dhambi, naye anao uwezo kamili wa kuwaonyesha bila kukosea wale wote waliokata shauri kufanya mapenzi Yake.

## NI KAWAIDA ILIYO YA ZAMANI KAMA HISTORIA ILIVYO

Kuna kawaida moja iliyotujia sisi kupitia katika vizazi vyote toka wakati ule wa mwanzo kabisa mpaka huu wa sasa. Kawaida hiyo inajulikana kama JUMA. Ni kipindi cha wakati kilicho na siku saba. Kilijulikana miongoni mwa mataifa mbalimbali pamoja na kabila za watu katika vizazi vyote vilivyopita.

Kila kipindi cha wakati cha aina nyingine [tofauti na juma] au kuzikusanya siku katika kundi moja, kimetawaliwa na mwendo fulani wa mianga ya mbinguni (heavenly bodies). Lakini hilo si kweli kuhusu hili juma. Hakuna mwendo wo wote wa mianga ya mbinguni, yaani, wa jua, au mwezi, au nyota, au sayari, ambao unaamua urefu wa juma utakavyokuwa.

Mwaka unahesabiwa kwa kufuata muda ule ambao dunia inachukua kumaliza mzunguko mmoja wa jua. Mwezi unahesabiwa kwa kutegemea mzunguko wa mwezi kuizunguka dunia hii. Siku inahesabiwa kwa kufuata mzunguko wa dunia katika mhimili wake.

Walakini muda wa juma haufuati utaratibu wo wote ule, yaani, hakuna kitu cho chote katika maumbile kinachopanga kuwako kwa mkusanyiko wa siku saba kama huo. Hakuna mwanga wo wote wa mbinguni unaoizunguka dunia, au jua, au mwezi, au nyota, au sayari yo yote, au unaozungukwa na hivyo vyote kwa muda huo wa siku saba.

## MWANZO WA JUMA

Basi, ni kwa vipi juma hili lilianza? Tutaiacha 'ENCYCLOPAEDIA BRITANNICA' itoe jibu:

"Juma ni kipindi cha siku saba, halina uhusiano wo wote na miendo ya mianga yo yote iliyoko mbinguni ----- hili ndilo jambo ambalo kwalo [juma] linapata ulinganifu wake usiobadilika.... Limetumika tangu zama za kale sana zisizoweza kukumbukwa karibu katika nchi zote za Mashariki; na kwa kuwa haliwi sehemu yo yote dhahiri ya mwaka wala ya mwezi unaohesabiwa kwa kuangalia mwezi mbinguni, basi, hao wanaoyakataa maneno ya Musa, kama anenavyo Delambre, hawatajua la kufanya wanapotaka kuliwekea [juma] chanzo chake ambacho ni sawa na kubahatisha tu." ----- Toleo la Kumi na moja, Gombo la IV, uk.988, Makala "Kalenda."

Mawazo pia yanaelekezwa kwa mambo yafuatayo yaliyoonwa na Thomas Hartwell Horne, katika kitabu chake cha 'AN INTRODUCTION TO THE CRITICAL STUDY AND KNOWLEDGE OF THE HOLY SCRIPTURES':

"Mojawapo ya uthibitisho unaojitokeza sana unaokwenda sambamba na historia ya Musa ya uumbaji ni matumizi ya kawaida ya mgawanyo wa wakati katika MAJUMA, ambao unaenea toka nchi zile za Kikristo za Ulaya mpaka pwani za mbali za Hindustani, na vile vile limeendelea kutumika miongoni mwa Waebrania, Wamisri, Wachina, Wayunani [Wagiriki], Warumi, na washenzi [wapagani] wa kaskazini ----- mataifa ambayo baadhi yao yalikuwa na mawasiliano kidogo au hayakuwa na mawasiliano yo yote na [mataifa] mengine, na hata hayakufahamika kwa majina na Waebrania." ----- Toleo la l825, Gombo la I, Sura ya 3, Sehemu ya 2, Aya ya 1, uk.l63.

Dkt. Lyman Coleman anasema maneno haya:

"Saba ni hesabu ya kale ambayo inaheshimiwa miongoni mwa mataifa ya ulimwengu. Wameupima wakati wao kwa kutumia majuma tangu mwanzo. Asili yake ilikuwa ni ile Sabato ya Mungu, kama vile Musa alivyokwisha kutoa sababu kwayo katika maandiko yake." ----- BRIEF DISSERTATIONS ON THE FIRST THREE CHAPTERS OF GENESIS, UK.26.

## LILIJULIKANA TANGU ZAMANI SANA

Bodi ya Uchapishaji ya Kanisa la Presbyterian, katika Kijizuu (Tract) chake Na.271, cha 'THE CHRISTIAN SABBATH' kinatoa maelezo haya:

"Mgawanyo wa wakati katika majuma sio tu WA ASILI, bali kwa maana nyingine ni KINYUME NA ASILI, kwa vile juma hili la siku saba sio mgawanyo mdogo wa aidha mwezi au mwaka unaohesabiwa kwa njia ile ya kawaida. Lakini kipimo hiki cha wakati wa siku saba kinaweza kufuatiwa sio tu katika historia takatifu kabla ya kizazi kile cha Musa, bali katika ustaarabu wote wa kale wa kila kizazi, wengi wao ambao haiwezekani kwamba wangekuwa wamelipata wazo hilo toka kwa Musa.... Miongoni mwa wasomi wa Misri, Wabrahmani wa India, Waarabu, Waashuru, kama zinavyoweza kukusanywa taarifa kutoka kwa wanajimu wao na makuhani, mgawanyo huo [wa majuma] ulijulikana. Hesiod (900 K.K.) anatangaza kwamba siku ya saba ni takatifu. Naye Homer na Callimachus wanasema vivyo hivyo. Hata

katika hadithi za miungu ya Wasaksoni (Saxon mythology) mgawanyo huo kwa majuma unaonekana wazi. Ndio, hata miongoni mwa makabila ya Afrika yanayoabudu mashetani, tunaambiwa ya kwamba jambo la pekee la dini yao ni siku takatifu ya kila juma, uvunjaji wake kwa kufanya kazi ambao utaleta ghadhabu ya mungu wao shetani. Dalili za mgawanyo huo wa wakati zimeonekana miongoni mwa Wahindi [Wekundu] wa Kontinenti lile la Amerika. Sasa, ni nadharia gani nyingine ambayo kwayo ukweli huu unaweza kuelezeka isipokuwa ni kwa kuhisi kwamba ni ile Sabato iliyoamriwa na Mungu tangu mwanzo wa kuwako taifa la kibinadamu?" ----- BOUND TRACTS, Vol. XII, uk.5-7.

## SIKU YA SABA KUENDELEA KUTUNZWA BILA KUKATIZWA

Alexander Campbell, mwasisi wa dhehebu lililojulikana kama 'Christian Church', katika HOTUBA zake ZILIZOPENDWA SANA (POPULAR LECTURES), asema maneno haya:

"Mbingu hazikuuacha ukweli huu, yaani, uumbaji, kuwa ndio msingi wa kuandikwa magombo maelfu, yaliyokusanya habari zake kutokana na mawazo ya kinadharia, mapokeo potofu, mifano iliyobuniwa kwa werevu, ama dhana zinazoonekana kana kwamba ni za kweli, bali kutokana na KUMBUKUMBU iliyowekwa ambayo ilikuwa YA ULIMWENGU MZIMA iliyo sawa na habari za miaka ya wakati, kama vile kuzaliwa kwa mataifa, na lugha zilizozungumzwa na wanadamu wenye hali ya kufa. Pia ile kawaida ambayo, bila kujali madai yake, sio tu ya sehemu ya saba ya wakati wote, bali ya SIKU YA SABA ambayo iliendelea kutunzwa pasipo kukatizwa, ilisherehekewa tangu wakati wa uumbaji mpaka wakati ule wa Gharika, wakati wa Gharika yenyewe, na baada ya Gharika mpaka hapo sheria ilipotolewa [Mlimani Sinai]." ----- Ukurasa 283, 284.

Mwandishi yuyo huyo, katika kitabu chake cha 'EVIDENCES OF CHRISTIANITY', anatangaza hivi:

"Siku ya saba ilitunzwa tangu siku za Ibrahimu, la, tangu uumbaji." ----- Ukurasa 302.

Mwanahistoria Myahudi wa zamani, Josephus, katika kitabu chake cha 'AGAINST APION', anasema:

"Hakuna mji wo wote wa Wayunani, wala ule wa washenzi [wapagani], wala taifa liwalo lote, ambako desturi yetu ya kupumzika siku ya saba haijafika." ----- Kitabu cha 2, Aya ya 40, katika 'WORKS OF FLAVIUS JOSEPHUS (Winston ed.), uk.899.

Kwa kuwa Sabato ilitengwa na Mungu tangu siku ile ya saba ya mwanzo wa wakati wa dunia hii, basi, kipindi hiki cha juma kilijulikana tangu mwanzo. Pia ni dhahiri ya kwamba juma hilo lilijulikana na Nuhu wakati ule wa Gharika.

"Akangoja na SIKU SABA TENA; kisha akamtoa yule njiwa katika safina mara ya pili, njiwa akamjia jioni, na tazama, alikuwa na jani bichi la mzeituni kinywani mwake, ambalo amelitunda, basi Nuhu akajua ya kwamba maji yamepunguka juu ya nchi. Akangoja na SIKU SABA TENA, akamtoa yule njiwa; naye asimrudie tena kamwe" (Mwanzo 8:l0-l2).

Sasa, ni kitu gani, kwa njia isiyokuwa ya kawaida, pasipo kufuata mwendo wo wote wa mianga ile ya mbinguni [jua, mwezi, nyota, n.k.] ambacho huliwekea mipaka yake juma hili ambalo kipindi chake hakibadiliki kamwe?

Kuna jibu moja tu, nalo ni hili: Ni kule kuendelea daima bila kukoma kwa Sabato ya Bwana kwa kila siku saba.

Sabato hii ya siku ya saba imetunzwa bila kukatizwa kwa mfululizo katika karne zote zilizopita. Ilikuwa haijapotea kabla ya siku zake Kristo. Tangu hapo haijapotea. Yehova, aliyeifanya, ameihifadhi, na kuionyesha kwa watu wake kama Sabato Yake tena na tena.

Zaidi ya miaka elfu mbili na mia tano baada ya Uumbaji, Mungu alichukua wasaa kuonyesha wazi ipi ilikuwa ndiyo siku ya saba ya awali, naye aliionyesha kwa njia ambayo hata kama pangekuwa na kuchanganyikiwa ko kote mioyoni mwa watu Wake kabla yake, hakuna ambako kungeendelea kubakia baada ya Yeye kukamilisha kuitambulisha siku Yake takatifu.

Kumbukumbu ya kile alichofanya na jinsi alivyoitambulisha siku hiyo ----- siku ile ile hasa ya saba ya kwanza ----- itapatikana katika sura ya kumi na sita ya kitabu cha Kutoka. Ni kisa cha kudondoka kwa mana jangwani.

## SIKU YA SABA ILE ILE ILIONYESHWA NA MUNGU

"Na ulipoinuka ule umande uliokuwa juu ya nchi, kumbe! juu ya uso wa bara kitu kidogo kilichoviringana, kidogo kama sakitu juu ya nchi. Wana wa Israeli walipokiona, wakaambiana, Nini hiki? maana hawakujua ni kitu gani. Musa akawaambia, Ndio mkate ambao BWANA amewapa ninyi, mle. Neno hili ndilo aliloagiza BWANA, Okoteni ninyi kitu hicho kila mtu kama ulaji wake ulivyo; ndivyo mtakavyotwaa, kila mtu kwa ajili ya hao walioko hemani mwake.

"Wana wa Israeli wakafanya hivyo, wakaokota wengine zaidi, wengine kupungua. Nao walipoipima kwa pishi, yeye aliyekuwa ameokota kingi hakubakiwa na kitu, na yeye aliyekuwa ameokota kichache hakupungukiwa, wakaokota kila mtu kama ulaji wake ulivyokuwa. Musa akawaambia, Mtu awaye yote asikisaze hata asubuhi. Lakini hawakumsikiza Musa; wengine miongoni mwao wakakisaza hata asubuhi, nacho kikaingia mabuu na kutoa uvundo; Musa akawakasirikia sana. Basi wakaokota asubuhi baada ya asubuhi... na hapo jua lilipokuwa ni kali, kikayeyuka.

"Basi ikawa siku ya sita wakaokota kile chakula sehemu maradufu, kila mtu pishi mbili; na wazee wote wa mkutano wakaenda na kumwambia Musa. Akawaambia, ndilo neno alilonena BWANA, Kesho ni starehe takatifu, Sabato takatifu kwa BWANA.... Basi wakakiweka hata asubuhi, kama Musa alivyowaagiza; nacho hakikutoa uvundo wala kuingia mabuu.

"Musa akasema, Haya, kuleni hiki leo; kwa kuwa leo ni sabato ya BWANA; leo hamtakiona nje barani. Siku sita mtaokota; lakini siku ya saba ni sabato, siku hiyo hakitapatikana.

"Ikawa siku ya saba wengine wakatoka kwenda kukiokota, wasikione. BWANA akamwambia Musa, Mtakataa kuyashika maagizo yangu na sheria zangu hata lini? Angalieni, kwa kuwa BWANA amewapa ninyi hiyo sabato, kwa sababu hii huwapa siku ya sita chakula cha siku mbili; kaeni kila mtu mahali pake kwa siku ya saba. Basi hao watu wakapumzika kwa siku ya saba" (Kutoka l6:l4-30).

Hapa Sabato ile ile inaonyeshwa na Mungu, bila kuangalia kalenda zo zote za wanadamu na bila ya kuwa na lhaja ya kuzichunguza kumbukumbu za wanadamu. Aliyezifanya siku, Muumbaji wa mianga ya mbinguni, Bwana wa wakati na umilele, anaridhika kuvionyesha viumbe vyake vinavyokosea na vyenye dhambi siku gani ni siku Yake, yaani, siku ya saba ile ile ya Uumbaji. Hapakuwa na uwezekano wo wote wa kukosea kuitambua siku hiyo. Hakuna ye yote ambaye angeweza kusema kweli kwamba alikuwa hawezi kuiona siku hiyo. Ilikuwa wazi sasa hata hakuna mtu ye yote ambaye angeweza kuipoteza.

## KILA JUMA MIUJIZA DHAHIRI MITATU ILIITAMBULISHA SIKU HIYO

Kwa miujiza dhahiri mitatu Mungu aliitambulisha siku hiyo: Alitoa mana maradufu kuliko kawaida siku ile ya sita; Aliihifadhi mana ile bila kutoa uvundo usiku kucha, ambapo usiku wa siku zile nyingine kilitoa uvundo na hakikuweza kuhifadhiwa; na siku ile ya saba, yaani, siku ile ile ya saba ya uumbaji, siku Yake Mungu, Sabato iliyobarikiwa, Alizuia mana yote isidondoke chini.

Na miujiza hiyo mitatu ilirudiwa kila juma, yaani, majuma hamsini na mbili kwa mwaka, kwa miaka arobaini, wakati wa kutangatanga jangwani kwa Waisraeli.

Yaani, miaka 2,500 kuja upande huu tangu Uumbaji, Bwana wa Sabato alichukua jukumu Mwenyewe kuonyesha siku karibu 2,080 za siku ya saba ile ile pasiwepo na haja ya kukosea kuitambua Sabato.

La, Sabato ya siku ya saba sio ngumu kuiona. Kinyume chake, ni vigumu kabisa kuipoteza.

Waisraeli wameendelea kuitunza siku ile ile, iliyokuwa imeonyeshwa kwa njia hiyo, katika karne zote zilizopita bila kuipoteza tangu wakati ule au kuchanganyikiwa kuhusu siku hiyo. Wakaingia katika kiapo kutembea katika sheria ya Mungu, hasa kuhusu utunzaji wa Sabato.

"Nao wakaingia katika laana na kiapo, ya kuwa wataiendea torati [sheria] ya Mungu... na kuziangalia, na kuzitenda, amri zote za BWANA, Bwana wetu, na hukumu zake na sheria zake... tena watu wa nchi wakitembeza biashara, au chakula cho chote, siku ya Sabato, tusinunue kwao siku ya Sabato" (Nehemia l0:29-3l).

Hawakuwa na kalenda ya Gregory (Gregorian calendar) ambayo sisi tunayo. Hawakuihitaji ili kuhesabu saba. Mwisho wa kila kipindi cha siku saba waliiadhimisha Sabato takatifu.

## SABATO HAIKUBADILIKA KUTOKANA NA MABADILIKO YA KALENDA

Kalenda zimebadilika, bali juma kamwe halijavurugika tangu mwanzo wa wakati. Bila kujali mifumo yote ya kuhesabu wakati, ingawa pamekuwa na mabadiliko toka kalenda moja kwenda nyingine, ingawa pamekuwa na makosa mengi yaliyofanywa na wanadamu, mfululizo huo wa juma unaendelea bila kuvunjika kwenda nyuma mpaka mwanzo kabisa Mungu alipoumba vitu vyote. Huwezi kuipoteza Sabato. Kuja kwake [Sabato] na kurudi kwake tena na tena hakutegemei hesabu za wanadamu zinazobadilikabadilika, bali kunategemea uwezo usio na kikomo na hekima isiyo na kikomo ya Bwana Mungu wetu.

Miaka elfu nne kuja upande huu tangu Uumbaji, kwa mara moja tena tunaikuta siku ya saba ile ile ikiwa imeonyeshwa kwa dhahiri, safari hii tunaikuta katika Agano Jipya. Ni tukio lile la kusulibiwa na ufufuo wa Bwana wetu. Kumbukumbu ni hii:

"Mtu huyo [Yusufu wa Arimathea] alikwenda kwa Pilato, akataka kupewa mwili wa Yesu. Akaushusha, akauzinga sanda ya kitani, akauweka katika kaburi lililochongwa mwambani, ambalo hajalazwa mtu bado ndani yake. Na SIKU ILE ilikuwa siku ya Maandalio, na Sabato ikaanza kuingia. Na wale wanawake waliokuja naye toka Galilaya walifuata, wakaliona kaburi, na jinsi mwili wake ulivyowekwa. Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na SIKU YA SABATO WALISTAREHE KAMA ILIVYOAMRIWA [Kutoka 20:8-ll]. Hata SIKU YA KWANZA YA JUMA, ilipoanza kupambazuka, wakiyaleta manukato waliyoweka tayari. Wakalikuta lile jiwe limeviringishwa mbali na kaburi" (Luka 23:52 hadi 24:2).

Hapa siku ile aliyosulibiwa, ambayo inajulikana kwamba ilikuwa siku ya Ijumaa, au siku ya sita ya juma, imepewa jina la "siku ya Maandalio." Siku iliyofuata, yaani, ile ya saba, siku ambayo Bwana wa uzima alipumzika kaburini, inajulikana kabisa kama "siku ya Sabato... kama ilivyoamriwa," yaani, ni siku ile ile ya saba ya Uumbaji. Siku iliyofuata, siku ya kwanza ya juma, siku aliyofufuka Bwana wetu kutoka kwa wafu, haijapewa jina, aidha takatifu au la kawaida, bali inasemwa tu kama "siku ya kwanza ya juma."

Kwa hiyo, katika kifungu hiki cha maneno, siku tatu zimewekwa mbele yetu, pamoja na uhusiano wao moja kwa nyingine umeonyeshwa wazi. Siku ya Sabato, "Sabato ... kama ilivyoamriwa," inaonekana hata katika Agano Jipya, kuwa ni siku ile iliyo katikati ya siku ile ya sita, Ijumaa, na siku ile ya kwanza, ambayo siku hizi inaitwa Jumapili. Yaani, Jumapili sio wala haijapata kuwa Sabato ya Agano Jipya. Sabato ile, Sabato ya kweli ya Mungu, ile "Sabato... kama ilivyoamriwa," ni siku iliyo kabla ya Jumapili. Jumapili inapoanza, Sabato ya kweli inakuwa imekwisha pita.

## HAKUNA UWEZEKANO WA KUIPOTEZA SABATO

Wakati ule ule Jumapili ilikuwa inaadhimishwa na waabudu jua. Baadaye, kwa njia ya uasi na kumwacha Mungu, utunzaji wa Jumapili uliingizwa ndani ya kanisa. Haikuletwa kamwe kwa kibali cha Mungu, utunzaji wake hauna sehemu yo yote na Ukristo wa kweli.

Basi, wakati ule pia siku ya saba ilikuwa inatunzwa na Wayahudi. Siku ya kwanza ilitunzwa na waabudu jua. Siku hizi mbili, ya saba na ya kwanza, zimeshikwa kwa mfululizo usiokatizwa, tangu wakati huo, siku ya saba ikitunzwa na Wayahudi na Wakristo Wasabato, siku ya kwanza ikishikwa na waabudu jua, na hatimaye na Wakristo wanaoitunza siku ya Jumapili. Siku hizi mbili, zikiwa zimetunzwa hivyo, zimetujia sisi bila kukatika mfululizo wake, zikitunzwa juma kwa juma katika karne zote za Kikristo, pasipokuwapo uwezekano wo wote wa kupotea.

Kwa hiyo tunaweza kuifuatilia Sabato kupitia katika miaka yote katikati ya Uumbaji na wakati huu wa sasa. Haijapotea. Hapajakuwa na badiliko lo lote katika siku hiyo. Ni Sabato ile ile SASA kama ilivyokuwa wakati ULE ilipokuwa imetoka mkononi mwake Mungu. Ilifanywa kwa kuichukua siku ile ya saba. Nasema tena, mbali na kushindwa kuipata siku ya saba, ukweli ni kwamba hatuwezi kuipoteza.

Swali linaulizwa, lakini, je! kalenda hazijabadilishwa mara nyingi, na mabadiliko kama hayo hayajaleta matokeo ya kuibadili Sabato? Swali hili, pia, tutalichunguza.

# SURA YA 6

## BADILIKO LA KALENDA

Kalenda ya Gregory, ambayo sasa inatumika ulimwenguni kote, iko sawasawa na ni sahihi. Itakuwa msaada kwa msomaji kuiweka mbele ya macho yake kalenda hiyo kwa uchunguzi wa

makini tunapoanza kujifunza mabadiliko yaliyofanya ianze kutumika. Naam, ni ile uliyo nayo inayoning'inia ukutani.

Angalia hasa mpangilio wake wa siku za juma. Jumapili ni siku ya kwanza, Jumatatu ni ya pili, Jumanne ni ya tatu, Jumatano ni ya nne, Alhamisi ni ya tano, Ijumaa ni ya sita, na Jumamosi ni ya saba.

Majina ambayo siku hizi zimepewa yote ni ya kipagani kwa asili yake. Jumapili (SUNday) imetajwa kwa ajili ya jua, yaani, ni siku ya jua; Jumatatu (MONday) kwa ajili ya mwezi; Jumanne (TUESday) kwa mungu wa kike Tiw; Jumatano (WEDNESday) kwa mungu wa vita wa kale wa Kijerumani aliyeitwa Woden; Alhamisi (THURSday) kwa mungu wa zamani wa radi wa nchi za Skandinavia aliyeitwa Thor; Ijumaa (FRIday) kwa mungu wa kike Frigga; na Jumamosi (SATURday) kwa mungu Sarateni. Majina ya Kilatini ya zamani kwa mpangilio uo huo ni kama ifuatavyo: DIES SOLIS, DIES LUNAE, DIES MARTIS, DIES MERCURII, DIES JOVIS, DIES VENERIS, DIES SATURNI, na majina hayo yakiwa yametolewa kwa heshima ya jua (sun), mwezi (moon), Mihiri (Mars), Zebaki (Mercury), mungu wa Kirumi (Jove), Zuhura (Venus), na Sarateni (Saturn), kwa mfuatano wake.

Ni wazo la watu wengi kudhani kwamba mabadiliko mengi yametokea katika kalenda mbalimbali kati ya wakati ule wa Kristo na huu wetu. Hii sio kweli. Pamekuwa na badiliko moja tu, badiliko toka Kalenda ya Julius [Julyasi] (Julian calendar) kwenda ile ya Gregory (Gregorian calendar). Na badiliko lile halikuwa na athari yo yote kwa siku za juma. Hapajakuwa na badiliko lo lote katika siku za juma tangu siku zake Kristo, wala hapakuwa na badiliko lo lote kabla yake, kwa kadiri kumbukumbu zinavyoonyesha. Siku za mwezi zilibadilishwa wakati wa kuitumia kalenda ya Gregori, lakini sio siku za juma. Hizo zimebaki pasipo badiliko lo lote tangu mwanzo na ni zile zile sasa kama zilivyokuwa katika historia iliyopita.

Kalenda ile iliyotumika kule Palestina na katika majimbo yote ya Dola ya Kirumi wakati wa siku zake Kristo ilijulikana kama Kalenda ya Julyasi. Ilianza kutumika kwa idhini ya mamlaka ya na wakati wa Kaisari Julyasi, nayo inaitwa kwa jina lake. Ilitangazwa rasmi mwaka ule wa 708 wa mji wa Rumi, karibu na mwaka 46 K.K.

Kaisari Julyasi alipenda kujionyesha kuwa yeye alikuwa mtu mashuhuri sana. Akajitwalia haki nyingi. Akauita mwezi ule wa saba kwa jina lake mwenyewe, na mpaka leo unaitwa Julai, kufuatia jina lake la Julyasi. Inasemekana kwamba katika kuchagua mwezi huu aliouita kwa jina lake mwenyewe, alikuwa mwangalifu kuchagua ule uliokuwa na siku thelathini na moja. Kaisari Augusto (Augustus Caesar), aliyembadili Julyasi, alijihesabu mwenyewe kuwa hakuwa na upungufu wo wote kwa kujilinganisha na Julyasi, na wakati alipoupa mwezi wa Agosti (August) jina lake mwenyewe, aliongeza siku nyingine moja kwa mwezi huo, ambayo aliitwaa toka mwezi wa Februari, ili uwe na idadi ile ile ya siku kama Julai.

## KALENDA YA JULYASI HAIKUWA SAHIHI

Kalenda ya Julyasi ilitumika kwa karne kumi na tano baada ya Kristo karibu katika ulimwengu wote uliostaarabika. Walakini haikuwa kalenda iliyo sahihi. Ilichukuliwa kwamba urefu wa mwaka mmoja wa jua (calendar year) ni siku 365 1/4, ambapo ni dakika kumi na moja na nukta chache chini ya hapo. Hilo halionekani kama ni kosa kubwa, lakini miaka mingi inapopita linaongezeka. Matokeo yake ni kwamba chini ya Kalenda ya Julyasi wakati kidogo ulipotea kila mwaka; yaani, haikufuata sawasawa mwendo ule wa mianga ya mbinguni, na matokeo yake ni kwamba mwaka baada ya mwaka, majira yale ya jua kuwa kichwani (vernal equinox, March 2lst), katika nchi zilizo kaskazini ya Ikweta, yalitokea karibu na Machi 25 wakati ule wa Julyasi, na pole pole yakarudishwa nyuma hadi Machi mosi. Kufikia mwanzo wa karne ya kumi na sita baada ya Kristo [majira] yalikuwa yanatokea karibu na Machi 11.

Mbali huko nyuma kama karne ya kumi na tatu, wataalam wa nyota (astronomers) wakaanza kuandika juu ya makosa yaliyomo katika Kalenda ya Julyasi. Baadhi ya nchi za Ulaya zikataka kuchukua hatua zikitarajia kufanya marekebisho ya kalenda ile. Lakini hakuna lo lote lililofanyika kwa muda mrefu kwa sababu uongozi na mapatano yalikuwa ni mambo muhimu kuwapo ili kuanzisha marekebisho ya kalenda ambayo yangeleta umoja katika nchi zote.

## TOKA KALENDA YA JULYASI KWENDA YA GREGORI

Hatimaye ushirikiano na upendeleo wa Upapa ulishirikishwa. Chini ya Papa Gregori wa XIII kalenda ile ilibadilishwa, na masahihisho ya SIKU KUMI yalifanyika ili kuyarudisha majira ya jua kuwa kichwani hadi Machi 21 (vernal equinox, March 2lst), siku ambayo jua lilikuwa kichwani wakati wa Baraza la Nicaea mwaka 325 wakati suala la kuadhimisha sikukuu ya Pasaka (Easter celebration) lilipoamuliwa na baraza lile la Kanisa. (Angalia CATHOLIC ENCYCLOPEDIA, Vol. III, uk.l68,l69, art. "Calendar, Reform of the"). Alitoa tangazo la kipapa, akizifuta siku zile KUMI, ili siku ile ambayo ingekuwa tarehe 5 Oktoba, l582, ihesabike kama tarehe 15 Oktoba. Kalenda ile mpya ikapewa jina la papa yule ambaye katika mwaka wake wa utawala kalenda ile mpya ilianza kutumika, yaani, Papa Gregori. Kwa hiyo, inajulikana kama Kalenda ya Gregori (Gregorian calendar).

Kalenda ya Gregori, ambayo sasa unaitumia nyumbani mwako, na ambayo karibu ulimwengu wote unaitumia kuhesabu wakati, kama ilivyosemwa huko nyuma, ilianza kutumika kwa tangazo la Papa wa Rumi mwaka 1582 B.K. Badiliko lililofanya kalenda hiyo iweko, yaani, lile badiliko la siku kumi kati ya kalenda ya Julyasi ya zamani, lilifanyika siku ya Ijumaa, Oktoba 5, 1582. Njia iliyotumika kuzirekebisha siku zile kumi ilikuwa tu kuiita siku ile, ambayo chini ya Kalenda ya Julyasi ilikuwa tarehe 5 Oktoba kuwa tarehe 15 Oktoba. Hayo ndiyo yote yaliyofanyika. Na jambo hilo lilifanya kalenda ya mwaka ikubaliane na majira ya jua kuwa kichwani katika nchi za kaskazini ya Ikweta (vernal equinox, [March 2lst]).

## HAKUNA TOFAUTI YO YOTE KATIKA SABATO

Siku ile bado ilikuwa ni siku ya Ijumaa, lakini badala ya kuwa Ijumaa tarehe 5, ikawa Ijumaa tarehe 15. Hapakuwa na badiliko lo lote la mwezi. Ulikuwa bado ni mwezi wa Oktoba. Hapakuwa na tofauti yo yote katika siku ya juma lile. Ilikuwa bado ni siku ya Ijumaa ile ile. Tofauti ilikuwa katika tarehe ya mwezi ule. Ilikuwa tarehe 15 badala ya tarehe 5. Hayo ndiyo yote.

Siku iliyofuata ilikuwa Jumamosi, sawa na vile ambavyo ingalikuwa endapo kalenda ile isingebadilishwa. Isipokuwa ilikuwa tu ni tarehe kumi na sita badala ya tarehe sita. Badiliko hilo la kalenda halikuleta badiliko lo lote katika Sabato ya Bwana, wala halileti ugumu wo wote katika kuitambua sasa siku ya saba ile ile.

Hispania, Ureno, na Italia mara moja zikaanza kuitumia kalenda hiyo ya Gregori. Kitambo kidogo baadaye katika mwaka ule wa 1582, Ufaransa nayo ikaanza kuitumia, kwa kuiita tarehe 10 ya Desemba kuwa ni tarehe 20. Majimbo ya Kikatoliki yanayojitawala (catholic states) kule Ujerumani yakaanza kuitumia kalenda hiyo mpya katika mwaka 1583, bali katika majimbo ya Kiprotestanti yanayojitawala (Protestant states) kule Ujerumani mtindo ule wa zamani au Kalenda ya Julyasi iliendelea kutumika hadi mwaka 1700. Katika mwaka huo nchi za Eneo la Chini (Low Countries) kama zilivyoitwa, au 'Netherlands,' zikaanza kuitumia kalenda ile mpya. Hawakuwa na urafiki wo wote na Upapa, na kwa ajili hiyo hawakuharakisha kupokea kitu cho chote walichodhani kimetoka kwa papa.

Uingereza haikuitumia kalenda hiyo mpya mpaka mwaka ule wa 1752. Sweden na Denmark waliikubali karibu kwa wakati ule ule kama yalivyofanya majimbo yanayojitawala ya Kiprotestanti ya Ujerumani.

## SIKU NI ZILE ZILE KABISA KATIKA KALENDA ZOTE MBILI

Katika kipindi chote hiki wakati nchi nyingine zilikuwa zikihesabu wakati wao chini ya kalenda moja na nyingine chini ya kalenda nyingine, siku za juma zilikuwa ni zile zile katika nchi zote. Ilipokuwa ni Jumamosi kule Hispania na Ureno na Italia, ilikuwa ni Jumamosi pia kule Uingereza, japokuwa hadi kufikia mwaka ule wa 1700 walitofautiana kwa siku kumi katika tarehe zao, na baada ya 1700 wakatofautiana kwa siku kumi na moja.

Uingereza ilikuwa imekataa kuipokea kalenda mpya kwa sababu wakati ule ilikuwa katika harakati ya kuanzisha kile ambacho hatimaye kilikuja kujulikana kama Kanisa la Uingereza (Church of England), nayo haikutaka kitu cho chote kile kinachohusiana na Upapa. Walakini, tofauti hizi katika kuhesabu siku [tarehe] zilileta machafuko na ugumu katika kuendesha shughuli za kibiashara kati ya Uingereza na Bara la Ulaya. Hatimaye wafanya biashara wa Uingereza walileta msukosuko juu ya suala hili hata ikabidi Uingereza ikubali kutumia kalenda ile mpya, ambayo kufikia wakati ule ilijulikana kwamba ilikuwa sahihi na sawasawa.

Katika kujifunza historia mara nyingi mtu ataweza kuona herufi "O.S." ama "N.S." wakati tarehe za matukio fulani zinapotajwa. Herufi hizo ni kwa ajili ya kuonyesha endapo mtindo wa zamani (Old style) au mtindo mpya (New style) wa kalenda ulikuwa unatajwa.

## TAREHE ILIBADILISHWA, LAKINI SIO SIKU

Ilikuwa Septemba 2, 1752 wakati ambapo mtindo mpya wa kalenda, yaani, ya Gregori, ulipokubaliwa na Bunge la Uingereza. Sheria ya Bunge hilo inasomeka tu kwamba siku ile iliyofuata baada ya tarehe 2 Septemba ingeitwa tarehe 14 Septemba. Siku ile ilikuwa ni Alhamisi. Chini ya mtindo wa zamani, au Kalenda ile ya Julyasi, ingalikuwa ni Alhamisi tarehe 3. Sheria ya Bunge iliyoikubali kalenda ile ya Gregori ikaifanya siku hiyo ya Alhamisi kuwa ni tarehe 14. Tofauti kati ya mtindo wa zamani na mtindo mpya kufikia wakati ule ilikuwa siku kumi na moja. Tarehe mbili Septemba ilifuatiwa na tarehe l4 Septemba. Tarehe ya mwezi ule ilibadilishwa lakini sio siku ya juma. Tarehe 2 ilikuwa Jumatano. Siku iliyofuata, tarehe 14, ilikuwa ni Alhamisi. Ingekuwa ni Alhamisi kama badiliko hilo lisingefanyika. Lakini ingekuwa Alhamisi tarehe 3, sasa ikawa Alhamisi tarehe 14. Kufuatia siku hiyo ilikuwa ni siku ya Ijumaa tarehe 15, kisha Jumamosi tarehe l6. Kama badiliko hilo lisingefanyika, basi, Jumamosi hiyo ingekuwa tarehe 5 Septemba. Lakini bado ingekuwa ni Jumamosi. Ilikuwa ni siku ya saba ya juma katika Bara lile la Ulaya; ilikuwa ni siku ya saba kule Uingereza; ilikuwa ni siku ya saba kila mahali. Tarehe zilizowekwa kwa siku ile zilikuwa tofauti katika Bara la Ulaya na kule Uingereza. Sasa zikarekebishwa na kuwa sawa. Lakini siku ile haikubadilishwa. Siku ile haikupotea. Hapakuwa na kuchanganyikiwa ko kote katika suala hilo. Badiliko lililofanywa halikuziathiri hata kidogo siku zile za juma. Ziliendelea na kubaki zile zile tu.

Kuanzia mwaka 1582, kalenda ya mtindo mpya ilipoanza kutumika kule Italia mpaka kufikia mwaka 1752 ilipoanza kutumika kule Uingereza ni miaka 170. Katika kipindi hiki chote cha miaka 170, nchi za Bara lile la Ulaya zilipokuwa zinatumia kalenda hii ya mtindo mpya, Uingereza ilikuwa inatumia kalenda ya mtindo wa zamani. Wakati mmoja walitengana kwa siku kumi katika hesabu zao, hapo baadaye walitengana kwa siku kumi na moja. Lakini katika kipindi chote hiki siku za juma zilikuwa ni zile zile tu katika Bara la Ulaya kama zilivyokuwa kule Uingereza. Hapakuwa na kuchanganyikiwa ko kote juu yake [siku hizo]. Hakika huo ni ushahidi wa kukata maneno kwamba badiliko lile katika kalenda halikuleta tofauti yo yote katika siku zile za juma.

## CHINI YA KALENDA TOFAUTI, LAKINI ZOTE ZIKIWA NA SIKU ZILE ZILE

Urusi na Ugiriki waliendelea kutumia mtindo wa kalenda ya zamani. Walikuwa chini ya utawala wa Kanisa la Kiyunani (Greek Church), ambalo halikuwa na ushirikiano wo wote na jimbo (see) la Rumi; kwa hiyo hawakutaka kutumia kalenda ile mpya. Walakini, Rumania, Serbia, na Uturuki mwishowe wakaanza kuitumia kalenda ile ya Gregori mwaka 1919, na Urusi ya Kisovieti ilifanya badiliko hilo mara tu baada ya mapinduzi. Katika mabadiliko haya yote hayakuathiri siku zile za juma. Kufikia wakati ule tofauti kati ya kalenda hizo mbili ilifikia siku kumi na nne.

Ijapokuwa TAREHE kule Ujerumani hazikuwa sawa na tarehe katika nchi ile ya Urusi, siku zilikuwa ni zile zile tu. Ilipokuwa Jumatatu kule Urusi ilikuwa Jumatatu kule Ujerumani, ingawa zilikuwa chini ya kalenda tofauti. Sabato ilipoingia katika nchi ya Ujerumani, yaani,

siku ile ya saba ya juma, ilikuwa ni Sabato pia kule Urusi, ingawa tarehe juu ya kalenda zilitofautiana kwa siku kumi na nne. Kile ambacho 'ENCYCLOPAEDIA BRITANNICA' ilikiita "ulinganifu usiobadilika" wa juma haujaweza kuathirika kamwe kwa mabadiliko hayo katika kalenda. Hivyo siku ya Sabato haijabadilika au kugeuzwa au kuathirika hata kwa kiwango kidogo sana kutokana na mabadiliko hayo.

Basi, usimruhusu mtu ye yote kukuchanganya mawazo yako kwa kuzungumza juu ya badiliko la kalenda. Wale wanaojua hasa jinsi badiliko hilo lilivyofanyika wanatambua kwamba matumizi ya kalenda mpya yo yote hayakuweza kuziathiri siku za juma kwa njia yo yote ile. Naam, kalenda yenyewe [ya Gregori, sio zile zilizowekwa na baadhi ya makanisa leo] ni mojawapo ya njia ya kuthibitisha uhalisi wa siku ile ile ya saba ya Uumbaji

## NI SIKU ILE ILE YA SABA YA UUMBAJI

Sisi tunasadiki kwamba Biblia inasema kweli. Biblia ndiyo inayoamuru utunzaji wa siku ya saba ya juma. Siku ile ile ya saba inaweza kupatikana kama mtu ye yote anataka kuitafuta. Nayo inaweza kupatikana hata kama mtu ye yote anataka kuipoteza. Jua linapotua [linapozama] siku ya Ijumaa jioni, siku ya saba ya Uumbaji ile ile inaanza kuingia. Ni siku ile ile ya saba ambayo amri ya Mungu inatuagiza kuitunza. Amri ile inatangaza kwamba, "Siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote." Kwa hiyo, jua litakapotua Ijumaa hii ijayo wakati wa jioni, utakuwa umeingia katika saa takatifu.

## SURA YA 7.

# MSIMAMO WA UPROTESTANTI

Msimamo wa Uprotestanti juu ya Sabato ni wa kuchanganyikiwa sana. Sauti nyingi zinapazwa, zikijadili pande zote za hoja hii na kutoa sababu ambazo zote kwa pamoja zinaleta uharibifu tu.

Kutokana na utafiti wa mafundisho ya kawaida ya madhehebu mbalimbali za Kiprotestanti, inadhihirika ya kwamba Wakristo wa Kiprotestanti, katika kuiadhimisha Jumapili, wanajiingiza katika desturi ambayo haina utetezi wo wote unaokubalika katika mafundisho ya Kiprotestanti, na ambayo, kama kanuni ile ya Kiprotestanti ya "Biblia na Biblia peke yake" itazingatiwa, basi, itabidi [desturi hiyo] itupiliwe mbali. Kwa bahati mbaya, desturi inayofuatwa na Waprotestanti sio kwamba siku zote inapatana na mafundisho yao ya Kiprotestanti.

Uprotestanti ulianza kwa kuyakataa mafundisho potofu ya Ukatoliki wa Rumi, nao ukakimbilia Biblia kuwa ndiyo mamlaka pekee katika masuala yanayohusu imani ya Kikristo na kawaida zake. Chillingworth, katika usemi wake uliosifika, aliliweka jukwaa la Waprotestanti kwa maneno ambayo yameungwa mkono, yangestahili kuungwa mkono na Waprotestanti wote wa kweli. Alisema:

## BIBLIA, NA BIBLIA PEKE YAKE

"Biblia, mimi nasema, Biblia peke yake, hiyo ndiyo dini ya Waprotestanti!... Mimi kwa upande wangu, baada ya utafiti wa muda mrefu usiopendelea upande wo wote (kama mimi ninavyosadiki na kutumaini) juu ya ile 'njia ya kweli ya kwenda kwenye raha ya milele,' nakiri wazi kwamba siwezi kupata mahali pa kuweka unyayo wangu kwa raha isipokuwa juu ya mwamba huu peke yake. Naona wazi na kwa macho yangu mwenyewe ya kwamba kuna mapapa wanaopingana na mapapa, mabaraza yanayopingana na mabaraza, Mababa wengine wanaopingana na wengine, Mababa wale wale wanaojipinga wenyewe, kibali cha Mababa wa kizazi kimoja kwenda kinyume na kibali cha Mababa wa kizazi kingine....

"Hakuna kweli inayotosheleza bali ile ya Maandiko peke yake kwa mtu ye yote anayefikiria kujenga juu yake. Kwa hiyo, hayo [Maandiko], na hayo peke yake, ninayo sababu ya kusadiki: hayo ndiyo nitayakiri; kwa mujibu wa hayo mimi nitaishi, na kwa hayo, kama utatokea wakati, sio tu nitakuwa tayari kupoteza maisha yangu, bali hata kwa furaha nitapoteza maisha yangu, japokuwa nitasikitika kwamba Wakristo ndio watakaoniondolea maisha yangu. Unishauri mimi kitu cho chote kutoka katika kitabu hiki, na kutaka kujua kama mimi nakisadiki au la, mradi kisionekane kamwe kuwa hakiwezi kufahamika kwa akili za kibinadamu, mimi nitatia sahihi kwa mkono wangu na kwa moyo wangu, nikijua hakuna ushahidi wo wote utakaokuwa na

nguvu kuliko huu: Mungu kasema hivyo, kwa hiyo ni kweli." ----- THE RELIGION OF PROTESTANTS A SAFE WAY TO SALVATION (1846), uk.463

Dkt. John Dowling, ambaye kwa miaka mingi alikuwa mchungaji wa Kanisa la Kibaptisti la Berea katika mji mkuu wa New York, aliandika kitabu cha 'HISTORY OF ROMANISM,' ambamo alirudia usemi huo wa Chillingworth, na kisha aliendelea kuongeza yafuatayo:

"'Biblia, mimi nasema, Biblia peke yeke, hiyo ndiyo dini ya Waprotestanti!' Wala haina maana yo yote katika tathmini ya Mprotestanti wa kweli kujua ni MAPEMA JINSI GANI fundisho hilo lilianzishwa, kama halipatikani katika Biblia.... Kwa hiyo, kama fundisho lo lote linatolewa kwake ili alikubali, anauliza, Je, linapatikana katika Neno la Mungu lililovuviwa? Je, lilifundishwa na Bwana Yesu Kristo pamoja na Mitume Wake? Kama hawakujua cho chote juu yake [fundisho], haidhuru kama kwake [anayelitoa] aliligundua katika kitabu kikubwa chenye kuvu cha mwota ndoto gani wa zamani wa karne ya tatu au ya nne, au katika ubongo wa mwota ndoto wa siku hizi yupi wa karne hii ya kumi na tisa, kama halipatikani katika Maandiko Matakatifu, basi, halina madai halali ya kupokewa kama sharti la imani yake.... Ye yote ambaye anapokea fundisho hata kama ni moja kwa kufuata mamlaka ya mapokeo, hebu na aitwe kwa jina liwalo lote lile, kwa kufanya hivyo, anashuka chini ya mwamba huu wa Uprotestanti, anavuka mstari unaotenganisha Uprotestanti na Upapa, wala hawezi kutoa sababu yo yote iliyo halali kwa nini asingepokea mafundisho yote ya mwanzo pamoja na kawaida za ibada za Uroma kwa mamlaka ile ile." ----- Toleo la Kumi na tatu, Uk. 67,68.

Katika nuru ya kanuni hii kuu na ya kweli tunayaelekeza mawazo yetu kwenye desturi ile ya Waprotestanti ya kuiadhimisha siku ya kwanza ya juma [Jumapili] badala ya Sabato ya kweli ya Mungu, ambayo ni siku ya saba [Jumamosi]. Mambo haya yanawezaje kusuluhishwa?

## AMRI KUMI HAZIJAFUTWA

Kuna waalimu wengine wa dini siku hizi wanaodai kwamba sheria ile ya Amri Kumi imebatilishwa, imefutwa, imewekwa kando, imesulibishwa msalabani pamoja na Kristo, na ya kwamba, kwa hiyo hakuna Mkristo ye yote anayewajibika kuitunza Sabato hiyo. Hata imani ya dhehebu lao wenyewe haitaweza kuwathibitisha katika madai kama hayo, bila kusema kitu juu ya mafundisho dhahiri ya Maandiko Matakatifu. Mafundisho ya kawaida ya madhehebu mbalimbali za Kiprotestanti kuhusu umilele wa sheria ya Mungu yameandikwa kwa matamko yaliyo wazi katika vitabu vyao vya kanuni, maadili, maungamo ya imani, na katika maneno ya viongozi wao wanaowatambua. Hakuna hata kimojawapo kati ya hivyo, kwa kadiri tulivyo na kumbukumbu zao, kinachotoa msimamo unaosema kwamba Sheria ya Mungu imewekwa kando na haiwafungi tena wanadamu. Naam, ushuhuda wake [vitabu] wa pamoja ni kinyume chake kabisa.

Katika makanisa yote mawili, Kanisa la Uingereza (Church of England) na kanisa la 'Protestant Episcopal Church' lililoko Marekani (U.S.A.), ni kawaida kwa mchungaji anapoendesha huduma ya Meza ya Bwana kuzisoma mbele ya watu zile Amri Kumi, na mwisho wa kila amri watu husema, "Bwana uturehemu na kuielekeza mioyo yetu kuishika amri hii." Hakika matawi haya ya Uprotestanti hayafundishi kwamba Amri Kumi zimewekwa kando.

## SHERIA NI "YA MILELE NA HAIBADILIKI"

Mafundisho ya kawaida ya dhehebu la Kibaptisti yameandikwa katika kitabu cha 'NEW HAMPSHIRE CONFESSION OF FAITH,' na kusema kweli hakuna mafundisho yo yote ndani yake yanayofundisha kufutwa, au hata kuibadili sheria ya Mungu katika usemi wenye nguvu ufuatao:

"Tunasadiki Maandiko yanafundisha kwamba sheria ya Mungu ni kanuni ya milele na isiyobadilika ya serikali Yake takatifu; kwamba [sheria] ni takatifu, ya haki, na njema; na kwamba kule kutokuwezekana kuyatimiza maagizo yake ambako Maandiko yanawahesabia wanadamu walioanguka [dhambini] kunatokana kabisa na wao wenyewe kuipenda dhambi; kuwakomboa kutokana nayo [dhambi], na kuwarejeza kupitia kwa Mpatanishi hadi kufikia utii wa kweli kwa sheria Yake takatifu, hilo ndilo hitimisho mojawapo kuu la Injili, na la ile njia ya neema ambayo imehusishwa na uanzishaji wa kanisa lake linaloonekana." ----- Article l2, quoted in O. C. S. WALLACE, WHAT BAPTISTS BELIEVE (1934), uk. 79.

## KUIKATAA SHERIA NI KUIPINDUA INJILI

Kwamba, kwa sababu Wakristo wanayo nuru kubwa, wanao wajibu mkubwa zaidi kuyatii maagizo yote ya sheria hii kuliko watu wengine wo wote, jambo hilo limesisitizwa katika kijizuu Na. 64 cha 'Baptist Publication Society' ambacho kinatangaza hivi:

"Kuthibitisha kwamba amri kumi zinawafunga watu, hebu mtu awaye yote azisome, moja moja, na kuiuliza dhamiri yake mwenyewe anapoendelea kuzisoma, kama ingekuwa dhambi kuzivunja. Je, hizo [amri kumi] au sehemu yake yo yote, sio uhuru wa injili? Kila dhamiri ambayo haijaungua kwa kuchomwa moto kwa chuma cha moto haina budi kuyajibu maswali hayo kwa kukana... Mtoa sheria na Mwokozi wetu ni yule yule mmoja; na waumini hawana budi kuafikiana na yule wa kwanza kama wanavyopaswa kwa yule wa pili; lakini kama tunaidhalilisha sheria ambayo Kristo alipendezwa kuiheshimu, na kukana uwajibikaji wetu katika kuitii, je, tunawezaje kuwa na nia Yake? Je, hatuna nia ile iliyo na uadui zaidi juu ya Mungu, ambayo haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii?... Kama sheria sio kanuni ya mwenendo wa waumini, na kanuni iliyo kamilifu pia, basi, wao hawako chini ya kanuni yo yote; au sivyo, jambo ambalo ni lile lile moja, yaani, wao ni waasi [wavunja sheria]. Lakini kama hivyo ndivyo ilivyo, basi, hawafanyi dhambi; maana PASIPOKUWAPO SHERIA, HAPANA KOSA; basi, katika suala kama hilo, hawana dhambi zo zote za kuungama, ama kwa Mungu, ama wao kwa wao; wala hawana haja yo yote na Yesu kama Mwombezi wao kwa Baba, wala hawahitaji msamaha wa kila siku kwa njia ya damu Yake. Hivyo ndivyo ilivyo, kwa kuikataa sheria, wanadamu wanaipindua [wanaiharibu] injili kabisa. Kwa hiyo, badala ya waumini kuwekwa huru mbali na wajibu wao wa kuitii, wako chini ya uwajibikaji mkubwa zaidi kufanya hivyo [kuitii] kuliko wanadamu wengine ulimwenguni. Kusamehewa wajibu huo ni kuishi pasipo sheria, na, kusema kweli, ni kuishi bila dhambi; katika hali kama

hiyo TUSINGEKUWA NA HAJA YO YOTE NA MWOKOZI, jambo ambalo ni MAPINDUZI kabisa ya dini yote." ----- Ukurasa 2-6.

NEEMA NA UPATANISHO WAKE KRISTO HUBATILISHWA NA WENYE IMANI INAYOIKATAA SHERIA YA MUNGU (ANTINOMIANISM)

Reverend Andrew Fuller, mchungaji mashuhuri wa Kibaptisti aliyejulikana kama "Franklin wa thiolojia," asema hivi:

"Kama fundisho la upatanisho wake Kristo linatuongoza sisi kuwa na mawazo ya kuidhalilisha sheria ya Mungu, au kudai kuwa tumesamehewa kutokana na mamlaka ya amri zake, basi, tuwe na hakika kwamba hilo silo fundisho la Biblia la Upatanisho. Upatanisho unaheshimu haki, na haki inaheshimu sheria, au mapenzi yaliyofunuliwa ya Mungu Mwenyezi, ambayo yamevunjwa; na kusudi hasa la upatanisho ni kurudisha heshima ya sheria. Kama sheria iliyovunjwa ilikuwa haina haki, basi, badala ya upatanisho kuhitajika kwa ajili ya kuivunja, ingestahili kubatilishwa [kufutwa], na Mtoa Sheria naye angepaswa kubeba aibu Yeye Mwenyewe kwa kuiamuru [sheria hiyo].... Ni rahisi kuona kuanzia hapo, kwamba kwa kiwango kile kile sheria hiyo inavyodhalilishwa, ndivyo injili nayo inavyodhoofishwa, na neema pamoja na upatanisho, vyote viwili, hubatilika. Ni sheria iliyotumiwa vibaya, au iliyogeuzwa katika mtindo wa maisha unaopingana na injili, ambao kamwe haukutolewa kwa kiumbe kilichoanguka dhambini, hiyo ndiyo Maandiko Matakatifu huidhalilisha; na sio kama yalivyo yale mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa, kanuni ile ya mema na mabaya isiyobadilika. Kwa mtazamo huu Mitume waliifurahia [sheria]; na kama sisi ni Wakristo, tutaifurahia pia, nasi hatutakataa kuwa chini yake [sheria] kama kanuni yetu ya uwajibikaji; maana hakuna mtu ye yote anayepinga kutawaliwa na sheria zile anazozipenda." ----- "Atonement of Christ," in WORKS OF ANDREW FULLER, uk. l60,l6l

UKAMILIFU USIOKUWA NA KIFANI NI UTHIBITISHO WA UTAKATIFU WA SHERIA HIYO

Charles Spurgeon, mkuu wa wahubiri wa Kibaptisti, katika kitabu chake cha 'PERPETUITY OF THE LAW OF GOD,' asema hivi:

"Yesu hakuja kuitangua sheria, bali alikuja kuifafanua, na ukweli huo unaonyesha hasa kuwa inaendelea kuwako; maana hakuna haja yo yote ya kueleza kile ambacho kimefutwa.... Kwamba Bwana hakuja kuibadili sheria ni dhahiri, kwa sababu baada ya kuitumia katika maisha Yake Mwenyewe, alijitoa Mwenyewe kwa hiari kulipa adhabu yake, ingawa Yeye alikuwa hajapata kuivunja kamwe, alibeba adhabu yake kwa ajili yetu sisi, kama ilivyoandikwa, 'Kristo alitukomboa katika laana ya torati [sheria], kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu'.... Kama sheria ingekuwa imetudai sisi zaidi ya kile ilichopaswa kudai, je, Bwana Yesu angelipa adhabu ile iliyotokana na masharti yake makali mno? Nina hakika asingeweza. Walakini, kwa kuwa sheria iliomba kile tu ilichostahili kuomba, yaani, UTII MKAMILIFU, na kumdai

mvunja sheria alipe kile tu ambacho ingestahili kumdai, yaani, MAUTI kama mshahara [malipo] wa dhambi ----- mauti chini ya ghadhabu ya Mungu ----- kwa hiyo Mwokozi aliangikwa mtini, na kuzichukua dhambi zetu, na kuzisafisha zote." ----- Ukurasa 4-7.

Tena, katika kitabu chake cha 'SERMONS,' Spurgeon asema:

"Sheria ya Mungu ni sheria tukufu, takatifu, ya mbinguni, kamilifu.... Hakuna amri iliyovuka mpaka wake, hakuna moja iliyopunguka mno; lakini HAILINGANISHWI NA CHO CHOTE hata UKAMILIFU wake umekuwa ushahidi wa utakatifu wake. Hakuna mtoa sheria wa kibinadamu ye yote ambaye angeweza kutoa sheria kama hiyo tunayoikuta katika Amri Kumi." ----- Vol.II, Sermon l8, uk.280.

## UMETHODISTI UNAITETEA SHERIA

Tunageukia sasa kwenye mafundisho ya kawaida ya Kanisa la 'Methodist Episcopal Church,' tunalikuta kundi lile kubwa la Wakristo wakitetea wajibu wa kuitii sheria ya Mungu:

"Japokuwa sheria ile iliyotoka kwa Mungu kwenda kwa Musa iligusa kawaida za ibada ya dhabihu [kafara] pamoja na taratibu zake za dini haiwafungi Wakristo, wala zile sheria za utawala hazina umuhimu wo wote kupokelewa katika jamii yo yote inayojitawala; hata hivyo, hakuna Mkristo ye yote aliye huru mbali na utii kwa amri zile zinazoitwa za maadili." ----- Constitution of the Methodist Episcopal Church, "Articles of Religion," Art. 6, in METHODIST EPISCOPAL CHURCH DOCTRINES AND DISCIPLINE (l928), uk.7.

Baba wa Umethodisti, John Wesley, alikuwa na mengi ya kusema kuhusu sheria ya Mungu, na wajibu uwapasao Wakristo katika kuitii. Aliitetea kwa nguvu dhidi ya wale waliofundisha kwamba imefutwa. Tunayaelekeza mawazo yenu hasa kwenye usemi ufuatao, wote ukiwa umechukuliwa katika maandiko yake:

"Sheria ya Maadili iliyo katika Amri Kumi, ambayo manabii waliwagiza watu kuitii, Yeye [Kristo] hakuiondolea mbali. Halikuwa kusudi la kuja kwake kutangua sehemu yo yote ya [sheria] hiyo. Hii ndiyo sheria isiyoweza kuvunjwa kamwe, ambayo 'inasimama imara kama shahidi mwaminifu mbinguni.' Sheria hii ya maadili inasimama juu ya msingi tofauti kabisa na sheria ya kafara [dhabihu] au sheria ya taratibu za ibada.... Kila sehemu ya sheria hii haina budi kuendelea kuwa na nguvu juu ya wanadamu wote, na katika vizazi vyote; haitegemei wakati au mahali, au jambo jingine lo lote ambalo linaweza kubadilika, bali [inategemea] tabia ya Mungu na tabia ya mwanadamu, na uhusiano wao usiobadilika kwa kila mmoja." ----- On the Sermon on the Mount," Discourse 6, SERMONS ON SEVERAL OCCASIONS (l8l0), Uk.75, 76.

## WESLEY AKIONGEA JUU YA UMILELE WA SHERIA

Kutoka katika hubiri lile lile tunachukua maneno haya:

"Katika safu za juu kabisa za maadui wa injili yake Kristo ni wale ambao, mbele ya watu na kwa waziwazi, 'wanaihukumu sheria' yenyewe, na 'kunena mabaya juu ya sheria'; ambao wanawafundisha watu kuvunja (LUSAI, KUTANGUA, KULEGEZA, KUFUNGUA UWAJIBIKAJI WA) sio tu moja, iwe ndogo sana, au iwe kubwa sana, bali amri zote kwa pigo moja; ambao hufundisha, pasipo kujificha, kwa maneno mengi, wakisema, 'Bwana wetu alifanya nini na sheria? Aliifutilia mbali. Kuna wajibu mmoja tu, ule wa kuamini....' Kweli huko ni kuyaendesha mambo kwa ujeuri; huko ni kumpinga Bwana wetu ana kwa ana, na kumwambia kwamba Yeye hakujua jinsi ya kuutoa ujumbe ule aliotumwa kuupeleka. Ee Bwana, usiwahesabie dhambi hii! Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo!

"Jambo la kushangaza kuliko yote, linaloambatana na udanganyifu huu mkuu ni kwamba wale waliochukuliwa nao wanasadiki kweli kwamba wao wanamheshimu Kristo kwa kuitupa chini sheria Yake, na kwamba wanaitukuza kazi Yake, wakati wanaliharibu fundisho Lake! Naam, wanamheshimu kama vile alivyofanya Yuda, aliposema, 'Rabi, akambusu.' Naye [Kristo] anaweza kusema na kila mmoja wao, 'Wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu?' Si kitu kingine ila ni kumsaliti kwa kumbusu, kuzungumza juu ya damu Yake; kwa kuihafifisha sehemu yo yote ya sheria Yake, na kujifanya kuwa wanaiendeleza injili Yake. Wala kwa kweli haiwezekani kwa ye yote kuikwepa lawama hii, hasa yule anayeihubiri imani kwa njia kama hii, aidha moja kwa moja au kwa kuzunguka kwa kuiweka kando sehemu yo yote inayohusiana na utii; yule anayemhubiri Kristo kwa namna ambayo anaibatilisha, au anaidhoofisha [sheria] kwa njia yo yote ile, hata kama ni amri moja ya Mungu iliyo ndogo sana." ----- Kitabu kile kile (ibid.), Uk. 8l,82.

## INJILI HAINA MAANA YO YOTE ISIPOJENGWA JUU YA SHERIA

Askofu Matthew Simpson, wa Kanisa la 'Methodist Episcopal Church,' alitoa hotuba za Chuo cha Yale juu ya Mahubiri katika mwaka wa l878, ambazo hatimaye zilichapishwa na 'Eton and Mains' chini ya kichwa cha 'LECTURES ON PREACHING.' Katika hobuba yake ya nne Askofu Simpson alisema:

"Sheria ya Mungu... lazima ionyeshwe waziwazi. Mikusanyiko ya waumini wetu na ikusanywe kana kwamba iko chini ya Mlima Sinai, wakati sauti ya Mungu inasikika toka kileleni ikizitangaza amri zile ambazo hazibadiliki na za milele kwa tabia yake.... Kuna wahubiri wengi wanaopenda kuongea juu ya injili peke yake.... Lakini wakati mwingine wanavuka mpaka huo, na kupinga kwa sauti kuu mahubiri yale yanayogusa sheria ----- wakisema kwamba hiyo [sheria] inahusu kizazi kilichopita, yaani, watu wale waliostaarabika kidogo tu; na ya kwamba watu wanaweza kuguswa kwa [kuhubiri] upendo peke yake.... Injili kama hiyo yaweza kujenga jengo zuri; lakini msingi wake umejengwa juu ya mchanga. Hakuna jengo lo lote la kweli linaloweza kujengwa bila msingi wake kuchimbwa kwa kina kwa njia ya toba kwa Mungu.... Sheria pasipo injili ni giza tupu na haileti matumaini yo yote; injili pasipo sheria haifai kitu wala haina nguvu yo yote. Moja inatuongoza kwenye utumwa, ile nyingine kwenye imani inayoikataa kabisa sheria ya Mungu (antinomianism). Zote mbili

zikijumuishwa pamoja [Sheria na Injili] zinazaa 'upendo utokao katika moyo safi, na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki.'" ----- Ukurasa l28,l29.

## SHERIA HAIWEZI KAMWE KUWA KUUKUU

Katika KATEKESIMO, Nambari 1 na 2, ya Kanisa la 'Methodist Episcopal', kuna mafundisho haya:

"SWALI. ----- Mungu anataka nini kwa mwanadamu?

"JIBU. ----- Utii kwa mapenzi Yake yaliyofunuliwa.

"SWALI. ----- Kanuni ya utii wetu ni ipi?

"JIBU. ----- Ni Sheria ile ya Maadili.

"SWALI. ----- Sheria hii ya Maadili imetolewa wapi?

"JIBU. ----- Katika zile Amri Kumi.

"SWALI. ----- Je, Wakristo wote wanawajibika kuitii Sheria hiyo?

"JIBU. ----- Ndio."

----- Number 2, Uk.38,43; Number 1, Uk.l8.

Askofu E.O.Haven, pia wa Kanisa la 'Methodist Episcopal', aliyepata kuwa rais wakati mmoja wa Chuo cha Michigan, alisema:

"Amri hizi Kumi haziwezi kuwa kuukuu. Zilikusudiwa kwa wanadamu wote, nazo, kama zikitiiwa, zinaweza kuwafanya wanadamu wote kuwa na utukufu na kufaa kwa mibaraka ile ya milele. Ni kielelezo [Amri Kumi] cha kujiweka wakf kwa mafundisho ya maadili yaliyo katika Biblia." ----- PILLARS OF TRUTH, uk.235.

## KRISTO ALIUIMARISHA UWAJIBIKAJI WETU KWA KUISHIKA SHERIA MWENYEWE

Dhehebu la Presbyterian haliko nyuma hata kidogo kwa mengine hayo katika utii kwa zile Amri Kumi za Mungu. Sura ya V ya MAUNGAMO YA IMANI ya Kanisa la Presbyterian hutangaza kwa nguvu hivi:

"Sheria ya Maadili inawafunga wote milele, wakiwamo wale waliohesabiwa haki sawasawa na wale wengine, na kuwataka waitii; sio tu kuhusu mambo yaliyomo ndani yake [sheria hiyo], bali pia kuhusu mamlaka ya Mungu Muumbaji aliyeitoa. Wala Kristo kwa njia ya injili hautangui [wajibu wetu] kwa namna iwayo yote ile, bali anauimarisha zaidi wajibu huo." ----- Chapter l9, Sec.5, in THE CONSTITUTION OF THE PRESBYTERIAN CHURCH IN THE UNITED STATES OF AMERICA (l896), uk. 88,89.

## NI KANUNI YA MILELE YA MAISHA YA UTAUWA NA UTAKATIFU

Mwanamatengenezo mkuu, John Calvin, akitoa maoni yake juu ya Mathayo 5:17 na Luka 6:17, katika kitabu chake cha 'COMMENTARY ON A HARMONY OF THE GOSPELS', asema:

"Tusifikiri ya kwamba kuja kwake Kristo kumetuweka huru mbali na mamlaka ya Sheria; kwa maana hiyo ni kanuni ya milele ya maisha ya utauwa na utakatifu, na kwa ajili hiyo inapaswa isiweze kubadilika kama ilivyo haki ya Mungu, ambayo imo ndani yake [sheria hiyo], nayo ni ya kudumu na linganifu." ----- Volume I, uk. 277.

Katika kitabu chake cha 'INSTITUTES', Calvin aliandika hivi:

"Sheria haikupata athari yo yote ya kupunguziwa mamlaka yake, bali inapaswa sikuzote kupokea kutoka kwetu HESHIMA ile ile na UTII." ----- ii.7, sec.15.

## YESU HAKUZIFUTA WALA KUZITANGUA AMRI KUMI

Dkt. Albert Barnes, mfafanuzi mwenye kusifika wa Kanisa la Presbyterian, katika maoni yake juu ya Mathayo 5:l8, asema hivi:

"Sheria za Wayahudi kwa kawaida zimegawanyika katika Maadili, Kafara [Dhabihu], na Hukumu. Sheria za Maadili (Moral Laws) ni kama zile zinazotokana na MAUMBILE YA VITU, ambazo, kwa sababu hiyo, haziwezi kubadilishwa ----- kama vile wajibu wetu wa kumpenda Mungu na viumbe vyake. Hizo [Sheria za Maadili] haziwezi kufutwa, kwa vile haiwezi kuwa sawa kwetu sisi KUMCHUKIA Mungu, ama KUWACHUKIA wanadamu wenzetu [Mathayo 22:34-40]. Katika kundi hili [la sheria] zimo zile AMRI KUMI; naye Bwana wetu alisema kwamba [amri] hizo hajazifuta wala kuzitangua [kwa kuweka kitu kingine mahali pake]." ----- NOTES, EXPLANATORY AND PRACTICAL, ON THE GOSPELS (l860 ed.), Vol. I, uk. 65.

Akitoa maoni yake juu ya Mathayo 5:l9, mwandishi yule yule asema hivi:

"Hapa tunajifunza: 1. Kwamba sheria yote ya Mungu [Amri Kumi] inawafunga Wakristo. Linganisha na Yakobo 2:l0. 2. Kwamba amri zote [kumi] za Mungu zingepaswa kuhubiriwa

na Wachungaji Wakristo kwa mahali pake. 3. Kwamba wale wanaojifanya kuwa hawana haja ya kuzitii amri zo zote wanazosema ni ndogo sana, hao hawafai kuingia katika ufalme Wake. Na jambo la 4. Kwamba uchaji Mungu wa kweli unaziheshimu amri ZOTE [kumi] za Mungu. Linganisha na Zaburi 119:6,[5]." ----- kkk [Kitabu kile kile], Uk.66.

Timothy Dwight wa Kanisa la 'Congregationalists', anatangaza hivi:

"Sheria ya Mungu [Amri Kumi] kwa umuhimu wake ni lazima iwe haibadiliki na ya milele." ----- THEOLOGY, Vol. IV, uk. l20.

Jonathan Edwards, mhubiri mkuu wa Kanisa la 'Congregationalists', ambaye wakati mmoja alikuwa rais wa Chuo cha Princeton, katika kitabu chake cha 'THE WORKS OF JONATHAN EDWARDS, anasema:

"Kwa njia ya Upatanisho wake Kristo HESHIMA nyingi zaidi inatolewa kwa Sheria [Amri Kumi], na matokeo yake ni kwamba Sheria hiyo INATHIBITIKA zaidi, kuliko kama Sheria hiyo ingekuwa imetekelezwa kama ilivyo [bila upatanisho], wanadamu wote wangekuwa wamehukumiwa ya kuwa wana hatia. Jambo lo lote linaloelekea kuleta heshima nyingi sana kwa Sheria hiyo, huelekea kuyaimarisha sana MAMLAKA yake." ----- Toleo la 1842, Gombo la II, Uk. 369.

## KRISTO ALIIFANYA SHERIA IPENYE NDANI ZAIDI

Dwight L. Moody, mwanauamsho mkuu, katika kitabu chake cha 'WEIGHED AND WANTING', anatoa semi (statements) hizi:

"Wanadamu hivi sasa wanaweza kubishana wapendavyo juu ya sehemu nyingine za Biblia, lakini mimi sijapata kukutana na mtu ye yote MNYOFU ambaye alizikosoa [alizitoa makosa] AMRI KUMI. Makafiri wanaweza KUMDHIHAKI Mtoa Sheria na kumkataa yule aliyetukomboa sisi katika laana ya Sheria [torati], lakini hawawezi kujizuia kukiri ya kwamba AMRI ZENYEWE NI ZA HAKI. Renan alisema kwamba [Amri] hizo ni kwa ajili ya MATAIFA YOTE, na kwamba zitaendelea kuwa Amri [Kumi] za Mungu katika KARNE ZOTE."

"Watu wanatakiwa KUELEWESHWA ya kwamba Amri Kumi hizo BADO ZINATUFUNGA LEO kama zilivyofanya tangu zilipotangazwa katika usikivu wa watu wale [pale Sinai]. Wayahudi wenyewe walisema kwamba Sheria hiyo haikutolewa kule Palestina (ambayo ilikuwa ni nchi yao Israeli), bali katika JANGWA, kwa sababu Sheria hiyo ilikuwa kwa ajili ya MATAIFA YOTE."

"Kamwe Yesu hakupata KUIHUKUMU Sheria hiyo wala Manabii, bali ALIWAHUKUMU wale ambao HAWAKUMTII. Kwa kuwa alitoa amri mpya, haifuati kwamba alizifuta zile za zamani. Maelezo yake Kristo juu yake [amri hizo] yalizifanya zote ziweze kupenya ndani zaidi." ----- Kurasa 11,16,15.

## INATUMIKA ULIMWENGUNI KOTE

Msimamo wa Kanisa la Kilutheri unaweza kuelezwa kwa maneno ya mojawapo ya Katekesimo zake za siku hizi:

"23. PALIKUWA NA SHERIA NGAPI ALIZOZITOA MUNGU KATIKA AGANO LA KALE?

"Aina tatu: 1. Sheria ya kanisa ya Kafara [dhabihu] (The Ceremonial Church Law); 2. Sheria ya Serikali (The Civil Law); 3. Sheria ya Maadili (The Moral Law).

"24. NI IPI KATI YA SHERIA HIZI TATU AMBAYO BADO INA NGUVU?

"Ni Sheria ya Maadili, ambayo imo katika AMRI KUMI.

"25. JE, SHERIA HII HAIWEZI KUFUTWA?

"LA; kwa sababu imejengwa juu ya TABIA YAKE MUNGU takatifu na ya haki."

----- EPITOME OF PONTOPPIDAN'S "EXPLANATION OF MARTIN LUTHER'S SMALL CATECHISM" (1935), Uk. 6,7.

Katika kitabu chake cha "Against the Antinomians", Luther anasema hivi:

"Nashangaa mno jinsi ilivyotokea kunihesabu mimi kuwa ningeikataa Sheria ile ya Amri Kumi.... Je, kuna mtu ye yote anayeweza kufikiri kwamba dhambi inaweza kuhesabiwa pasipokuwapo Sheria? Ye yote anayeitangua Sheria, itampasa pia kwa umuhimu uo huo kuitangua dhambi pia." ----- Translated from LUTHER'S WORKS (Weimar ed.), Vol. 50, Uk. 470,47l.

Katika kitabu cha M. Michelet cha 'LIFE OF LUTHER' ananukuliwa akisema:

"Ye yote anayeliharibu fundisho la Sheria, anaharibu utaratibu wa serikali na jamii kwa wakati uo huo. Kama ukiitupa Sheria [Amri Kumi] nje ya kanisa, hapatakuwa na dhambi tena itakayotambulikana hivyo ulimwenguni kote; kwa maana Injili inafafanua tu na kuiadhibu dhambi kwa KUIHUSISHA NA SHERIA hiyo." ----- v.4, Hazlitt's tr. (2nd ed.), Uk.315.

Msimamo wa Kanisa la 'Free Methodist Church' unaweza kuonekana katika kitabu chao cha 'FREE METHODIST DISCIPLINE', ambacho kinasomeka hivi:

"Hakuna Mkristo awaye yote aliye huru mbali na UTII WA AMRI zile zinazoitwa ZA MAADILI."

Alexander Campbell anaweza kuchukuliwa kama ndiye mnenaji wa Kanisa la 'Christian Church.' Katika mahojiano yake na Purcell alisema:

"MANENO KUMI ya Mungu,... sio tu katika Agano la Kale, bali katika ufunuo [Maandiko] wote, yanaangaliwa kwa mkazo sana kama ndio muhtasari wa dini yote na maadili." ----- DEBATE ON THE ROMAN CATHOLIC RELIGION, uk. 214.

Kamusi ya Smith ya Biblia inatangaza hivi:

"Japokuwa hata Amri Kumi zinaathiriwa na Agano Jipya, si kwa njia ile ya kuzitangua au kuzifuta kabisa. ZIMEINULIWA juu, zimebadilishwa na kuwa NZURI ZAIDI, ZIMETUKUZWA humo [katika Agano Jipya], lakini zenyewe zinabaki na MAMLAKA yake pamoja na UKUU wake." ----- Toleo la 1863, Gombo la III, Uk. 1071.

Katika Kamusi ya Thiolojia ya Buck, katika makala yake juu ya "Sheria," kuna maneno haya:

"Sheria ya Maadili [Amri Kumi] ni tangazo la MAPENZI yake Mungu ambayo yanawaongoza na kuwafunga wanadamu WOTE, katika kila kizazi na kila mahali, kuwaonyesha WAJIBU wao Kwake. Ilitangazwa na Mungu Mwenyewe kwa njia ya kutisha sana pale Sinai.... Inaitwa kuwa ni [Sheria] KAMILIFU (Zaburi 19:7), YA MILELE (Mathayo 5:17,18), TAKATIFU (Warumi 7:12), NJEMA (Warumi 7:12), YA ROHONI (Warumi 7:14), PANA MNO (Zaburi 119:96)." ----- Ukurasa 230.

Ukosefu wa nafasi unazuia kuongeza madondoo zaidi kuhusu Sheria [Amri Kumi]. Walakini, [karibu] madhehebu zote za Kiprotestanti zinakubali kwamba Sheria ile ya Amri Kumi za Mungu inapaswa kutiiwa na Wakristo; kwamba hiyo ndicho kipimo cha milele cha haki na HAKIBADILIKI; na ya kwamba WAJIBU wetu wa kuzishika amri zake umeimarishwa zaidi na Kristo badala ya kuupunguza ama kuuondolea mbali kabisa.

Walakini, japokuwa wametoa ukubali wao rasmi na kuiunga mkono Sheria hiyo, washiriki wa madhehebu hizi kwa umoja wanaendelea kuitunza siku ambayo kamwe haijatajwa katika Amri Kumi, nao kwa pamoja wanadharau na kupuuza utunzaji wa siku ile ambayo imeamriwa kwa dhahiri na kuonyeshwa kwa wazi.

## WANAKIRI SABATO INAENDELEA KUWAKO BILA KUBADILISHWA

Je, kule kushindwa kwao kuishi kulingana na madai yao kunatokana na imani yao ya dhati kwamba sehemu ile ya Sheria inayoamuru utunzaji wa siku ya saba imeondolewa mbali, wakati ambapo amri zote [tisa] zilizobaki zinaendelea kuwa na nguvu? La, hasha, maana madhehebu zizi hizi zinakazia sana amri ya nne kama vile zinavyokazia amri zile zilizobaki. Hii inaonekana dhahiri katika maandiko yao wenyewe ambayo yametolewa hapa:

Askofu Mkuu Farrar (Church of England) akiandika juu ya namna utunzaji wa Jumapili ulivyoingia katika kawaida za ibada ya Wakristo, katika kitabu chake cha 'THE VOICE FROM SINAI,' asema hivi:

"Kanisa la Kikristo halikufanya mabadiliko rasmi, bali kwa taratibu (gradual) na bila ya kutambua waliihamisha siku moja kwenda kwa ile nyingine." ----- Ukurasa 167.

Dkt. Peter Heylyn (Church of England), katika kitabu chake cha 'HISTORY OF THE SABBATH,' asema:

"Mchukue ye yote umtakaye, aidha wale Mababa (Fathers) au watu wa siku hizi, wala hatutaipata siku yo yote ya Bwana ikiwekwa kwa mamlaka [amri] ya Mtume ye yote, hakuna Sabato yo yote iliyoanzishwa nao na kuwekwa juu ya siku ya kwanza ya juma." ----- Sehemu ya 2, Sura ya 1, Uk.28.

Askofu Jeremy Taylor, pia wa Kanisa la 'Church of England,' katika kitabu chake cha 'DUCTOR DUBITANTIUM', anaandika hivi:

"Siku ya Bwana [Jumapili] haikuwekwa mahali pa Sabato, bali Sabato iliondolewa kabisa, na Siku ya Bwana [Jumapili] ilikuwa ni siku iliyowekwa na kanisa tu. Haikuletwa kwa sababu ya amri ya nne, kwa sababu kwa karibu miaka mia tatu waliitunza sambamba na siku ile iliyokuwa katika amri [Sabato ya siku ya saba]." "Wakristo wale wa kwanza walifanya kila aina ya kazi katika Siku ya Bwana [Jumapili], hata katika kipindi kile cha mateso, walipokuwa watunzaji wenye bidii wa amri zote za Mungu; lakini katika siku hii [Jumapili] walijua hakuna amri [ya Mungu]." ----- Part 1, ii.2, rule 6, secs. 51,59 (1850 ed.), Vol. IX, uk.458,464.

## KATIKA PUMZIKO LA JUMAPILI HAKUNA AMRI YA MUNGU INAYOINGIA HUMO

Kasisi mwenye kiti Eyton (Church of England), katika kitabu chake cha 'TEN COMMANDMENTS,' asema hivi:

"Hakuna neno lo lote, dokezo lo lote, katika Agano Jipya juu ya kuacha kufanya kazi siku ya Jumapili.... Katika pumziko la Jumapili hakuna amri ya Mungu yo yote inayoingia humo.... Kuadhimisha Jumatano ya Majivu (Ash Wednesday) au Kwaresima (Lent) kunasimama katika hali moja na Utunzaji wa Jumapili." ----- Kurasa 62,63,65.

Reverend Isaac Williams, B.D. (Church of England), katika kitabu chake cha 'PLAIN SERMONS ON THE CATECHISM,' asema:

"Ni wapi katika Maandiko tunapoambiwa kuitunza siku ya kwanza? Tunaamriwa kuitunza siku ya saba; lakini hakuna po pote tunapoamriwa kuitunza siku ya kwanza.... Sababu inayotufanya sisi kuitunza siku ya kwanza ya juma kama siku takatifu badala ya ile siku ya saba ni sababu ile ile inayotufanya tutunze mambo mengi mengine, SI kwa sababu BIBLIA IMEAMURU, BALI kwa sababu KANISA LIMEAMURU." ----- Gombo la I, Uk. 334-336.

William E. Gladstone, Waziri Mkuu kuliko wengine wa Uingereza, pia akitoka katika Kanisa la 'Church of England,' katika kitabu chake cha 'LATER GLEANINGS,' anatoa maneno haya:

"Siku ya saba ya juma imeshushwa chini kutoka katika cheo chake cha kutunzwa kama WAJIBU wa kidini, na mamlaka yake imehamishiwa katika siku ile ya kwanza, bila kuwako amri ya moja kwa moja toka katika Maandiko." ----- Ukurasa 342.

Katika kitabu cha 'MANUAL OF CHRISTIAN DOCTRINE' (Protestant Episcopal), swali hili na jibu lake vinaonekana humo:

"Je, kuna amri yo yote katika Agano Jipya inayoruhusu kubadili siku ya mapumziko ya kila juma toka Jumamosi kwenda Jumapili? ----- HAKUNA." ----- Ukurasa 127.

## HAKUNA USHAHIDI WA MAANDIKO KWA BADILIKO HILO

Katika Konferensi [mkutano mkuu] ya Wachungaji iliyofanyika katika mji wa New York, tarehe 13 Novemba, 1893, Dkt. Edward T. Hiscox, mwandishi wa kitabu cha 'THE BAPTIST MANUAL,' alisoma karatasi lenye mada ya kuihamisha Sabato toka siku ya saba kwenda siku ya kwanza. Tangazo la karatasi hilo lilitolewa katika toleo la 'New York EXAMINER,' gazeti la Kibaptisti la tarehe l6 Novemba, l893, ambalo lilieleza habari ya ari kubwa walioionyesha wachungaji wale waliokuwapo, na mjadala uliofuata baada ya kuisoma. Kutokana na nakala yenye anwani hii, iliyotolewa na Dkt. Hiscox mwenyewe, tunayaelekeza mawazo yenu kwenye semi hizi za kushangaza na zilizotolewa kwa nguvu:

"Ilikuwako na bado ipo amri ya kuitakasa siku ya Sabato, walakini siku ile ya Sabato haikuwa Jumapili. Basi, itasemwa hivi, na kwa kushangilia kidogo, kwamba Sabato ilihamishwa toka siku ya saba kwenda siku ya kwanza ya juma, pamoja na wajibu wake wote, haki zake, na makatazo yake. Kwa dhati tukitamani kupata maelezo juu ya suala hili, ambalo mimi nimejifunza kwa miaka mingi, nauliza, Ni wapi kumbukumbu ya kitendo kama hicho inaweza kupatikana? Sio katika Agano Jipya, sio kabisa. Hakuna ushahidi wo wote wa Maandiko kuhusu badiliko la Sabato iliyowekwa katika siku ile ya saba kuhamishwa na kwenda katika siku ya kwanza ya juma.

"Napenda kusema ya kwamba hoja hii ya Sabato, kwa mtazamo huu, ni hoja nzito sana na inayotatanisha mno kuhusu mambo ya Kikristo yaliyowekwa ambayo hivi sasa yanavuta mawazo ya Wakristo; na sababu ya pekee ambayo inafanya lisiwe jambo linaloleta utata sana katika fikira za Kikristo na katika mijadala ya kidini, ni kwa sababu ulimwengu wa Kikristo umetulia na kuridhika kwa kusadiki kwamba kwa namna fulani uhamisho huo umetokea mwanzo wa historia ya Kikristo...

"Kwangu inaonekana kwamba ni jambo la ajabu lisiloelezeka ya kwamba Yesu, katika miaka ile mitatu ya kuongea na wanafunzi wake, akiongea nao mara nyingi juu ya Sabato, akilizungumzia suala hili katika baadhi ya mapana na marefu yake mbalimbali, akiiweka [Sabato] huru mbali na makosa makubwa ya uongo, kamwe hakutaja pamoja na mambo mengine uhamisho wo wote wa siku hii; pia, katika kipindi kile cha siku arobaini baada ya ufufuo wake, hakugusia kitu kama hicho. Wala, kwa kadiri tujuavyo, yule Roho, aliyetolewa kuwakumbusha mambo yote aliyowaambia, hakulishughulikia suala hili. Wala hata wale

Mitume waliovuviwa, walipokuwa wanahubiri injili, wakianzisha makanisa, wakiwashauri na kuwafundisha waliokuwamo katika makanisa hayo, hawakujadili au kuligusia suala hili.

"Ni kweli, mimi nami najua vizuri sana kwamba Jumapili ilianza kutumika katika historia ya Kikristo ya mapema [mwanzoni] kama siku ya dini, kama tunavyojifunza toka kwa Mababa Wakristo na vyanzo vingine. Lakini, basi, ni jambo la kusikitisha jinsi gani ya kwamba [Jumapili] inakuja kwetu ikiwa imetiwa alama ya kipagani, na kubatizwa kwa jina la mungu jua, hapo ilipochaguliwa na kuidhinishwa na ule UASI wa kipapa, na kurithishwa kama urithi mtakatifu kwa Uprotestanti!"

## NI ROHO ASIYETOKA KATIKA INJILI

Dkt. H. Gunkel (Lutheran), katika kitabu chake cha 'ZUM RELIGIONSGESCH. VERSTAENDNIS DES N.T.,' asema hivi:

"Kuipokea Jumapili kwa Wakristo wale wa kwanza, kwa akili zangu, ni dalili muhimu mno ya kuonyesha kwamba kanisa lile la kwanza lilikuwa limeongozwa na roho asiyetoka katika injili, wala katika Agano la Kale, bali katika mfumo ule wa dini ulio mbali kabisa naye [Roho]." ----- Ukurasa 76.

Ungamo la Imani la Augsburg (Lutheran) lasema hivi:

"Wao [Wakatoliki] wanadai kufanya badiliko la Sabato kwenda Siku ya Bwana [Jumapili], kinyume na Amri Kumi, kama inavyoonekana; nao hawana mfano unaotajwa sana vinywani mwao kuliko badiliko hilo la Sabato. Wanasema uwezo wa kanisa lao bila shaka ni mkubwa sana, kwa sababu limeiondoa amri katika Sheria ile [ya amri kumi]." ----- PHILIP SCHAFF, CREEDS OF CHRISTENDOM (4th ed.), Vol. III, uk.64.

Katika kitabu cha Binney cha 'THEOLOGICAL COMPEND IMPROVED' (Methodist Episcopal), semi hizi zinatokea:

"Ni kweli kwamba hakuna amri ya dhahiri kuwabatiza watoto wachanga.... Wala hakuna amri yo yote ya kuitakasa siku ya kwanza ya juma." ----- Toleo la 1902, Uk. l80,l8l.

## HAKUNA AMRI KATIKA AGANO JIPYA KUHUSU SIKU YA KWANZA

Kamusi ya Thiolojia iliyoandikwa na Charles Buck (English Independent), yasema hivi:

"Katika lugha ya Kiebrania Sabato huashiria pumziko, nalo ni lile la siku ya saba ya juma,... nasi hatuna budi kukiri ya kwamba hakuna amri yo yote katika Agano Jipya kuhusu siku hii ya kwanza." ----- Ukurasa 403, makala "Sabato."

Katika 'BISHOP'S PASTORAL' (Methodist Episcopal) ya l874 lugha hii inatokea:

"Sabato iliyowekwa tangu mwanzo, na kuthibitishwa tena na tena na Musa pamoja na Manabii, kamwe haijaondolewa. Ni sehemu ya Sheria ya Maadili, ambayo, wala yodi moja, wala nukta moja ya utakatifu wake, haitaondoka."

Askofu E.O. Haven (Methodist Episcopal), katika kitabu chake cha 'PILLARS OF TRUTH,' asema:

"Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu; sio kwa ajili ya Waebrania, bali kwa ajili ya wanadamu wote." ----- Ukurasa 88.

Katika kitabu cha 'THE WORKS OF PRESIDENT EDWARDS' (Congregationalist) kuna semi hizi juu ya Sabato:

"Hoja ya ziada juu ya umilele wa Sabato tunayo katika Mathayo 24:20, 'Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya Sabato.' Hapa Kristo anazungumza juu ya kukimbia kwa wale Mitume pamoja na Wakristo wengine kutoka Yerusalemu na Yudea, kabla tu ya maangamizi yao ya mwisho, kama kifungu hicho chote kinavyodhihirisha, hasa fungu lile la l6: 'Ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani.' Lakini maangamizi ya mwisho ya Yerusalemu yalikuwa baada ya kutanguka kwa Katiba ya Wayahudi, na baada ya kipindi cha Kikristo (Christian dispensation) kuanzishwa kikamilifu. Lakini inaonekana wazi kwamba maneno hayo ya Bwana yalimaanisha ya kwamba Wakristo wa wakati ule walilazimika nao kuitunza Sabato kwa makini." ----- Reprint of Worcester ed., 1844-1848, Vol. IV, Uk.621,622.

## NI WAJIBU WA ULIMWENGU WOTE AMBAO UNADUMU MILELE

Dkt. Archibald Hodge, katika Kijizuu Na. 175 cha Bodi ya Uchapishaji ya Presbyterian, asema:

"Mungu aliianzisha Sabato wakati ule wa uumbaji wa mwanadamu, akiitenga siku ya saba kwa kusudi hilo, na kuamuru utunzaji wake kuwa ni wajibu wa kimaadili wa ulimwengu wote ambao unadumu milele." ----- Ukurasa 3,4.

Dkt. Thomas Chalmers (Presbyterian) asema hivi:

"Tunaweza kubishana juu ya umilele wa Sabato na mahali pake katika Amri Kumi, ambapo inasimama ikiwa imehifadhiwa sana miongoni mwa maadili ya haki ambayo hayabadiliki na yanadumu milele." ----- SERMONS, Vol. I, uk.51,52.

Kitabu cha Timothy Dwight cha 'THEOLOGY' (Congregationalist) kinasema:

"Sabato ya Kikristo [Jumapili] haimo katika Maandiko, wala haikupata kuitwa Sabato na kanisa lile la kwanza." ----- Sermon 107 (1818 ed.), Vol. IV, uk.49.

Dkt. R.W. Dale (Congregationalist), katika kitabu chake cha 'TEN COMMANDMENTS,' asema hivi:

"Ni dhahiri kwamba, haidhuru kwa ukali au kumcha Mungu kiasi gani tunavyoweza kuitumia Jumapili, hatuitakasi Sabato.... Sabato ilianzishwa katika msingi wa amri dhahiri ya Mungu. Hatuwezi kujitetea kwa kutaja amri kama hiyo kwa uwajibikaji wetu wa kuitunza Jumapili.... Hakuna mstari hata mmoja katika Agano Jipya unaodokeza ya kwamba tunastahili kupata adhabu yo yote kwa kunajisi utakatifu unaodhaniwa tu wa siku hii ya Jumapili." ----- Ukurasa 127-129.

## NI HALI YA KUTAHAYARISHA

Lakini, basi, yatosha kwa madondoo. Itasemwaje juu ya hali hii isiyokuwa ya kawaida ambayo Uprotestanti unajikuta umeingia ndani yake kuhusu suala hili la utunzaji wa Sabato? Hapa ni kanisa la Kristo, lililoitwa kutoka katika Ukatoliki wa Roma katika karne ile ya kumi na sita ili lipate kusimama juu ya "Biblia na Biblia peke yake," likidai kukitii Kitabu chake Mungu, kutii Sabato ya Mungu, kutii kweli yote ya Mungu, lakini wakati uo huo likiwa bado linaendelea kuitunza siku ambayo Biblia haijapata kamwe kuamuru itunzwe, na kuitupilia mbali kabisa siku ile ambayo Biblia inaitangaza kuwa ni takatifu.

Amini usiamini, Kanisa Katoliki la Roma halijashindwa kuiona hali hiyo ya kutahayarisha [kuaibisha] ambayo binti yake aliyejitenga naye [Uprotestanti] amejikuta amejiingiza ndani yake. Pengine hakuna maoni mazuri zaidi yanayoweza kutolewa kuliko maoni ya gazeti rasmi la Kadinali Gibbons, liitwalo 'CATHOLIC MIRROR,' la Septemba 23, 1893:

"Ulimwengu wa Kiprotestanti katika kuzaliwa kwake [Mwanzo wa Matengenezo ya Kanisa ya Karne ya Kumi na Sita] uliikuta Sabato ya Kikristo [Jumapili] imejiimarisha kwa nguvu mno kiasi cha kutokuwapo uwezekano wa kwenda kinyume na kule kuwako kwake; kwa hiyo ikabidi mpangilio huo ukubalike kwa shida, kwa kufanya hivyo ikidokeza ya kwamba Kanisa hili [Katoliki] lina haki ya kubadili siku, kwa zaidi ya miaka mia tatu [l5l7 hadi l893]. Kwa hiyo, Sabato ya Kikristo [Jumapili] mpaka leo hii inakubalika kama mtoto wa Kanisa Katoliki likiwa mke wa Roho Mtakatifu, wala hakuna neno hata moja la kugombeza kutoka kwenye ulimwengu huo wa Kiprotestanti.

"Wala mipaka ya upotofu wake haijafikiwa bado. Mbali na huo. Kule kujifanya kwao kuwa wanakiacha kifua cha Kanisa Katoliki kulitokana na sababu ya UASI [wa Kanisa Katoliki] kutoka katika kweli kama inavyofundishwa katika Neno. Walilitumia Neno lililoandikwa kama mwalimu wao wa pekee, jambo ambalo wao walikuwa bado hawajaanza kulifanyia kazi mara walipoliacha kwa ghafula.... na kwa upotofu ulio wa makusudi kama vile ulivyo wa makosa, wanakubaliana na fundisho hili la Kanisa Katoliki wakiwa wanapingana moja kwa moja na mafundisho dhahiri, yasiyogeuka, na manyofu ya mwalimu wao wa pekee [Biblia] katika fundisho hili muhimu sana la dini yao, kwa njia hiyo wanaikuza hali yao waliyo nayo ambayo

wanaweza kuitwa vema ya kuwa wamo katika hali ya 'dhihaka, udanganyifu, na mtego.' ----- Reprinted by the Catholic Mirror as a pamphlet, THE CHRISTIAN SABBATH, uk.31,32.

Ni kweli haiwezekani kwa yule anayeitunza Jumapili, ambaye hawezi kutaja idhini ya Maandiko kwa kuidharau kwake Sabato ya kale na kwa kuiheshimu kwake Jumapili, kuweza kuyajibu madai haya ya Kanisa Katoliki. Lakini MPROTESTANTI WA KWELI [anayefuata Biblia, na Biblia peke yake] haoni ugumu wo wote kama huo, maana anakana mara moja na kwa nguvu haki ya kanisa lo lote, haidhuru liwe la zamani jinsi gani, kubadili Sheria ya Mungu [Amri Kumi], naye ANACHUKUA MSIMAMO wake ana kwa ana na BILA_________________________________________________________________ _______________________________________________________ mwao w
alitambua wazi msimamo sahihi ambao wote wangekuwa nao kuihusu KWELI ni dhahiri ukiziangalia semi zilizomo katika hot__________________________________________________________________ _____________________________________________________ ibada kama zile za Roma]. Hao walitamani kwa dhati kurudi katika mfumo wa ibada rahisi usiokuwa na mapambo na usafi wa kandisho linalosema kwamba Wakristo leo wangepaswa kuitunza Sabato ya siku ya saba sio fundisho jipya. Katika Biblia kuna unabii wa miaka maelfu iliyopita, unabii ambao kila Mkristo angepaswa kuufahamu, unaosema kwamba watu wa Mungu wa kizazi hiki wangekuwa WASABATO [Watunza Sabato].

Petro anaueleza unabii wa Biblia kama "TAA ing'aayo mahali penye giza" (2 Petro l:l9). Unabii huu unatoa mwanga mkubwa sana juu ya hali ya baadaye ya watu wa Mungu. Unamwezesha mwanafunzi wa Biblia kuwa na uzoefu wa kuwaangalia watu wa Mungu kama walivyotabiriwa katika Maandiko.

## WASABATO WA SIKU ZA MWISHO

Unabii wa Agano la Kale unaeleza waziwazi kuwa katika siku zile za mwisho wa historia ya wanadamu wale ambao ni WATIIFU kwa Mungu watakuwa wanashika SABATO ya siku ya saba. Hivyo Isaya akiuona wakati ule wa mwisho katika maono yake aliyopewa kutoka mbinguni, wakati ule ambao "wokovu wangu u karibu kuja, na haki yangu kufunuliwa" (Isaya 56:1), anasema kwa sauti kubwa, "Heri afanyaye haya, na mwanadamu ayashikaye sana; AZISHIKAYE SABATO ASIZIVUNJE, azuiaye mkono wake usifanye uovu wo wote" (fungu la 2).

Baraka hii iliyoahidiwa kwa kuishika Sabato katika siku zile zilizo karibu sana na kuja kwake Kristo haijawekwa kwa ajili ya Wayahudi tu, wala kwa kundi lo lote la watu. "Na WAGENI, walioandamana na BWANA ili wamhudumu, na kulipenda jina la BWANA, kuwa watumishi wake; KILA AISHIKAYE SABATO ASIIVUNJE, na kulishika sana agano langu [Kutoka 3l:l6]; Nitawaleta HAO NAO hata mlima wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala; makafara yao na dhabihu zao zitakubaliwa juu ya madhabahu zangu; kwa maana nyumba yangu itaitwa NYUMBA YA SALA kwa MATAIFA YOTE" (Isaya 56:6,7).

Katika wakati ule wa mwisho, watu watakapokuwa wanangojea marejeo ya Kristo, kutakuwa na ujumbe wa Matengenezo ya Sabato (Sabbath Reform), mwito kwa wale wampendao Kristo ili wajitenge wenyewe na ulimwengu pamoja na wapinzani wote, ili kuitunza Sabato ya kweli ya Bwana na kujitenga na dhambi zote pamoja na uovu [2 Wakorintho 6:l4-l8; Ufunuo l8:4].

## "UWAHUBIRI WATU WANGU KOSA LAO"

Wakati huu tulio nao sasa, wakati wa kumngojea Bwana, Mungu anawaagiza wajumbe Wake:

"PIGA KELELE, usiache, PAZA SAUTI yako kama tarumbeta, UWAHUBIRI watu Wangu KOSA lao, na nyumba ya Yakobo dhambi zao" (Isaya 58:1).

Katika siku za mwisho wale wanaodai kuwa ni watu wake Mungu wanapaswa kuyaelekeza mawazo yao kwenye "KOSA" la wazi ambalo wanalitenda. Mpaka hapo mawazo yao yatakapokuwa yameelekezwa kwenye kitu hicho, hawataweza kabisa kutambua ya kwamba mazoea yao ni mabaya kwa kila hali, kwa maana Mungu anapowaeleza jinsi walivyo anasema, "Walakini wanitafuta kila siku; hupenda kujua njia zangu; kama vile taifa waliotenda haki; wasioacha sheria ya Mungu wao [Amri Kumi], hutaka kwangu amri za haki; hufurahi kumkaribia Mungu" (Isaya 58:2).

Ni katika wakati huu ambapo wale wanaofurahi kumtumikia Mungu, pasipo kujua, WANAVUNJA takwa Lake moja lililo la muhimu, wanapoiacha "sheria ya Mungu wao," hapo ndipo Mungu anapowaita wachungaji Wake ku"piga kelele" na kuwataka "wasiache," "kupaza sauti [zao] kama tarumbeta," ku"wahubiri watu Wangu kosa lao."

## MISINGI YA VIZAZI VINGI

Mungu anasema na watu wake wale wanaofanya kazi ya kupiga kelele, wale wanaoionyesha sheria ile ambayo watu wanaiacha, naye anawaambia: "Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; UTAIINUA MISINGI YA VIZAZI VINGI; nawe utaitwa, MWENYE KUTENGENEZA MAHALI PALIPOBOMOKA; na, MWENYE KUREJEZA NJIA ZA KUKALIA" (Isaya 58:12).

Sheria ambayo watu wa Mungu wameiacha katika siku hizi za mwisho imeonyeshwa wazi katika mafungu haya yafuatayo: "Kama ukigeuza mguu wako USIIHALIFU SABATO, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya BWANA yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika BWANA; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha BWANA kimenena hayo" (Isaya 58:l3,l4).

Kwa hiyo, "sheria" ambayo katika siku za mwisho za historia ya ulimwengu huu watu wa Mungu wataitwa kuirejeza, ni amri ile ya nne ya Sheria ya Mungu ya Amri Kumi, inayoamuru kuitakasa Sabato. Kifungu hiki katika Isaya kinaonyesha wakati ule wale wanaodai kumtumikia Mungu wakatapokuwa WANAIKANYAGA [Sabato] chini ya miguu yao, wakiitumia kwa ajili ya kufanya kazi zao; pasipo kuipa HESHIMA yake inayostahili, lakini huku wakiwa wanaiita [Sabato] "ya Kiyahudi," na kwa njia nyinginezo KUIKASHIFU. Wakati huu Mungu anawataka kuacha kuikanyaga amri hii takatifu aliyoiweka na kuiita TAKATIFU na yenye HESHIMA, sio tu kwa neno litokalo kinywani bali kwa kuyatoa maisha yao yapate kuoshwa kwa damu yake Kristo ili wawe WASABATO wa kweli.

Huu ndio ujumbe wa maana kwa LEO, ujumbe wa kufanya Matengenezo ya Sabato. Bwana aliona mbele hali ambazo zingekuwako katika ulimwengu wa kidini LEO, naye akamvuvia nabii huyu kuandika kama vile alivyoandika.

## WENYE KUTENGENEZA MAHALI PALIPOBOMOKA

Kwa wale wanaoshughulika na kazi hii ya kuhubiri ukweli huu wa suala hili la Sabato kwa ulimwengu katika siku hizi za mwisho, Mungu anasema, "Nawe utaitwa, MWENYE KUTENGENEZA MAHALI PALIPOBOMOKA; na, MWENYE KUREJEZA NJIA ZA KUKALIA." Litakuwa jambo la kupendeza kuchunguza umuhimu wa majina hayo.

Tukirudi nyuma katika kitabu hiki cha Isaya hadi sura ile ya thelathini, tunaukuta unabii umefunuliwa kwamba watu wa Mungu katika siku za mwisho WATAKUWA WAASI, watu ambao hawatataka kuisikia Sheria Yake. Mungu anamwita Isaya ku"andika neno hili katika kibao mbele ya macho yao, [kulichora] katika kitabu ili iwe kwa ajili ya majira yatakayokuja [pambio, "siku za mwisho"], kwa USHUHUDA hata milele. Kwa maana watu hawa ni WATU WAASI, watoto wasemao uongo, watoto WASIOTAKA kuisikia Sheria ya BWANA" (Isaya 30:8,9).

## KUTAKA MANENO LAINI

Katika siku zile za mwisho watu hao ambao ni waasi, ambao hawatataka kuisikia Sheria ya Mungu, wanaonekana katika mafungu yafuatayo wakizungumza na VIONGOZI wao wa DINI, na kusema, "Msitoe unabii wa mambo ya haki, TUAMBIENI MANENO LAINI, hubirini maneno YADANGANYAYO; TOKENI KATIKA NJIA, geukeni MTOKE katika MAPITO; mkomesheni Mtakatifu wa Israeli mbele yetu" (Isaya 30:10,11).

Hapa ni unabii ambao haiwezekani kukosa kuuelewa. Unatabiri dhahiri ya kwamba katika siku zile zilizo karibu sana na kuja mara ya pili kwa Kristo, yaani, "siku za mwisho," kutakuwako na kundi la watu wanaokiri KUMTUMIKIA BWANA, lakini ambao ni WAASI kuhusiana na suala la SHERIA, wanaokataa katakata kuyasikia au kuyatii mafundisho ya

Sheria. Watawaambia wachungaji wao waziwazi kwamba HAWATAKI UKWELI ULIO DHAHIRI, bali wanataka wahubiriwe kutoka kwenye mimbara "MANENO LAINI." Wanawataka viongozi wao wa dini 'wageuke na KUTOKA katika MAPITO,' na ku"TOKA katika NJIA," ili wapate kuhubiri "MANENO YADANGANYAYO."

## MAPITO YA AMRI ZA MUNGU

Kwamba "NJIA" hii ni ipi, na "MAPITO" hayo ni yapi ambayo yanasemwa hapa tunaweza kuona dhahiri endapo tutavichunguza vifungu viwili au vitatu katika Zaburi.

"Heri walio kamili NJIA ZAO, WAENDAO KATIKA SHERIA YA BWANA" (Zaburi 119:1). "Naam, hawatakutenda ubatili, Wamekwenda KATIKA NJIA ZAKE" (fungu la 3). "Uniendeshe KATIKA MAPITO YA MAAGIZO [AMRI] YAKO; Kwa maana nimependezwa nayo" (fungu la 35).

Kwamba ile "NJIA" na "MAPITO" yanayozungumzwa katika unabii uliotolewa na Isaya yanahusu zile AMRI KUMI itakuwa dhahiri zaidi tukikichunguza kifungu hiki kingine: "BWANA asema hivi, Simameni katika NJIA kuu, mkaone, mkaulize habari za MAPITO ya zamani, I wapi NJIA iliyo njema? mkaende katika NJIA hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema, HATUTAKI kwenda katika NJIA hiyo" (Yeremia 6:16).

Kwa sababu watu Wake wanakataa kwenda katika njia iliyo njema, Mungu anasema, "Sikia, Ee nchi; tazama, nitaleta mabaya juu ya watu hawa, naam, matunda ya mawazo yao, kwa sababu hawakuyasikiliza maneno yangu; tena kwa habari ya SHERIA yangu, WAMEIKATAA" (Yeremia 6:19).

Vifungu hivi vinaeleza wazi kwamba mifano iliyotumika ya "MAPITO" na "NJIA" inamaanisha AMRI ZA MUNGU [KUMI], na ya kwamba KWENDA katika NJIA ni KUZISHIKA AMRI [KUMI], na "kugeuka na KUTOKA katika MAPITO" ni KUIKATAA SHERIA ya Mungu na KUTOITII.

## MAHALI PALIPOBOMOKA KATIKA SHERIA

Tukirudia sasa kuuchunguza zaidi unabii huu wa ajabu wa Isaya kuhusu siku zile za mwisho, na kukumbuka kwamba Mungu anatabiri kwamba watu Wake katika siku hizi za mwisho hawatataka kuisikia Sheria Yake, tunaona sasa Mungu anavyoulinganisha UASI huo na MAHALI PALIPOBOMOKA KATIKA UKUTA.

"Basi, UOVU huu utakuwa kama MAHALI PALIPOBOMOKA, palipo tayari kuanguka, patokezapo katika ukuta mrefu, ambapo kuvunjika kwake huja ghafula kwa mara moja" (Isaya 30:13).

Hivyo SHERIA ya Mungu sio tu inafananishwa na MAPITO na NJIA ambamo watu Wake wanapita, bali pia inafananishwa na UKUTA unaomzunguka Mkristo na kuyazuia

mashambulio ya adui wa roho yake. Kadiri mtoto wa Mungu anavyozidi kukaa NDANI YA AMRI KUMI kwa UWEZO WAKE KRISTO, ndivyo atakavyozidi kuwa SALAMA kutokana na adui wake. Sheria ndani ya Kristo ni UKUTA unaomlinda [Mkristo] asiweze kushindwa. Kadiri anavyozidi KUITII anagundua kwamba inakuwa BOMA [NGOME] lake dhidi ya MAJARIBU ya Shetani; lakini ANAPOIVUNJA papo hapo anakuwa amefanya UFA katika BOMA lake linalomlinda, au UKUTA, na adui anaweza kuingia ndani na kumwangamiza.

Katika siku za mwisho Mungu aliona kwamba mahali palipobomoka pangetokea katika [ukuta wa] AMRI Zake. Mojawapo ya amri Zake ingeondolewa katika zile kumi, na kuacha MAHALI PALIPOBOMOKA, au UFA, katika UKUTA [SHERIA] huo. Pia Mungu aliona mbele kwamba VIONGOZI wa dini miongoni mwa watu Wake katika siku zile za mwisho WASINGETAKA kuyasikia mafundisho Yake juu ya KUPAJENGA MAHALI PALIPOBOMOKA, au UFA, na kuwafundisha watu UWAJIBIKAJI wa kuitunza Sabato ya siku ya saba. Zaidi ya hayo, wao wangeenda mbali sana hasa kwa KUJITAHIDI KUUFICHA UKWELI kwamba mahali pale palipobomoka palikuwa hapajabomoka, nao WANGEJARIBU KUPAFUNIKA kwa kuweka hapo Sabato ya Uongo [Jumapili] badala ya ile ya Kweli [Jumamosi].

"Ee Israeli, manabii wako wamekuwa kama mbweha, mahali palipo ukiwa. Hamkupanda kwenda MAHALI PALIPOBOMOLEWA, wala hamkuitengenezea nyumba ya Israeli BOMA, wapate kusimama vitani katika siku ya BWANA" (Ezekieli 13:4,5).

Suala lile lile linatajwa hapa, mifano ile ile imetumika, kama katika unabii ule wa Isaya. Kipindi ambacho mambo hayo yatatimizwa ni kipindi kile cha kujiweka tayari kwa siku ile ya Bwana. Siku ya Bwana inafuata baada ya siku ya wokovu na inamaanisha siku ile kuja kwa Kristo mara ya pili kutakapotokea.

## "BWANA HAKUWATUMA"

Ndipo katika siku hizo, manabii wa Mungu, na wachungaji, watakuwa wameshindwa kufanya kile ambacho wangekuwa wamefanya, na kile ambacho Mungu ALIWATAZAMIA KUFANYA ----- KUWAFUNDISHA WATU WAO SHERIA ya Mungu. Kufanya hivyo kungemaanisha KUWATAYARISHA watu wao kusimama katika wakati ule ambapo vitu vingine vyote VITAPINDULIWA. Lakini badala ya wao kufanya hivyo "wameuona ubatili, na uganga wa uongo, hao wasemao, BWANA asema; nao WAMEWATUMAINISHA watu ya kuwa neno lile litatimizwa" (Ezekieli 13:6).

Lakini ule "uganga [wao] wa uongo" wanaposema "BWANA asema" HAUTASIMAMA, kwa maana Mungu anawaambia: "Je! hamkuona maono ya bure, hamkunena mabashiri ya uongo? nanyi mwasema, BWANA asema; ila MIMI SIKUSEMA NENO. Basi tazama, Bwana MUNGU asema hivi; kwa sababu mmenena ubatili, na kuona uongo, basi, kwa sababu hiyo, Mimi ni juu yenu, asema Bwana MUNGU. Na mkono wangu utakuwa juu ya manabii wanaoona ubatili, na kutabiri uongo; hawatakuwa katika MASHAURI ya watu Wangu, wala HAWATAANDIKWA katika maandiko ya nyumba ya Israeli, wala HAWATAINGIA katika nchi ya Israeli; nanyi MTAJUA ya kuwa Mimi ndimi Bwana MUNGU" (Ezekieli 13:7-9)

## "MMOJA ALIJENGA UKUTA"

Sababu imekwisha tolewa kwa nini WATAADHIBIWA. "Kwa sababu hiyo, kwa sababu WAMESHAWISHI watu Wangu, wakisema, AMANI; wala HAPANA AMANI; na MTU MMOJA ajengapo [alijenga] ukuta, tazama, WAUPAKA CHOKAA ISIYOKOROGWA VEMA" (Ezekieli 13:10).

Hapa kuna utabiri wa jaribio litakalofanywa na viongozi wa dini KUFUNIKA MAHALI PALE PALIPOBOMOLEWA katika [ukuta wa] SHERIA ya Mungu. Mahali hapo palipobomolewa palitokea kwa KUIONDOA amri ile ya nne, yaani, AMRI YA SABATO.

Sasa "MMOJA" anajenga ukuta, na "WENGINE" wanajitahidi kuuficha ukweli huu kwamba SABATO YA UONGO [JUMAPILI] imewekwa na yule "MMOJA" badala ya SABATO YA KWELI [JUMAMOSI] ya YEHOVA [BWANA]. Wanafanya hivyo kwa KUIPAKA siku hiyo [Jumapili] iliyowekwa mahali hapo [ilipokuwa Sabato], au huo ukuta wa bandia, "CHOKAA ISIYOKOROGWA VEMA" ili kupajaza MAHALI HAPO PALIPOBOMOLEWA [kwa kuiondoa Sabato].

Basi, hapa tunao unabii unaoonyesha kwamba JARIBIO litafanywa katika siku za mwisho KUUFUNIKA UKWELI usemao kwamba SABATO YA MUNGU haijapewa HESHIMA yake inayostahili kwa kuondolewa katika Sheria [ya Mungu], na SABATO YA UONGO nyingine kuwekwa mahali pake. Yule "MMOJA" aliyeujenga "UKUTA [HUO] HAFIFU" (pambizo) alikuwa ni KANISA LA ROMA. "WENGINE" ambao "WAUPAKA CHOKAA ISIYOKOROGWA VEMA" ni MAKANISA YA KIPROTESTANTI ambayo yanawafundisha watu kuwa badiliko hilo [la Sabato] lilifanywa kwa idhini na mamlaka ya Mungu. Ile "CHOKAA ISIYOKOROGWA VEMA," ambayo kwayo wanajaribu kuufunika ukweli halisi wa Sabato hii ya Bandia [Jumapili], ni kule kusema kwao kuwa "BWANA asema" wakati Bwana HAJASEMA NENO LO LOTE kama hilo.

## MISINGI ITAFUNULIWA

Bwana anao UJUMBE WA PEKEE kwa wale wanaojaribu kufunika ukweli dhahiri kwa kuiweka Jumapili mahali pa Sabato: "Basi waambie hao wanaoupaka ukuta CHOKAA ISIYOKOROGWA VEMA, ya kwamba UTAANGUKA; kutakuwa mvua ya kufurika; nanyi, enyi MVUA YA MAWE MAKUBWA YA BARAFU [Ayubu 38:22,23; Ufunuo l6:21], MTAANGUKA; na upepo wa dhoruba UTAUPASUA [ukuta wa bandia]. Na huo ukuta utakapoanguka, je! hamtaambiwa, Ku wapi kupaka kwenu mlikoupaka? Basi Bwana MUNGU asema hivi; Nitaupasua kwa upepo wa dhoruba, katika ghadhabu yangu [Ufunuo l5:l]; tena kutakuwa na mvua ya barafu ya kufurika katika hasira yangu; na mawe makubwa ya barafu katika hasira ya KUUKOMESHA. Ndivyo nitakavyoubomoa ukuta mlioupaka chokaa isiyokorogwa vema, na KUUANGUSHA CHINI, hata MISINGI YAKE ITAFUNULIWA; nao

UTAANGUKA, nanyi MTAANGAMIZWA katikati yake; nanyi MTAJUA ya kuwa mimi ndimi BWANA" (Ezekieli 13:11-14).

Hivi sasa Mungu anaupa ulimwengu maarifa ya KUIJUA SABATO YAKE pamoja na KWELI zingine nyingi. "Tena habari njema ya ufalme," kasema Kristo, "itahubiriwa katika ulimwengu wote, KUWA USHUHUDA kwa mataifa yote; hapo ndipo ule MWISHO utakapokuja" [Mathayo 24:14]. Mungu anawaambia sasa wale wanaoupaka ukuta wao wa bandia [Jumapili] chokaa isiyokorogwa vema, kwamba "UTAANGUKA." Wakati unakuja ambapo hasira ya Mungu juu ya wale wanaoitangua Sheria Yake HAITAZUIWA tena. Katika siku ile "MISINGI" ya kuiweka Jumapili "ITAFUNULIWA," ndipo "nanyi, enyi MVUA YA MAWE MAKUBWA YA BARAFU, MTAANGUKA." Walakini, siku ile, Mungu atakapounyosha mkono wake KUWAADHIBU wakazi wa dunia hii kwa uovu wao, itakuwa baada ya wale wote watakaotaka kuitoa mioyo yao na maisha yao ili KUMTII Yeye watakapokuwa wamefanya hivyo. Wanaomfuata Mwana-Kondoo IDADI YAO ITAKUWA IMEKAMILIKA, NA MLANGO WA REHEMA [TOBA] UTAKUWA UMEFUNGWA [Ufunuo 22:11]. (Angalia Isaya 26:20,21; Ufunuo 16:17-21.) Wakati wa kujifunza ukweli huu juu ya suala hili la Sabato ni sasa, kwa maana "Wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa" [2 Wakorintho 6:2]. Sio jambo la muhimu tu bali ni la lazima kwetu sisi KUMTII Mungu SASA.

## WAMEFUMBA MACHO YAO WASIIANGALIE SABATO

Hapana shaka lo lote kwamba ni suala hili la Sabato ambalo Mungu analishughulikia kwa njia ya kutumia mafumbo katika unabii wote huo, kwa maana, tukiutaja tena mfano ule ule wa "chokaa isiyokorogwa vema" katika kitabu cha Ezekieli, Anasema:

"Makuhani wake wameihalifu sheria yangu, wametia unajisi vitu vyangu vitakatifu; hawakuweka tofauti ya vitu vitakatifu na vitu vya kutumiwa siku zote; wala HAWAKUWAFUNDISHA WATU kupambanua vitu vichafu na vitu vilivyo safi, NAO WAMEFUMBA MACHO YAO, WASIZIANGALIE SABATO ZANGU, nami nimetiwa unajisi kati yao. Wakuu wake kati yake wamekuwa kama mbwa-mwitu wakirarua mawindo; ili kumwaga damu, na KUHARIBU ROHO ZA WATU, wapate faida kwa njia isiyo halali. Na manabii wake WAMEUPAKIA CHOKAA ISIYOKOROGWA VEMA, wakiona ubatili, na kuwatabiria maneno ya uongo, wakisema, Bwana MUNGU asema hivi; iwapo BWANA hakusema neno.... Nami nikatafuta mtu miongoni________________________________________________________________
________________________________________________________________ Wanafunzi Wake Kristo wangerudi leo na kuja kufundisha katika miji yetu hali wana UKATA [UMASKINI] na NJA kama walivyokuw______________________________________________________________
________________________________________________________________________
________†__________________________________†_____________________________
_________________________________E KUTENGENEZA MAHALI PALIPOBOMOKA; na, MWENYE KUREJEZA NJIA ZA KUKALIA" (Isaya 58:12).

Hivyo ni wazi kutokana na unabii huu kwamba katika siku za mwisho watu fulani watajitahidi kuirejeza Sabato mahali pake pa halali katika Sheria ya Mungu; kwamba wao wenyewe wataitunza siku ya saba kama Sabato; kwamba wata"PIGA KELELE," nao [HAWATAACHA], na wata"PAZA SAUTI [ZAO] kama tarumbeta" ulimwenguni kote ku"WAHUBIRI WATU WA MUNGU KOSA LAO"; kwamba itawapasa kupambana na upinzani mkali sana kutoka kwa viongozi wale wa dini watakaoishi kipindi chao, ambao watajiunga upande wa Upapa kuipinga kweli ya Mungu; kwamba watatambuliwa na Mungu kama watu wake wanaopatengeneza mahali palipobomoka katika [ukuta wa] Sheria Yake; na hatimaye, kutokana na uaminifu na unyofu wao, watapandishwa mahali pa nchi palipoinuka, na kupewa urithi wa Yakobo baba yao, ambao ni NCHI MPYA.

## KUITWEKA BENDERA

Unabii mwingine ambao bila shaka unalihusu kundi hili la siku za mwisho litakaloiinua juu sheria unapatikana katika Isaya. "Piteni, piteni, katika malango; Itengenezeni NJIA ya watu; Tutieni, tutieni BARABARA; toeni mawe yake; TWEKENI BENDERA kwa ajili ya kabila za watu. Tazama, BWANA ametangaza habari mpaka MWISHO WA DUNIA, Mwambieni binti Sayuni, Tazama, thawabu yake i pamoja naye, Na malipo yake yako mbele zake" (Isaya 62:10,11).

Mfano huu umechukuliwa katika desturi ile ya zamani ya kuviondoa vizuizi vyote katika njia ya mfalme anayemtembelea mfalme mwingine. Barabara maalum ilitengenezwa kwa ajili yake kutembea juu yake, mawe yote yaliondolewa, na mchukua bendera alimtangulia mbele, na mpiga mbiu akitangaza kuja kwake [mfalme huyo].

Kulingana na unabii huu jambo fulani linalofanana na hilo halina budi kutangulia kabla ya kuja mara ya pili kwa Kristo. Hapana shaka kwamba unabii huu unahusu kuja kwa Kristo mara ya pili, kwa maana unasema ataleta thawabu Yake pamoja naye, Yeye hawezi kufanya hivyo mpaka hapo atakapokuja mara ya pili (Ufunuo 22:l2). Kuhusiana na kuja kwake unabii huu unatangaza kwamba njia kuu haina budi kutengenezwa. Hiyo tayari tumekwishaiona kuwa inahusu MAPITO ya amri Zake. Unabii unatangaza pia kwamba BENDERA (STANDARD) haina budi kutwekwa kwa ajili ya kabila za watu. BENDERA hiyo ni SHERIA YA MUNGU. Ni KIPIMO (STANDARD) cha HUKUMU ya Mungu. [Sheria] ilikuwa kipimo alichotumia Mungu kumhukumu Ibrahimu. "Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na Sheria zangu" (Mwanzo 26:5).

Hiyo [Sheria] ndiyo KIPIMO ambacho kwacho WAJIBU wote wa mwanadamu unajumlishwa. "Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri Zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu" (Mhubiri 12:13).

Hiyo [Sheria] ndiyo KIPIMO ambacho kwacho wanadamu wote WATAHUKUMIWA. "Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, AMEKOSA juu ya yote. Kwa maana yeye aliyesema, Usizini, pia alisema, Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa MVUNJA SHERIA. Semeni ninyi, na kutenda kama watu WATAKAOHUKUMIWA KWA SHERIA YA UHURU" (Yakobo 2:10-12).

## KANISA LA MWISHO LA KIKRISTO

Ukweli uo huo umeelezwa wazi katika Agano Jipya pamoja na lile la Kale. Katika maono yake matakatifu Mtume Yohana, akiwa kisiwani Patmo, aliruhusiwa kuangalia mpaka mwisho wa karne za Kipindi cha Kikristo. Analiona Kanisa la Mwisho la Kikristo, yaani, Kanisa ambalo litamlaki Bwana atakapokuja mara ya pili. Naye Yohana analieleza hivi kanisa hilo. "Joka akamkasirikia yule mwanamke [kanisa], akaenda afanye vita juu ya wazao wake WALIOSALIA, WAZISHIKAO AMRI ZA MUNGU, na KUWA NA USHUHUDA WA YESU" (Ufunuo l2:17).

"JOKA" hapa anamwakilisha Shetani. "MWANAMKE" analiwakilisha Kanisa la Kristo. "WAZAO WAKE WALIOSALIA" huhusu Kanisa mpaka mwisho kabisa wa dunia, Kanisa litakalokuwako wakati wa kuja mara ya pili kwa Kristo. Hapa Kanisa linaonyeshwa kuwa lina tabia za pekee mbili: Kwanza, LINASHIKA AMRI ZA MUNGU; pili, LINA KARAMA YA UNABII [ROHO YA UNABII], ambayo ndiyo USHUHUDA WA YESU (Ufunuo 19:10). Kanisa hili la mwisho litakuwa ni KANISA LINALOSHIKA SABATO, kwa maana kwa kweli isingeweza kusemwa kamwe juu ya kanisa lo lote ambalo halishiki Sabato kuwa lilizishika amri za Mungu. Kanisa linalozishika amri za Mungu tisa tu ni kanisa linalovunja amri za Mungu. Kanisa hilo la mwisho ni Kanisa lishikalo amri zote, ni kanisa lishikalo Sabato.

Tena Yohana, akiangalia mbele kupita karne zote, anauona ujumbe ule wa mwisho wa injili ukihubiriwa kwa '"Kila taifa na kila kabila na lugha na jamaa." Anaueleza ujumbe huo katika sura ile ya kumi na nne ya Ufunuo. Ujumbe huo ni wa aina tatu, na hapo utakapotimizwa, ndipo Kristo ATAKAPOONEKANA akija na mawingu ya mbinguni kuvuna mavuno ya nchi (Ufunuo 14:14,15). Kwa hiyo huo lazima uwe ni ujumbe wa mwisho kutolewa kwa wanadamu. Yohana pia anawaona watu wale watakaoutoa ujumbe huo, naye anaeleza hivi habari zao: "Hapa ndipo penye subira ya WATAKATIFU, hao WAZISHIKAO AMRI ZA MUNGU na IMANI YA YESU" (Ufunuo 14:l2).

Kwa hiyo katika Agano la Kale na Jipya Mungu anaonyesha wazi kwa mwanafunzi wa Biblia ya kwamba KILA MKRISTO ANAWAJIBIKA KUSHIKA KILA SEHEMU YA SHERIA YAKE TAKATIFU. Katika siku hizi za mwisho Sheria hii itakuwa KIPIMO CHA IMANI ya watu wa Mungu. Na wale ambao kwa uaminifu WATASHINDA katika jaribio [Kipimo] hilo wanapewa ahadi hii: "Heri wale wazishikao amri Zake, wawe na haki kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake" (Ufunuo 22:14, Tafsiri ya King James Version)

SURA YA 9

## KUYAKAMILISHA MATENGENEZO YALIYOSITISHWA

Wakati wa hatari unaotisha mno katika historia yake yote [ya Matengenezo ya Kanisa] sasa unalikabili Kanisa la Kikristo. Imani ya watu katika Biblia kama Neno la Mungu lililovuviwa na lenye mamlaka inaharibiwa sio tu kutokana na mashambulio yatokayo nje ya Kanisa bali pia kwa wale wanaokalia vyeo vya juu vinavyotegemewa wanapohubiri katika mimbara zao.

Ushawishi ule wenye sumu unaotaka kuifanya dini iende sambamba na hali ya dunia ya sasa (Modernism), uchambuzi wa Maandiko uletao uharibifu (destructive criticism), imani ya mizimu (spiritualism), evalusheni (evolution) [imani kwamba vitu vyote vilitokea vyenyewe

bila Muumbaji kuviumba], pamoja na moyo ule walio nao wachungaji wa madhehebu mbalimbali usiotaka kukubali mafundisho dhahiri ya Biblia badala ya thiolojia ya kila dhehebu, mambo ambayo yanawakengeusha watu kutoka nje ya mafundisho makuu ya msingi ya Biblia, na kuwafanya waweke tumaini lao katika thiolojia iliyotungwa na wanadamu tu.

Mkondo katika ulimwengu huu wa Kikristo ni kuwapeleka watu mbali na zile kweli rahisi za Neno la Mungu. Hii inatokana na sababu ya kwamba katika miaka ya hivi karibuni nadharia nyingi potofu, zilizotungwa kwa werevu na wanadamu wenyewe, zimezuka ndani ya kanisa. Mwelekeo wa nadharia hizo ni kuwafanya wanadamu kuweka imani na tumaini lao la wokovu kwa wanadamu hao, katika juhudi za kibinadamu, katika mifumo iliyobuniwa na wanadamu, badala ya KUMTEGEMEA Mungu, na MPANGO WAKE MKUU aliouweka kwa ajili ya WOKOVU wa wanadamu. Kanuni hizo za uongo pamoja na nadharia za kuwazia tu huchukua mahali pa injili safi ya Kristo katika mioyo ya watu wengi.

Mafundisho hayo ya uongo yanaifagilia mbali imani ya watu katika Biblia kama ndilo Neno la Mungu. Na shambulio hilo juu ya ukweli wa kimsingi wa Ukristo halitoki nje ya kanisa, kama ilivyokuwa zamani.. Palikuwa na wakati ambapo kanisa lililazimika kujitetea lenyewe kutokana na maadui zake wa nje. Makafiri, wale wanaokana kuwako kwa Mungu (atheists), na wale wanaokana kuwa hakuna habari za Mungu zinazoweza kupatikana (agnostics), sikuzote wamefurahi kuonyesha kile wanachodhani ni makosa katika Biblia, na kucheka kile wanachokiita ujinga wa watu wa Mungu kwa kusadiki Maandiko. Lakini hao walikuwa ni maadui wa wazi wa msalaba, na kamwe halikuwa jambo gumu kupambana na mashambulio yao na kuwashinda.

## UASI MPYA

Lakini hali ya mambo sasa imebadilika. Maadui hao wa ile kweli sasa wamo ndani ya kanisa, wamejiimarisha kwa kuwa na vyeo vyenye mamlaka kubwa na mvuto katika mimbara zao, seminari zao za thiolojia, nyumba zao kuu za kuchapisha vitabu. Kutoka mahali pao pa juu wanaongoza shambulio jipya, ni shambulio la kutisha mno dhidi ya Neno la Mungu pamoja na mafundisho yake yaliyovuviwa.

Kwa kweli huu ni uasi mpya. Majeshi hayo yanaliharibu kabisa kanisa kwa kulidhoofisha misingi yake, na kuzisumisha chemchemi zake za uzima, na wakati uo huo wakijidai ya kwamba wao ni marafiki zake [kanisa]. Kama Bwana wake Mbinguni, Biblia ----- NENO LA MUNGU ----- inajeruhiwa "katika nyumba ya rafiki [zake]" [Zekaria 13:6].

Kwa hiyo, mwito unaotolewa leo ni ule wa kutoa tangazo jipya kuhusu KWELI ZILE ZA ZAMANI, na kuwataka watu kurejea katika IMANI ILE YA MWANZO itokayo katika Biblia. Haja kuu ya saa hii sio tu kuwa na IMANI ile ya Kikristo, bali pia kuwa na MAISHA ya Kikristo yaliyojengwa juu ya Biblia na Biblia peke yake.

Wakati ule wa Zama za Giza ukweli wa injili ulifunikwa na giza na makosa yaliyotokana na mafundisho potofu yaliyokuwa yameingizwa kanisani kutoka kwenye upagani. Ushirikina na ujinga vikakithiri mioyoni mwa wanadamu, na kuyaondoa maarifa ya kweli nyingi sana tukufu za Biblia.

Martin Luther alikuwa ni mtu mashuhuri miongoni mwa wale walioitwa na Mungu ili kuutoa ulimwengu katika giza la mfumo ule potofu wa dini na kuuingiza katika imani iliyo safi zaidi. Alikuwa amejitoa kuifanya kazi hiyo kwa moyo wake wote, alikuwa na ari, na bidii. Hakujua hofu yo yote bali kumcha Mungu tu, hakuukubali msingi wo wote wa imani ya dini, isipokuwa ule tu uliojengwa juu ya Maandiko Matakatifu. Alikuwa mtu mwenye cheo kikubwa anayefaa kwa kipindi chake. Kwa njia ya mtu huyu na wenzi wake waaminifu Mungu alifanikiwa kufanya kazi kubwa ya kulitengeneza Kanisa Lake na kuuelimisha ulimwengu.

## MAENDELEO YA MATENGENEZO

Lakini Mungu hakumfunulia Luther kweli Yake yote. Alikusudia kwamba kazi ile ya Matengenezo [ya Kanisa] ingesonga mbele hatua kwa hatua, na kwamba watu wangeiweka mioyo yao wazi katika kuyachunguza Maandiko hayo na kuwa tayari daima kupokea nuru mpya ambayo angewapelekea kwa maongozi Yake. Walakini, Luther alipokufa, wale waliokuwa wameshirikiana naye hawakuendelea kujifunza kweli yote ya Mungu. Wafuasi wake wakayakusanya pamoja yale yote [Luther] aliyoyasadiki, na kutokana na hayo wakatengeneza KANUNI (CREED) YA IMANI yao. Wakakaa raha mustarehe katika kanuni hiyo ya imani yao kana kwamba walikuwa wamesonga mbele sana kama ilivyowezekana katika maarifa ya kuijua kweli.

Mungu alikuwa na KWELI ZINGINE alizotaka kuzifunua kwa ulimwengu mzima, lakini kwa kuitumia kanuni hiyo ya imani iliyojengwa juu ya IMANI YA LUTHER walifanya isiwezekane kwa Mungu kuupelekea ulimwengu kweli nyingi zaidi kupitia kwao. Watu wanapokataa kupokea kitu kingine zaidi ya kile kilichomo katika kanuni yao ya imani, basi, wanajifungia wenyewe mbali na NURU MPYA kwa kukataa kwao kwenda mbele zaidi ya kile kilichomo ndani ya kanuni yao ya imani.

Vivyo hivyo, Mungu akawaita watu wengine kuiendeleza mbele kazi ile ya Matengenezo [ya Kanisa]. Akamwita Knox na Calvin, na kupitia kwao alifanya kazi kubwa ya kuwajulisha watu kanuni za injili. Kazi ile ingepaswa kuendelea kukua. Wafuasi wa ile kweli wangepaswa kuendelea kuichunguza Biblia yao pasipo kukoma, hivyo wangeweza kuufikia zaidi na zaidi ujuzi wa ile kweli, na kuihubiri kwa ulimwengu. Badala ya kufanya hivyo, wakafanya KOSA LILE LILE lililokuwa limefanywa mapema. Madhehebu zingine zikaanzishwa. KANUNI ZA IMANI (CREEDS) zikajengwa kutokana na mafundisho ya Knox na Calvin, na wafuasi wao wakakaa raha mustarehe juu ya kanuni hizo za imani kana kwamba hizo zilikuwa ndiyo jumla ya kweli yote.

Mungu akawawezesha watu wengine zaidi kuiendeleza kazi ya kweli Yake. Alikusudia kuufunulia ulimwengu wote kweli Yake katika utimilifu wake wote, naye akatafuta watu ambao kupitia kwao kazi hiyo ingeweza kufanyika. Wanamatengenezo (Reformers) wakatokea vile vile katika nchi ya Uingereza. Lakini wakati walipokuwa wanayakataa baadhi ya makosa ya Roma, waliendelea kuzitunza kawaida zake nyingi. Kwa hiyo, wakati mamlaka na kanuni ya imani ya Kanisa la Roma inakataliwa, si chache kati ya kawaida na sikukuu zake zilizoingizwa katika ibada ya Kanisa la Uingereza (Church of England).

# "HUZUNI KUU INAYOPASWA KUOMBOLEZEWA"

Mungu akawapa Mababa Wasafiri (Pilgrim Fathers) NURU KUBWA ZAIDI pamoja na KWELI Yake, wakijumuishwa na wale walioitwa Wapyuritani (Puritans) [ambao walizikataa kawaida za ibada kama zile za Roma]. Hao walitamani kwa dhati kurudi katika mfumo wa ibada rahisi usiokuwa na mapambo na usafi wa kanisa lile la Mitume, lakini waliteswa na kufukuzwa watoke nje ya Uingereza, nao wakaja huku Amerika. Kwamba wengine miongoni mwao walitambua wazi msimamo sahihi ambao wote wangekuwa nao kuihusu KWELI ni dhahiri ukiziangalia semi zilizomo katika hotuba ya kuagana iliyotolewa na mmojawapo wa wachungaji wao, John Robinson, aliyoitoa pwani ya nchi ile ya Holland wakati wale Mababa Wasafiri walipokuwa karibu kuondoka kwenda Amerika. John Robinson alisema hivi:

"Ndugu zangu, sisi tuko hapa kabla hatujatengana kwa muda mrefu kuanzia sasa, na Bwana ajua kama nitakuwa hai kuweza kuziona nyuso zenu tena. Lakini kama Bwana ameagiza jambo hili au la, nawaapisha mbele zake Mungu na mbele ya malaika zake watakatifu ya kwamba msinifuate mimi zaidi ya vile nilivyomfuata Kristo. Endapo Mungu atawafunulia ninyi neno lo lote kwa njia ya chombo [mtumishi] Chake kingine, IWENI TAYARI KULIPOKEA kama vile ambavyo mngepata kuupokea ukweli wo wote kutokana na huduma yangu mimi, kwa maana nina imani kubwa sana kwamba Bwana anazo KWELI NYINGI SANA NA NURU ambazo zitajitokeza kutoka katika Neno Lake takatifu." ----- W. CARLOS MARTYN, THE PILGRIM FATHERS OF NEW ENGLAND (1867), uk. 70.

"Kwa upande wangu mimi, siwezi kuomboleza ya kutosha kuhusu makanisa yale ya Matengenezo (Reformed Churches), ambao wamekifikia kipindi hiki cha dini, nao hawataki kusonga mbele zaidi kuliko [waasisi] vyombo vile vya Matengenezo yao. WALUTHERI hawawezi kushawishika kwenda mbele zaidi ya kile LUTHER alichokiona,... na WAKALVINISTI (Calvinists), kama ujuavyo, wanapashikilia sana pale pale walipoachwa na mtu yule mkuu wa Mungu, ambaye alikuwa bado hajayaona mambo yote. Hii ndiyo HUZUNI KUU inayopaswa KUOMBOLEZEWA, kwa maana japokuwa [waasisi hao] walikuwa mianga iliyowaka na kung'aa sana katika nyakati zao, walakini walikuwa HAWAJAPENYA BADO NA KUYAJUA MAUSIA YOTE ya Mungu, hata hivyo, kama wangekuwa hai leo, wangekuwa tayari kabisa KUPOKEA NURU ZAIDI kama walivyofanya walipoipokea ile ya kwanza." ----- DANIEL NEAL, HISTORY OF THE PURITANS (1848), Vol. I, Uk. 269,270

"Kumbukeni agano la kanisa lenu, ambalo mmekubali kwenda katika njia zote za Bwana, zile MLIZOJULISHWA au MTAKAZOJULISHWA. Kumbukeni ahadi yenu na agano lenu na Mungu pamoja na ninyi kwamba mtakuwa tayari kuipokea NURU YO YOTE na KWELI ITAKAYOFUNULIWA kwenu kutoka katika Neno Lake lililoandikwa; zaidi ya hayo, jihadharini, nawasihi, kile mnachopokea kama KWELI, kilinganisheni na kukipima kwa kutumia Maandiko mengine ya kweli kabla hamjakipokea [Matendo ya Mitume 17:11; 1 Wathesalonike 2:13]; kwa maana haiwezekani kwamba ulimwengu huu wa Kikristo uweze kutoka hivi karibuni tu katika giza lile nene la Mpinga Kristo na kuwa na ujuzi mkamilifu wa maarifa [ya Neno la Mungu] mara moja." ----- THE PILGRIM FATHERS OF NEW ENGLAND, uk.70,71.

Kweli huo ulikuwa ni ushauri mzuri kabisa, na ungepaswa kuzingatiwa kwa makini na kutiiwa kwa moyo mnyofu, kama ilivyokuwa kweli kwa wale Wasafiri kule Plymouth kwa kipindi fulani. Walakini, kabla wale Wapyuritani hawajajiimarisha kule Massachusetts Bay wakaanza kuzivunja kanuni zote za Ukristo na Uprotestanti kwa kuanzisha mfumo wa UTAWALA WA MAKASISI (Theocracy), na kujiingiza katika pilikapilika za kuwatesa wale ambao walikuwa hawakubaliani nao (dissenters). Wao wenyewe hawakutaka kusonga mbele zaidi ya kanuni yao ya imani waliyojiwekea wenyewe; wala hawakutaka kumruhusu mtu mwingine ye yote kufanya hivyo.

KUSONGA MBELE KWA ILE KWELI KULIZUIWA

Akina Wesley wakaitwa na Mungu, nao wakafanya kazi kubwa ya injili. Watu wakazipokea KWELI FULANI TU, na kutokana na hizo wakajitengenezea kanuni zao za imani, huku wakiwa wanakataa kupokea KWELI ZAIDI kuliko zile zilizokuwamo katika mipaka finyu ya kanuni zao za imani, wakawa wamejifungia wenyewe mbali na Mungu; WALIMWEKEA MIPAKA MTAKATIFU WA ISRAELI. Wafuasi wake Wesley wakafanya KOSA LILE LILE walilofanya wale waliowatangulia, WAKICHAGUA KWELI CHACHE TU miongoni mwa kweli nyingi za Mungu ambazo alikuwa nazo kwa ajili ya kuwapelekea walimwengu, wakiziweka kwa MUHTASARI katika kanuni yao ya imani KUZUIA NURU YA ZIADA iliyokuwa inawajia kutoka Mb________________________________________
________________________________________i kipindi kile cha kujiweka tayari kwa siku ile ya Bwana. Siku ya Bwana inafuata baada ya siku ya wokovu na inamaanisha siku
________________________________________________________________
________________________________________"

Ndipo katika siku hizo, manabii wa Mungu, na wachungaji, watakuwa wameshindwa kufanya kile ambacho wangekuwa wamefu, maana ndio utimilifu wa matumaini yote ya Kanisa la Kikristo.

Wakati ulikuwa unakaribia ambapo ukweli huu mkuu ulipaswa kuhubiriwa ulimwenguni kote. Lilikuwa ni kusudil lake Mungu kulifunua fundisho hili kwa, na kulifanya lihubiriwe na, wale aliokuwa amewaita kuwa viongozi katika kazi ile ya Matengenezo [ya Kanisa]. Lakini kutokana na njia ile waliyoifuata wakajifungia wenyewe mbali ukweli huu mpya. Basi, wakati ulipofika wa kuhubiriwa ujumbe huu wa kuja Kwake ulimwenguni, aliona ni lazima aende tena nje ya makanisa yale yaliyokuwa yamejiimarisha na kuanzisha kundi jingine ambalo lingeweza kutangaza hadi miisho ya ulimwengu habari hii ya kuja kwa Kristo mara ya pili.

Pamoja na ujumbe huu wa marejeo Yake Kristo, Mungu alikusudia ya kwamba KWELI ZAKE ZOTE ambazo zilikuwa zimefundishwa kwa kuzipotosha na kufichwa wakati ule wa

ZAMA ZA GIZA zingefanywa kuwa wazi kwa jamii ya kibinadamu, ili wakati wa kuja Kwake upate kufunuliwa utimilifu wa KWELI YOTE kwa ulimwengu mzima. Mengi miongoni mwa makanisa yale ya Kiprotestanti, katika kujitenga kwao na Roma, yalikuwa yamechukua pamoja nayo baadhi ya MAKOSA yale ya Roma.

## MATENGENEZO YA SABATO

Miongoni mwa MAKOSA hayo ulikuwa ni utunzaji wa siku ya kwanza ya juma mahali pa Sabato ya kweli ya Mungu, ambayo ni siku ya saba. Utunzaji wa Sabato ulibadilishwa na Kanisa la Roma, na Waprotestanti wengi, bila kuchunguza asili yake, wakaikubali [Jumapili] pamoja na mambo mengine ambayo walikuwa hawajayachunguza. Katika UJUMBE HUU WA MWISHO Mungu alikusudia kuwapelekea jamii ya kibinadamu kabla tu ya kuja Kwake ulimwenguni, utata kuhusu suala hili ungeondolewa, na Sabato ya kweli ya Mungu INGERUDISHWA MAHALI PAKE HALALI katika Injili na katika mioyo ya watu wa Mungu. Hivyo ujumbe huu wa Mungu wa mwisho zaidi ya kuwa na ukweli wa kuja mara ya pili kwa Kristo, utakuwa na ukweli juu ya suala hili la Sabato. Jambo hilo litakapohubiriwa kwa watu wote duniani, nao watakuwa na WAJIBU ULE ULE wa kuikubali na kuyarekebisha maisha yao ili yapatane nayo kama vile ilivyokuwa kwa watu wale wa siku za Luther waliokuwa chini ya uwajibikaji wa kutembea katika nuru ile ambayo Mungu aliifanya iangaze njiani mwao.

Miongoni mwa MAKOSA mengine yaliyoletwa katika baadhi ya makanisa ya Kiprotestanti kutoka Kanisa la Roma ni mafundisho yale yanayohusu MATESO YA MILELE NA MILELE [MOTONI], UBATIZO wa watoto wachanga, na KUNYUNYIZA kama njia ya ubatizo. Hakuna hata moja katika hayo lililo na msingi uliojengwa katika mafundisho ya Biblia. Katika ujumbe huu wa mwisho ambao utakwenda kwa ulimwengu wote ni lazima MAKOSA YOTE hayo yatupiliwe mbali na wale ambao wangetaka kuipokea KWELI katika utimilifu wake kutoka kwa Mungu.

Hivyo inaweza kuonekana ya kwamba ujumbe huu wa kuja mara ya pili kwa Kristo na kuzishika amri za Mungu sio tu ujumbe wa mwisho wa Injili, bali pia ni UKAMILISHAJI WA MATENGENEZO [YA KANISA] yale ya karne ile ya kumi na sita, ambayo mpaka sasa YAMEZUIWA na KUSITISHWA kwa njia ya kuanzishwa kwa KANUNI ZA IMANI (CREEDS) za madhehebu mbalimbali.

Ni jambo la muhimu sana kwa Wakristo wote kwamba wajihadhari WASIKUBALI KUFUNGWA NA KANUNI YO YOTE YA IMANI, hata kama inaonekana kuwa ni kamilifu. Bado kuna NURU ZAIDI itakayofunuliwa kutoka katika Biblia, na Mungu anapoifunua

kwetu, tungekuwa na mwelekeo wa moyo utakaotuwezesha KUIPOKEA Wakristo wasingekuwa na kanuni nyingine ya imani isipokuwa ile ya Biblia takatifu peke yake. Imani yetu ingejengwa juu yake [Biblia], na endapo itagundulika ya kwamba tunakiamini kitu cho chote ambacho hakiwezi kuthibitishwa na mafundisho ya Biblia, basi, itabidi fundisho hilo litupiliwe mbali mara moja. Biblia na Biblia peke yake ingekuwa ndio msingi wa dini ya Wakristo.

Katika wakati huu ambapo watu walio na elimu kuu na vyeo vya juu katika makanisa wanajitahidi sana kuthibitisha kwamba Biblia haisemi kweli, ni muhimu kwa mtu yule wa IMANI kujiimarisha mwenyewe na kinga ile inayopatikana katika ukweli uliomo katika Biblia. JIFUNZENI Biblia zenu kwa dhati, ZICHUNGUZENI kwa bidii, na kuzitumia kanuni zake takatifu katika MAISHA yenu [Yakobo 1:22].

"Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga KWELI viunoni, na kuvaa dirii ya HAKI kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa INJILI ya amani; zaidil ya yote mkiitwa ngao ya IMANI, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya WOKOVU, na upanga wa Roho ambalo ni NENO LA MUNGU; kwa SALA zote na MAOMBI mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote" (Waefeso 6:13-18).

.

.

## SURA YA 10

## KWENDA NURUNI

Hakuna kazi ya juu zaidi kwa mtu ye yote mwenye akili kuliko ile ya KUJIFUNZA MAANDIKO ili kujua KWELI ni nini. Siku kwa siku Biblia ingechunguzwa kwa bidii. Kila wazo linalokuja moyoni halina budi kupimwa kwa uangalifu, Maandiko yalinganishwe na Maandiko. Kwa njia hii, kwa msaada wa Roho wa Mungu, tungekuwa na maoni yetu wenyewe, kwa maana inapaswa kukumbukwa ya kwamba sisi wenyewe ITATUPASA KUJIBU mbele zake Mungu kwa mambo yale yanayotuhusu.

Neno la Mungu likichunguzwa kwa njia hiyo, ndipo UJUZI wa ile kweli utakapotolewa kwetu. Kuyachunguza Maandiko kutatuongoza, hatua kwa hatua, kuingia katika kweli yote. Nuru ya ile kweli inapokuja, ni LAZIMA ifuatwe. Kwa njia hiyo tu ndipo KWELI ZAIDI itatolewa kwetu. Watu wanapokwenda katika NURU WALIYO NAYO, hapo ndipo NURU ZAIDI watapewa. Hawawezi kutegemea kuongozwa na Roho wa Mungu mpaka wawe tayari KUIFUATA NJIA YOTE. Kamwe hapatakuwa na wakati katika maisha ya Mkristo itakapokuwa ni sawa kurudi nyuma wakati KWELI INAFUNULIWA kwa njia ya Neno la Mungu kwa Roho Wake. NURU hiyo itageuka na kuwa GIZA kama watu watakataa kwenda katika [nuru] hiyo.

Mungu atawapelekea watu wake KWELI NYINGI ZAIDI NA ZAIDI mpaka mwisho wa wakati. Kutoka katika Biblia kila wakati zitakuja KWELI MPYA, kweli ambazo hazimo katika KANUNI ZA IMANI [CREEDS] za makanisa. Ndivyo ilivyokuwa sikuzote. Luther aliitwa na Mungu kuipokea nuru mpya, naye alifanya hivyo, na matokeo yake yakawa yale Matengenezo Makuu [ya Kanisa] ya karne ile ya kumi na sita. Hivyo ndivyo Calvin na Knox na Wesley walivyopata nuru mpya, nao wakaenda katika nuru hiyo.

## UJUMBE WENYE KWELI YA JUU

Na sasa, katika siku hizi, Mungu ameupeleka ujumbe wake kwa ulimwengu wote, yaani, onyo la kukaribia kuja kwa Kristo mara ya pili. Katika ujumbe huo imo NURU MPYA. Ni

UKWELI WA WAKATI HUU [LEO], na wote wanaousikia ujumbe huo wanatakiwa KUUPOKEA.

Katika ujumbe huo imo nuru mpya juu ya suala la SABATO, asili ya mwanadamu, hali ya wafu, thawabu ya wenye haki, mwisho wa waovu, na miaka elfu moja. Mapambano makubwa kati ya KWELI na UONGO yako mbele yetu, pambano litakalofungia [historia ya dunia hii] ni PAMBANO KATI YA DHAMBI NA HAKI. Ni wale tu walioiimarisha mioyo yao na kweli hizi kuu za Biblia WATAKAOWEZA kusimama katika nyakati za taabu zilizo mbele yetu. Kwa kila mtu litakuja JARIBIO KALI, Je, inanipasa KUMTII Mungu kuliko mwanadamu? Naam, hata SASA tumo katika saa ile ya KUKATA MANENO [KUAMUA]. Unasimama upande gani? Je, UMEIKITA miguu yako juu ya MWAMBA ule IMARA, yaani, NENO LA MUNGU? Je, wewe hutetereki katika kuzitetea AMRI ZA MUNGU na IMANI YA YESU?

Wengi, hata waalimu wengine wa dini, wanadhani kwamba kufuata mafundisho safi ya Biblia katika "KIZAZI HIKI CHA MAENDELEO, ni mambo yaliyopitwa na wakati na yasiyofaa. Hawahusiki KUYASIKIA wala KUYAFUATA mafundisho hayo ya Mwokozi, wao wanapendelea kutia sahihi zao kwenye Kanuni ya Imani (Creed) iliyo na uhuru zaidi.

## KUTOPENDA KUICHUNGUZA KWELI

Dini safi ya Yesu Kristo inatiwa giza kwa kawaida za ibada zenye ubaridi na kwa nguvu ya Kanuni ya Imani(Creed). Tunaambiwa kwamba kizazi cha sasa ni chenye kuruhusu uhuru mkubwa sana katika masuala ya dini, na kwamba wachaji Mungu wa kweli wanakuwa na mawazo mapana sana. Hivyo maelfu ya watu wanawaruhusu wahubiri [wachungaji] wao kufanya kazi ya KUFIKIRI kwa niaba yao. Matokeo yake ni kwamba kuna makundi na makundi ya watu ambao hawawezi kutoa sababu yo yote kwa mambo yale wanayoyasadiki zaidi ya kusema tu kwamba walifundishwa hivyo na mchungaji wao. Njia ile inayokanyagwa kila siku ina WASAFIRI wengi sana, wakiwamo wengi wasiotaka kwenda kando [ya njia hiyo] na KUFANYA UTAFITI wao BINAFSI kuichunguza KWELI hiyo. Wengi wameridhika kufuata katika nyayo za WASOMI wao; wanakuwa na mashaka kuichunguza kweli hiyo wenyewe, basi, WANAFUNGWA KABISA na minyororo ya MAKOSA.

KWELI hiyo imekuja ulimwenguni, bali watu WANAPENDA GIZA kuliko NURU. Wanaifuata njia ile ya MAKOSA, nao wanapenda mambo yawe hivyo. Laiti Wanafunzi Wake Kristo wangerudi leo na kuja kufundisha katika miji yetu hali wana UKATA [UMASKINI] na NJAA kama walivyokuwa zamani walipokuwa wanafundisha katika vilima vile vya Galilaya, laiti wangetembelea baadhi ya MAKANISA YA KIFAHARI ambayo yanaitwa kwa majina ya Wanafunzi hao hao, mahali ambamo wale waabuduo huketi hali wamevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, na ambamo huyo FARISAYO WA KISASA anajitapa akisema kwa UBARIDI wake, "Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine," [Wanafunzi] hao wasingeweza kutoa ujumbe wao wa ile KWELI humo mpaka kwanza wangeulizwa maswali kuhusu DHEHEBU lao, tena wangepewa MTIHANI ambamo wangetakiwa kuyakubali mafundisho na kanuni zao za imani ambazo [Wanafunzi] hao HAWAKUPATA KUZISIKIA KAMWE.

## GIZA LAWEZA KUWA BADALA YA NURU

"NURU ingaliko pamoja nanyi muda kidogo. Enendeni maadamu mnayo NURU, iaminini NURU hiyo, ili mpate kuwa wana wa NURU" (Yohana 12:35,36).

Kuikataa NURU, yaani, kuikataa KWELI, huwafanya watu kwenda GIZANI, yaani, katika MAKOSA. Wengi wanausikia ujumbe wa Mungu wa mwisho. Wengine WANAUPOKEA, wengine WANAUKATAA. Matokeo ya kukataa ni kwamba GIZA litakuwa badala ya NURU, "tena anakwenda katika GIZA, wala hajui aendako."

Mwenye hekima alisema, "Bali njia ya WENYE HAKI ni kama NURU ing'aayo, IKIZIDI kung'aa hata mchana mkamilifu [atakapokuja Yesu]" (Mithali 4:18).

Nuru nyingi zaidi na zaidi itaangaza katika njia ya mtoto wa Mungu mpaka siku ile Kristo atakapokuja. NURU inapokuja kwetu, ni WAJIBU wetu KWENDA KATIKA [NURU] hiyo. Huu ndio wajibu mzito unaomkalia kila mtu ambaye anaujua ujumbe wa Mungu wa mwisho kwa siku hizi za mwisho.

Ni kweli hata leo kwamba watu wanapenda giza kuliko nuru kama vile ilivyokuwa wakati ule Yesu alipoihubiri [nuru]. Kama vile ilivyokuwa katika siku Zake [Kristo] uliletwa kwa watu ujumbe ule wa ukweli wa kuja Kwake mara ya kwanza, ndivyo leo ujumbe huu wa ukweli wa kuja kwake mara ya pili unavyokwenda ulimwenguni kote. Leo ni kweli kwamba "nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru." Sio lazima kufanya dhambi fulani kubwa sana ili KUPOTEA. KUKATAA kumfuata Kristo, yaani, KUKATAA KWENDA NURUNI, ni hakika kwamba kutasababisha KUPOTEA KABISA kwa roho [mtu] hiyo. Hebu na isiwe kweli kwa mtu ye yote asomaye maneno haya kwamba anapenda giza kuliko nuru. Kinyume chake, unapoona na kusikia na kusadiki ukweli wa ujumbe huu wa Mungu wa mwisho, basi, UUPOKEE kwa moyo wa furaha, ukiyaleta MAISHA yako kupatana nao.

## NURU KATIKA BIBLIA

"NENO lako ni TAA ya miguu yangu, Na MWANGA wa njia yangu" (Zaburi 119:105). "Kufafanusha MANENO yako kwatia NURU, na kumfahamisha mjinga" (fungu la 130)

Kwa hiyo, kila kitu kinachofundishwa kwa wazi katika Biblia ni NURU, na ni LAZIMA KIPOKEWE na watu wa Mungu endapo WATAKWENDA humo [nuruni].

## NURU KATIKA SHERIA

"Maana MAAGIZO [AMRI] hayo ni TAA, na SHERIA hiyo ni NURU, Na maonyo ya kumwadilisha mtu ni njia ya uzima" Mithali 6:23).

Cho chote kinachofundishwa katika SHERIA YA MUNGU [AMRI KUMI] na NENO LA MUNGU, kama ulivyo ujumbe huu ambao wewe unaendelea kuusoma, hakina budi KUFUATWA na KUPOKEWA moyoni mwako. Kutoupokea ujumbe huu kutakuwa ni kuikataa nuru na kweli, na hakuna Mkristo ye yote anayeweza kuthubutu kufanya hivyo.

## NURU KATIKA UNABII

"Nasi tuna lile NENO LA UNABII lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama TAA ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu" (2 Petro 1:19).

Hapa UNABII unaitwa TAA [NURU]. Basi, kwa kadiri unabii huo unavyoendelea kutimizwa na maana yake kufunuliwa, ni wazi kwamba wanadamu watabeba UWAJIBIKAJI wa kuzifuata na kuzikubali KWELI MPYA kama hizo zitakazofunuliwa nao [unabii]. Kwa kuwa unabii huu utaeleweka, kwa mujibu wa Danieli 12:4, "hata WAKATI WA MWISHO," basi, ni dhahiri kwamba katika wakati huu mawazo ya wanadamu hayana budi kuelekezwa kwenye NURU MPYA, yaani, kwenye UKWELI MPYA. Unabii ule wa Danieli unafunuliwa, na unatimizwa, na sisi tunaelewa MAANA yake. Jambo hilo linaweka mabegani mwetu WAJIBU WA KWENDA NURUNI, ambayo imo ndani ya [unabii] huo.

Unabii wa Kitabu cha Ufunuo pia unaendelea kutimizwa leo. Mungu anasema hivi kuhusu unabii huo: "Heri ASOMAYE na wao WAYASIKIAO maneno ya unabii huu, na KUYASHIKA yaliyoandikwa humo" (Ufunuo 1:3).

Kutokana na hayo ni dhahiri kwamba unabii wa Biblia unapozidi kufunuliwa kutakuwa na ufunuo wa kudumu kuhusu MAJUKUMU MAPYA, ambayo hayana budi KUTIIWA na watu wa Mungu.

## UTIMILIFU WA NURU KATIKA UJUMBE WA AINA TATU

Katika kitabu cha Ufunuo kuna unabii wa ujumbe huu wa aina tatu ambao UTAFUNGA KAZI YA INJILI (Ufunuo 14:6-12). Ujumbe huu unayafunua MAJUKUMU MAPYA. Umejengwa juu ya NENO LA MUNGU, SHERIA YA MUNGU, na UNABII WA BIBLIA. Una ukweli wa mbinguni kwa WAKATI HUU. Unakwenda ulimwenguni kote katika KIZAZI HIKI, na kazi hiyo itakapokwisha, MWISHO WA MAMBO YOTE ya ulimwengu huu UTAKUJA.

Katika hiyo "INJILI YA MILELE" umo WOKOVU kwa wale wanaoipokea, na ndani yake pia kuna nafasi kubwa ya kuingia katika ufalme wa Mungu. "HERI WALE WAZISHIKAO AMRI ZAKE, WAWE NA HAKI KUUENDEA HUO MTI WA UZIMA, NA KUINGIA MJINI KWA MILANGO YAKE" (Ufunuo 22:14, Tafsiri ya King James Version).

Wale wanaoukubali ujumbe huo wa mwisho, yaani, wanaoishika ile "IMANI YA YESU," na kwa imani hiyo KUZISHIKA AMRI ZAKE, wataingia katika mji wa Mungu. Ni HAKI yetu na WAJIBU wetu KUICHUNGUZA KWELI YA WAKATI HUU, na tunapojifunza ya kwamba hiyo ndiyo KWELI, basi, na TUIPOKEE na KUITII.

"Laiti mawazo yetu na shukrani vingepanda juu

Kama ubani wa shukrani kwenda mawinguni,

Na kupata toka kwake Kristo raha ile tamu

Ambayo hakuna mwingine aijuaye ila yule aionjaye.

Amani hii ya mbinguni ikiwa moyoni

Ndiyo ahadi bora sana ya raha ile tukufu,

Ambayo imesalia kwa Kanisa la Mungu,

Kikomo cha masumbuko, kikomo cha maumivu."

.